# USAWIRI WA MHUSIKA MKINZANI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN: *KINJEKETILE* (1969), *JOGOO KIJIJINI* (1976) NA *ARUSI* (1980)

**WILSON OLUCHILI**
**C50/20429/2022**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2024**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote ile katika chuo kikuu chochote.

Sahihi:……………………………….. Tarehe:………………………………

**Wilson Oluchili**

**C50/20429/2022**

## MSIMAMIZI

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yangu kama msimamizi niliyeteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:……………………………….. Tarehe:………………………………

**Dkt. Richard. M. Wafula**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu cha Kenyatta**

## TABARUKU

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi Elikanah Fanuel Atieli na Mable Okwemba Ayieta kwa kunipenda kwa dhati, kunisomesha na kuniombea kwa Mola kila kukicha.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na ulinzi kila uchao. Tangu nilipojitosa katika bahari ya masomo, mashua yangu yameyumbishwa na dhoruba na mawimbi makubwa. Hata hivyo hujaniacha asilani, umenibariki ukanipa uwezo, maarifa, hekima na ufahamu hadi nimekifikisha chombo hiki ukingoni. Naamini si tamati tu bali ni msingi wa safari nyingine unayonipangia. Sifa na utukufu zikurudie milele na milele.

Aidha, nawapa shukrani sufufu wazazi wangu Eli na Mable kwa kuwa nami bega kwa bega katika safari yangu ya masomo. Mmenilea kwa maadili mema, mkanisomesha na kunitia moyo mara kwa mara. Sitasahau dua zenu kwa Mungu ambazo zimenifungulia njia. Ufanisi wangu huu ni wenu daima. Nawaombea kwa Mungu maisha marefu yenye baraka na afya njema ili muweze kuyaonja matunda ya kazi yenu kwangu. Jua lenu la machweo liwe angavu lipenyezalo miale ya tabasamu na amani mioyoni mwenu. Nawashukuru sana ndugu zangu Beatrice, Alice, Francis, Loyce, Davis, Banstar, Aggrey na Erick kwa kunifaa kwa hali nyingi.

Pia, nampa shukrani za dhati msimamizi wangu Dkt. Wafula Richard. Umejitolea kwa udi na uvumba kunielekeza, kunishauri na kuniboreshea kazi hii kwa tajiriba yako ya kupigiwa mfano. Umejigharimu muda wako ili kuhakikisha ubora na upekee wa kazi hii umetimia. Kungekuwepo na msamiati bora zaidi ya shukrani basi ningeutumia kwako. Nakuombea kwa Mungu maisha marefu yenye ustawi na siha njema. Siwezi kumsaza Profesa Githinji Peter. Umekuwa mwenye thamani kubwa kwangu kwa ufanisi wangu huu wa uzamili tangu kujiunga kwangu chuoni. Umenionyesha upendo wa dhati

kwa kunishauri, kunielekeza na kunihimiza kila uchao. Kila ulipoona ishara za kutamauka ndani yangu, ulinihimiza nipige moyo konde. Sina cha kukulipa ila dua yangu kwa Mola ni akupe maisha marefu yenye baraka na afya bora.

Shukran za dhati vilevile ziwaendee wahadhiri walionifundisha; Dkt. Chacha, Dkt. Kamau, Profesa Githinji, Dkt. Wafula, Dkt. Masinde, Dkt. Arege, na Profesa King'ei. Mmenijaza maarifa na kuninoa makali katika Kiswahili. Maarifa yenu yameubambua utando uliokuwa umejinata kwenye ubongo wangu. Hakika, nitaisafiria dira hii mlionikabidhi kufika vilele vya pembe zote za taaluma hii. Sitawasaza Dkt. Jesse, Dkt. Kaui, Dkt. Beth na Dkt. Mburu kwa ushauri mwema na kunihimiza kujizatiti. Heri njema zenu na motisha mlionipa zilinigusa na kunitia shime katika safari hii. Mwenyezi Mungu awabariki. Wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili, nawashukuru sana kwa kunifaa kwa njia anuwai katika uzamili wangu. Nyinyi ni hidaya kubwa niliyowahi kutunukiwa na Maulana maishani mwangu. Tupa yenye maarifa mliojihami nayo imeninoa na kuyeyusha ubutu uliokuwa umeganda kwenye bongo langu. Msichoke kuwafaa wasomi wengine maana thawabu yenu kuu ipo kwa Mola.

Mwisho, shukrani za dhati ziwaendee wanafunzi wanzangu Maggret, Ruth, Ann, Linah, Stella, Dianah, na Fadhili kwa ushirikiano wenu. Mumekuwa wa msaada mkubwa sana kwangu katika safari hii. Mbali na hao, nawashukuru sana Steve, Evans na Mutiso kwa kunitia motisha, kunishauri na kunielekeza vyema. Nalikunja jamvi la shukrani kwa swahibu wangu, Vincent, Osayo, Roddin, Yakub na Hamisi. Mumenifaa kwa namna isiyo mithilika.

Kwenu nyote mlionifaa, nimewatungia shairi hili fupi kudhihirisha thamani yenu kwangu.

**‘HIJAWA RAHISI KWELI**

Mimi kufika tamati, ni kwa neema ya Mungu,
Ndipo nikaweka hati, kushukuru Mola wangu,
Mapenzi yako ya dhati, Yarabi Muumba mbingu,
‘Hijawa rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa.

Pili ni wazazi wangu, kunipa malezi mema,
Kunifadhili elimu, Eli baba Mebo mama,
Wakiwemo pia ndugu, wamekuwa wangu wema,
‘Hijawa rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa.

Tatu ni kwa wahadhiri, nikianza na Wafula,
Githinji ninakariri, ushauri kwa maswala,
King’ei sitojibari, Kamau pamwe Pamela,
‘Hijawa' rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa.

Chacha na Masinde hata, Osore na Jese' pia,
Kaui, Arege, Beta', Ndung'o na Mburu tilia'
Siachi Onyango hata, Eva, Japhe na Ngugia',
‘Hijawa' rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa,

Wanafunzi wenza pia, Magi, Wendo na Auma,
Wote walonidudia, Muindi naye kiplima',
Swahibu ‘kimalizia, Vini na Yakubu wema,
‘Hijawa' rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa.

Waja tulipoungana, ‘liondoka tafaruko,
Meno yalipoumana, chakula ‘lipata shuko,
Umoja jambo la ma’na, ndipo ‘kafika niliko,
‘Hijawa rahisi kweli, kwa mimi kufika hapa.

**IKISIRI**

Utafiti huu umechunguza usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein; *Kinjeketile* (1969), *Jogoo Kijijini* (1976) na *Arusi* (1980). Mhusika mkinzani ni mhusika ambaye huenda kinyume cha maadili ya jamii yake au kukinzana na mhusika nguli katika kazi ya fasihi. Katika kufanya hili, mkinzani hukuza kutoelewana au mgogoro katika utungo wa kifasihi. Malengo yaliyonuiwa kutekelezwa ni; kubainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule, kuchunguza namna mhusika mkinzani anavyokuza mgogoro katika tamthilia teule na kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Nadharia mbili ndizo zilizoongoza utafiti huu; Naratolojia na nadharia ya Drama. Naratolojia iliasisiwa na Plato (1930) na kukuzwa na Rimmon-Kennan (1983), Stanzel (1984), Phelan (1987) na Keen (2003). Inahusika na vipengele vya usimulizi vikiwemo wakati, nafsi, nafasi, wahusika na maudhui. Vipengele vya wahusika na namna wanavyokuza maudhui ndivyo vilivyotufaa katika utekelezaji wa lengo la kwanza na la tatu. Naratolojia inafafanua kuhusu njia za kuwasawiri wahusika na vilevile kueleza kuhusu wahusika kama vyombo vya kuwasilishia ujumbe (maudhui). Hata hivyo, swala la ukuzaji wa mgogoro na mhusika mkinzani halielezeki vyema na nadharia ya Naratolojia. Hivyo, nadharia ya Drama iliyoasisiwa na Carl Jung (1964) ndiyo iliyotuongoza katika kutekeleza lengo la pili. Nadharia hii ya Drama inahusu matendo ya wahusika katika drama na namna yanavyopelekea kuzuka kwa migogoro. Sampuli iliteuliwa kwa mbinu ya kimaksudi ambapo tamthilia mbili; *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini* ziliteuliwa kimaksudi ili kuchunguza usawiri wa mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Kwa upande mwingine, tamthilia ya *Arusi* iliteuliwa ili kuchunguza usawiri wa mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa. Data ilikusanywa maktabani ambapo tasnifu, majarida na makala mbalimbali yanayohusiana na mada hii yalisomwa kwa kina. Aidha data ya kimsingi ilitoka katika tamthilia teule ambazo zilisomwa na kuchanganuliwa kwa umakini na uzingativu mwingi. Hoja zinazohusiana na mkinzani zilitengwa katika mada ndogondogo, zikachanganuliwa kisha kufafanuliwa kwa maelezo yaliyoambatanishwa na dondoo mwafaka kutoka katika tamthilia teule. Jumla ya ripoti ya utafiti huu imesukwa katika sura tano. Matokeo ya kazi hii yanatarajiwa kuwafahamisha wasomi kuhusu mbinu mbalimbali za kumsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia pamoja na nafasi yake katika ukuzaji wa mgogoro na maudhui. Utafiti uligundua kwamba, mhusika mkinzani katika tamthilia anaweza kuwasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa au kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Mhusika mkinzani anapowasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa, huzua ukinzani kutokana na wanachokisema wahusika wengine au msimulizi kuhusu matendo yake. Haya yalibainishwa katika tamthilia za *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini*. Aidha, iligundulika kuwa mhusika mkinzani anapowasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa, huzua ukinzani kutokana na mazungumzo na matendo yake ya moja kwa moja kama ilivyobainika katika *Arusi.* Mbinu ambazo mhusika mkinzani amesawiriwa nazo katika tamthilia teule ni pamoja na ya kuwatumia wahusika wengine, ya kinatiki, ya kimaelezo na ya ulinganuzi na usambamba. Pia, mkinzani amebainika kuwa nguzo muhimu katika ploti ya tamthilia kwani huchochea migogoro mikuu katika drama. Mbali na hayo, utafiti umeonyesha kwamba, katika tamthilia teule, mhusika mkinzani ametumiwa na mtunzi kama chombo cha kuwasilishia maudhui makuu, kama vile udhalimu, ukatili, usaliti, siasa na utawala kwa ujumla.

## ABSTRACT

This research sought to analyse an antagonist as a character in the selected plays of Ebrahim Hussein; *Kinjeketile* (1969), Jogoo *Kijijini* (1976) and *Arusi* (1980). An antagonist is an opposing force in a story or a play. He is a character who goes against the morals of his society or opposes the protagonist in a piece of art. By so doing, he causes conflicts with other characters in the play. The objectives that guided the study are; to discuss various ways of portrayal of an antagonist in the selected plays, to analyze how an antagonist generates conflicts in the selected plays and to evaluate the themes developed by an antagonist in the selected plays.Two theories were used to guide this research; Narratology and Drama theory. Narratology was invented by Plato (1930) and later developed by Rimmon-Kennan (1983), Stanzel (1984), Phelan (1987) and Keen (2003). It analyses aspects of narration in literature such as narrative time, character and characterization, space, focalization and narrative voice. Character and characterization was the point of focus in this research. Therefore, Narratology guided the reseacher in the analysis of the objectives regarding the portrayal of an antagonist and the themes developed by the antagonist in the selected texts. This is because this theory's tenets explain ways of character portrayal and how a charater generates themes. Narratology does not effectively analyse the aspect of conflict, hence the need for another appropriate theory. Drama theory which was invented by Carl Jung (1964) was therefore used to elaborate how an antagonist develops conflicts in drama. This helped in analysing the second objective. The study sample was selected purposively where the two plays; *Kinjeketile* and *Jogoo Kijijini* were chosen to analyse an antagonist as an absent character on stage. On the other hand, *Arusi* was selected purposively too to analyse an antagonist as a present character on stage. The research was library based where articles, theses and relevant information from the internet were read and critically analyzed. Primary data was obtained from the selected texts which were critiqued to get the results of this research. Issues and statements on the antagonist were isolated and categorized thematically, analysed and elaborated descriptively. Scholars will benefit from this reseach by being shown various ways of portrayal of an antagonist, themes and conflicts generated by an antagonist in selected plays. The report was presented in five chapters. This research found out that, an antagonist in a play can be depicted as an absent or present character on stage. When an antagonist is depicted as an absent character on stage, he creates antagonism through what other characters on stage or the narrator say about him. This was what was found out as a result of analysis in *Kinjeketile* and *Jogoo Kijijini*. On the other hand, when an antagonist is depicted as a present character on stage, he creates antagonism through his utterances, actions and partly what other characters say about him. This was what the researcher found in *Arusi*. Generally, the ways of portrayal of an antagonist that were found out in the selected plays were; the use of a character to explain a character, comparing and contrasting and the reader's point of view. Also, the research found out that, an antagonist is a pillar of a play's plot since he plays a big role in the creation of major conflicts which develops a play and makes it dramatically important. Futhermore, it was found out that an antagonist has been used by the author as a channel of conveying thematic message. Among the themes discussed are betrayal, neo- colonialism, arrogance and oppression.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Mhusika nguli**: Ni mhusika ambaye anawakilisha maadili ya jamii na anghalau huwa mhusika mkuu.

**Mhusika mkinzani**: Ni mhusika ambaye huenda kinyume na maadili ya jamii yake au kukinzana na mhusika nguli katika kazi ya fasihi.

**Mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa**: Ni mhusika ambaye hajitokezi popote jukwaani ila athari ya matendo yake hudhihirika kupitia wanachokisema wahusika wengine kwenye jukwaa au msimulizi kumhusu.

**Mhusika aliyepo kwenye jukwaa**: Ni mhusika ambaye anatagusana moja kwa moja na wahusika wengine jukwaani kupitia matendo na mazungumzo yake.

**Usawiri wa mhusika**: Ni uchoraji, ubebeshaji, na ufafanuzi wa mhusika ili kumwezesha kutenda matendo yake kwa misingi ya maudhui aliyodhamiria mtunzi katika kazi maalum ya kifasihi.

**Mgogoro**: Ni mkinzano, mgongano au kutoelewana kwa pande mbili au zaidi za wahusika katika tungo za fasihi.

**Piramidi ya Freytag**: Ni umbo lenye sehemu tano zinazoelezea mgogoro katika ploti ya tungo za kifasihi. Sehemu hizi ni utangulizi, utata, kilele, mshuko na kiliwazo.

# YALIYOMO

**UNGAMO** .................................................................................................. **ii**
**TABARUKU** .................................................................................................. **iii**
**SHUKRANI**.................................................................................................. **iv**
**IKISIRI**.................................................................................................. **vii**
**ABSTRACT** .................................................................................................. **viii**
**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU** ....................................................... **ix**
**YALIYOMO** .................................................................................................. **x**
**SURA YA KWANZA**.................................................................................... **1**
**UTANGULIZI** .................................................................................................. **1**
1.0 Usuli wa Mada .................................................................................... 1
1.1 Suala la Utafiti .................................................................................... 6
1.2 Malengo ya Utafiti ................................................................................ 7
1.3 Maswali ya Utafiti................................................................................ 7
1.4 Umuhimu wa Utafiti ............................................................................. 8
1.5 Sababu za Kuchagua Mada..................................................................... 8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada.................................................................. 9
1.6 Upeo na Mipaka.................................................................................. 15
1.8 Misingi ya Nadharia............................................................................ 16
1.8.1 Nadharia ya Naratolojia ................................................................ 16
1.8.2 Nadharia ya Drama ...................................................................... 19
1.9 Mbinu za Utafiti.................................................................................. 21
1.9.1 Eneo la Utafiti.............................................................................. 21
1.9.2 Uteuzi wa Sampuli........................................................................ 21

1.9.3 Ukusanyaji wa Data ........ 22

1.9.4 Uchanganuzi wa Data ........ 22

1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo ........ 24

1.10 Maadili ya Utafiti ........ 24

**SURA YA PILI ........ 25**

**USAWIRI WA MHUSIKA MKINZANI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN ........ 25**

2.0 Utangulizi ........ 25

2.1 Maisha ya Ebrahim Hussein Yanavyoibua Muktadha wa Ukinzani katika Tamthilia zake Teule ........ 25

2.2 Mhusika Mkinzani kama Mhusika Asiyekuwepo kwenye Jukwaa ........ 28

2.3 Mhusika Mkinzani kama Mhusika Aliyepo kwenye Jukwaa ........ 33

2.4 Mbinu za Usawiri wa Wahusika ........ 33

2.5 Muhtasari wa Tamthilia ya *Kinjeketile* ........ 34

2.5.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Kinjeketile* ........ 35

2.6 Muhtasari wa Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ........ 36

2.6.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ........ 39

2.7 Muhtasari wa Tamthilia ya *Arusi* ........ 39

2.7.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi* ........ 41

2.8 Usawiri wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Kinjeketile* ........ 41

2.9 Usawiri wa Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ........ 47

2.10 Usawiri wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi* ........ 52

2.11 Hitimisho ........ 55

**SURA YA TATU ........ 57**

**MHUSIKA MKINZANI NA UKUZAJI WA MGOGORO KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN ........................................ 57**

3.0 Utangulizi.............................................................................................. 57

3.1 Dhana na Aina za Migogoro ..................................................................... 57

3.2 Hali Zinazochochea Mgogoro baina ya Wahusika .................................... 59

3.3 Namna Mkinzani Anavyokuza Mgogoro.................................................. 61

3.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro Katika Tamthilia ya *Kinjeketile* ........................................................................................... 64

3.4.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani ........................................... 64

3.4.2 Matatizo Anayosababisha Mhusika Mkinzani........................... 66

3.4.3 Mtagusano wa Mkinzani na Wahusika Wengine....................... 67

3.4.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Kinjeketile*.............. 68

3.5 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro katika *Jogoo Kijijini* .......... 71

3.5.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani ........................................... 72

3.5.2 Matatizo Yanayoletwa na Mhusika Mkinzani ........................... 73

3.5.3 Mandhari Anayoumba Mhusika Mkinzani ................................ 74

3.5.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Jogoo Kijijini*........ 75

3.6 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro katika Tamthilia ya *Arusi* ... 78

3.6.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani ........................................... 79

3.6.2 Mtagusano wa Mhusika Mkinzani na Wahusika Wengine........ 81

3.6.3 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Arusi* ...................... 83

3.7 Hitimisho............................................................................................... 85

**SURA YA NNE ............................................................................................ 86**

**MAUDHUI YANAYOIBULIWA NA MHUSIKA MKINZANI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN ........................................ 86**

4.0 Utangulizi.............................................................................................. 86

4.1 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Maudhui ............ 86
4.2 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Kinjeketile* ............ 88
4.2.1 Dhulma na Unyanyasaji ............ 88
4.2.2 Ukatili ............ 91
4.2.3 Ufisadi ............ 92
4.2.4 Usaliti ............ 93
4.3 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ............ 94
4.3.1 Mateso ............ 94
4.3.2 Mashaka (Hofu) ............ 96
4.3.3 Ubinafsi ............ 98
4.3.4 Ukoloni na Ukoloni Mambo-leo ............ 98
4.4 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi* ............ 100
4.4.1 Ndoa ............ 100
4.4.2 Utamaduni ............ 101
4.4.3 Usaliti ............ 103
4.4.4 Ukatili ............ 104
4.4.5 Siasa ............ 105
4.5 Hitimisho ............ 106
**SURA YA TANO ............ 107**
**MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ............ 107**
5.0 Utangulizi ............ 107
5.1 Muhtasari wa Utafiti ............ 107
5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo ............ 109

5.3 Mchango wa Utafiti .......... 114
5.4 Changamoto Zilizokabili Utafiti .......... 114
5.5 Mapendekezo ya Utafiti .......... 115
**MAREJELEO .......... 116**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Wahusika ni uti wa mgongo wa kazi ya fasihi hasa tamthilia riwaya na hadithi fupi kwa kuwa ndio wanaoendesha matukio katika utungo mzima wa kifasihi. Bila wahusika, vipengele vingine vyote katika kazi ya fasihi kama vile maudhui, migogoro, dhamira, ploti na fani haviwezi kukuzwa vizuri. Watunzi wa kazi za sanaa huwatumia wahusika kama vyombo vya kuwasilishia yote wanayodhamiria katika tungo zao. Dhana ya mhusika imefasiriwa na wataalam mbalimbali kwa madhumuni ya kuonyesha nafasi yao katika kazi ya kifasihi.

Wamitila (2003) anafasili mhusika kama kiumbe anayepatikana katika kazi za fasihi na ambaye anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Anazidi kufafanua mhusika kama "binadamu" katika kazi za fasihi aliye na sifa za kitabia, kiitikadi, kifalsafa na kimaadili ambazo zinatambulishwa na usemi wake na matendo yake.

Kwa upande mwingine, Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa, wahusika ni viumbe wa kisanaa wanaobuniwa katika mazingira ya msanii. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kitamaduni, kijografia, kihistoria au kijamii. Senkoro (2011) kwa upande wake anaeleza dhana ya wahusika kuwa watu au viumbe ambao wamenuiwa kutumiwa kuwakilisha tabia, dhana, ama mawazo ya watu katika tungo za kifasihi.

Fasili ya Senkoro na Wamitila zinabainisha kuwa wanasisitiza mhusika kama kiwakilishi cha maadili, tabia, itikadi na falsafa ya binadamu. Kwa ujumla, mhusika ni

kiumbe ambaye hupatikana katika kazi ya kifasihi na anaweza kuwa mnyama, binadamu, hali, zimwi au kitu chochote kile ambacho hutumiwa na mwandishi kuendesha matukio katika kazi ya fasihi.

Wapo wahusika wa aina mbalimbali katika kazi za kifasihi. Wamitila (2002) anaainisha mhusika mkuu, mhusika msaidizi, bapa, nguli, na mhusika mkinzani (mpinzani). Anazidi kueleza kuwa, mhusika nguli ni mhusika ambaye huwakilisha maadili ya jamii ambayo mara nyingi huwa ndio falsafa ya mtunzi. Nguli huwa ndiye mhusika mkuu kwa kuwa ndiye atumikiwaye kotekote kusambaza ujumbe alioudhamiria mtunzi. Kwa upande mwingine, anamfafanua mhusika mkinzani kama mhusika ambaye huenda kinyume na maadili ya jamii yake au anayekinzana na mhusika nguli. Utafiti huu basi umejikita kwa mhusika mkinzani kwa kuchunguza namna alivyosawiriwa katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein.

Dhana ya usawiri wa wahusika imefasiriwa kwa upana na wataalam wengi. BAKIZA (2010) wanaeleza kuwa "sawiri" ni kitendo cha kuumba sura ya kitu, mtu au jambo katika akili. Ponera (2014) naye anafafanua dhana ya usawiri wa wahusika kuwa kitendo cha kuwachora, kuwatambulisha, kuwafafanua na kuwakuza wahusika huku ukiwapa usemi, matendo, na uwezo unaolandana nao. Majina wanayopewa wahusika, lugha pamoja na matumizi yake kifasihi hujumuisha dhana hii ya usawiri. Kwa ujumla, usawiri wa wahusika ni uchoraji, ubebeshaji, na ufafanuzi wa wahusika ili kuwawezesha kutenda matendo yao kwa misingi ya maudhui aliyodhamiria mtunzi katika kazi maalum ya kifasihi.

Wataalam wengi wamethibitisha kuwa utanzu wa tamthilia una upekee fulani kwa misingi ya wahusika, usimulizi na hata lugha inayotumika ikilinganishwa na tanzu zingine kama riwaya na hadithi fupi. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa tamthilia huwa na pande mbili au zaidi za wahusika wanaogongana ambao huiga masimulizi fulani. Uigizaji na mazungumzo ya wahusika ndio nguzo itegemewayo na tamthilia katika uwasilishaji wa ujumbe wake. Haya hutekelezwa na wahusika na tendo kuu la kidrama hukuzwa na kuendelezwa kwa mazungumzo na uigizaji huu wa wahusika.

Wamitila (2008) anazidi kubainisha upekee wa tamthilia kwa madai kuwa sio tu utunzi pekee unaoshikilia drama bali pia uigizaji, jukwaa, uangazaji wa jukwaa, mitagusano ya waelekezi na waigizaji (wahusika) wenyewe. Mwanadrama huwasiliana na hadhira yake kupitia kwa wahusika. Anasisitiza kuwa mgogoro huchukua sehemu kubwa katika tamthilia kwa kuwa ndio nguzo kuu ya kuwepo kwa tendo la kidrama ambalo huifanya drama isonge mbele. Migogoro hii huibuliwa na wahusika wanapogongana katika mazungumzo na matendo baina yao. Migongano baina ya mhusika mkinzani na wahusika wengine basi ndicho kiini cha utafiti huu.

Mhusika mkinzani anaweza kuelezewa vyema kwa kurejelea usuli wa fasihi andishi ya kimagharibi tangu enzi za Aristotle. Betti (2015) anamrejelea Aristotle (1920) na kumzungumzia mhusika mkinzani kwa upana. Anaeleza kuwa mhusika mkinzani alihusishwa na tamthilia za tanzia katika fasihi ya awali. Kulingana na Aristotle, tanzia ni aina ya tamthilia ambayo inahusu mhusika mkuu anayekumbwa na janga kuu na huwa na matukio ya kitanzia. Huhusisha maigizo ya huzuni yanayoibua huruma. Licha ya hayo, huwa na matumaini ya kuiona kesho nzuri. Betti ananukuu kauli ya Aristotle

aliyedai kuwa tanzia inahusu miigo kupitia matendo wala sio masimulizi. Matendo haya yanatekelezwa na mhusika katika tamthilia. Aristotle alitoa maelezo haya akirejelea tanzia zilizoigizwa kila mwaka huko Athens karne ya sita kabla ya Kristo na kuendelea mbele.

Betti anazidi kusema kuwa kimsingi wahusika wanaweza kuainishwa kwa makundi mawili ambayo ni nguli na mkinzani. Aghalabu, tamthilia huwa na mhusika nguli mmoja ambaye anawakilisha maadili ya jamii mahususi, naye mkinzani anasababisha mgogoro anapoenda kinyume na maadili ya jamii yake. Aristotle (1920) anaeleza kuwa, mhusika nguli katika tanzia halisi ni shujaa na ni mtu maarufu na wa tabaka la juu katika jamii yake.

Katika fasihi ya kisasa, dhana hii ya mhusika nguli na mkinzani ilianza kuingizwa katika aina zingine za tamthilia kama vile futuhi, melodrama na tanzia za kisasa zisizohusisha mashujaa. Katika tamthilia za aina hii nguli anakinzwa na mhusika mkinzani anapokuwa katika juhudi zake za kutekeleza mambo fulani. Kila anapotenda mema hupata upinzani kutoka kwa mkinzani. Utafiti huu basi utamchunguza mhusika mkinzani katika tamthilia ya tanzia halisi na zisizo za tanzia. Tanzia halisi iliyoteuliwa ni *Kinjekitile* nayo *Jogoo kijijini* na *Arusi* ndizo zisizo za tanzia zilizoteuliwa kimaksudi kuchunguzwa.

Mhusika mkinzani katika melodrama anasawiriwa kuwa mwenye matendo maovu dhidi ya nguli na mwishowe hukosa fursa ya kuyaungama, kwa hivyo hubaki katika hali ya kuteseka kimawazo katika matamanio yake ya kutaka kuungama (Betti, 2015).

Mtaalamu huyu anabainisha kuwa, kufikia sasa mhusika mkinzani anaweza kubainika katika aina zote za tamthilia licha ya kwamba hapo awali, alihusishwa na tanzia pekee. Vilevile, amepenya katika tungo zingine za kifasihi kama riwaya, na hadithi fupi. Hata hivyo, anavyosawiriwa katika tamthilia inakuwa na upekee fulani ikilinganishwa na ilivyo katika riwaya au hata hadhithi fupi. Hii ni kwa sababu tamthilia huhusisha sana matendo na maigizo baina ya wahusika kinyume na tungo za kinathari zinazojikita sana kwenye masimulizi. Kutokana na hayo, mtafiti alikuwa na msukumo wa kulenga tamthilia kwa kuchunguza namna mhusika mkinzani alivyosawiriwa katika utanzu wa tamthilia.

Zaidi ya hayo, mhusika mkinzani anaweza kuwasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa au mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Rosefeldt (2002) anafafanua mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa kama mhusika ambaye hajitokezi popote jukwaani ila athari ya matendo yake hudhihirika moja kwa moja katika drama kupitia wanachokisema wahusika wengine kwenye jukwaa au msimulizi kumhusu. Rosefeldt anazidi kueleza kuwa mhusika mkinzani akiwasilishwa katika sura hii ya kutokuwepo jukwaani huwa ndiye nguzo ya ploti ya drama kwa kuwa ndiye ajengaye kiini cha mgogoro na ukinzani katika drama. Wahusika katika drama wanaohusiana naye katika drama au wanaomuunga mkono, hutenda matendo yao kutokana na msukumo ndani kutoka kwa mhusika huyu mkinzani.

Carlson (2016) naye anasema kuwa wahusika wasiokuwepo kwenye jukwaa katika drama za Kigiriki walikuwa miungu ambao walibariki au kulaani wahusika halisi kwenye jukwaa na vilevile kuathiri mustakabali wao. Katika drama za kisasa, wanaweza

kuwa binadamu waliokufa, wanyama au viumbe walio hai. Athari ya matendo yao hudhihirika moja kwa moja au kupitia wanachokisema wahusika wengine akiwemo msimulizi kuwahusu katika drama.

Rosefeldt na Carlson wanamtaja mhusika aliyepo kwenye jukwaa kama anayetagusana na wahusika wengine jukwaani moja kwa moja na kuathiri drama kupitia matendo na usemi wake. Katika utafiti huu mhusika mkinzani amechunguzwa katika *Kinjeketile* kama asiyekuwepo kwenye jukwaa ila athari za matendo yake zinabainika moja kwa moja kutokana na wanachokisema wahusika wengine kumhusu. Kwa upande mwingine, katika *Jogoo Kijijini*, mhusika mkinzani amechunguzwa kama asiyekuwepo kwenye jukwaa bali anazua ukinzani kutokana na anachokisema msimulizi kuhusu matendo yake. Katika *Arusi*, mkinzani amechunguzwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa.

Kwa ujumla, mhusika mkinzani katika tamthilia teule amechanganuliwa kama aliyepo au asiyekuwepo kwenye jukwaa. Mchakato wa vipengele hivi vyote vinavyomzunguka mhusika mkinzani vikiwemo, sura alizowasilishwa nazo, utendaji na unenaji wake na nafasi yake katika ukuzaji wa mgogoro na maudhui, ndicho kichocheo kilichompa mtafiti shime ya kumchunguza katika tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*.

### 1.1 Suala la Utafiti

Wahusika wanabainika kuwa mhimili dhabiti katika kazi za fasihi kutokana na namna wanavyoendesha matukio yote katika tungo zenyewe. Swala la usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi limeshughulikiwa na watafiti mbalimbali huku wakichukua mitazamo tofautitofauti katika tafiti zao. Kutokana na uchunguzi wa mtafiti, inabainika

kuwa tafiti za awali kuhusu usawiri wa wahusika zimejikita kwenye wahusika wa kike, wa kiume, watoto, walemavu na wahusika kwa ujumla ambao si wakinzani. Mhusika mkinzani ametajwa tu kijuujuu katika tafiti zao. Kadri ya ujuzi wa mtafiti na utafiti wa awali, hakuna utafiti wa kina ambao umefanywa kuhusu usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia za Ebrahim Hussein: *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*. Bila mkinzani, mafanikio ya nguli na wenzake yatakuwa finyu. Ni vipi kuwepo kwa mkinzani hufanikisha na kukamilisha usanii wa tamthilia hizi kisanaa? Hili ndilo pengo linalochochea mtafiti kuzama katika utafiti huu ili kuliziba.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

Malengo yafuatayo ndiyo yaliyoongoza utafiti huu:

i. Kubainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi.*

ii. Kuchunguza namna mhusika mkinzani anavyokuza mgogoro katika tamthilia za *Kinjeketile, Jogoo Kijijini* na *Arusi*.

iii. Kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi.*

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Kutokana na malengo ya utafiti yaliyotajwa hapo juu, utafiti huu ulikusudia kujibu maswali yafuatayo:

i. Ni mbinu zipi za usawiri wa mhusika mkinzani zimetumika katika tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*?

ii. Ni kwa jinsi gani mhusika mkinzani amekuza mgogoro wa tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*?

iii. Ni maudhui yepi yameibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*?

**1.4 Umuhimu wa Utafiti**

Utafiti huu unatarajiwa kuwafahamisha wasomi kuhusu mbinu mbalimbali zinazotumiwa kumsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia. Umuhimu wa mhusika mkinzani katika tamthilia na kazi za kifasihi kwa ujumla unatarajiwa kubainika kutokana na utafiti huu. Aidha, utachangia kuweka msingi dhabiti wa kuendeleza mchakato wa kuchunguza dhana ya mhusika ikiwemo usawiri wa wahusika wa aina tofautitofauti katika utanzu wa tamthilia au hata tanzu zingine kama riwaya na hadithi fupi.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Sababu mojawapo ya kuchaguliwa kwa mada hii ni kwamba, wahusika ndio nguzo ya utungo wowote ule wa kazi ya kifasihi kwa kuwa matukio yote huendeshwa kupitia kwao. Katika tamthilia matukio huendelezwa na matendo yanayotendwa na wahusika. Mkinzani anapotenda matendo yanayoenda kinyume na maadili ya jamii, mivutano baina yake na wahusika wegine hutokea. Hii ndio dira inayoongoza tamthilia. Haya yalimchochea mtafiti kuteua mada hii. Mhusika ni kipengele cha fasihi kisichoepukika kwa hivyo, utafiti juu yake utaendelea kufanyika.

Aidha, katika sanaa ya maigizo kwa ujumla mhusika mkinzani hubainika kuwa na jukumu kubwa la kuzua mgogoro katika maigizo husika. Haya hujenga taharuki, msisimko na kukuza ploti ya kazi husika. Kutokana na umuhimu wa mhusika mkinzani katika sanaa ya fasihi kwa ujumla ndipo mtafiti amechagua mada hii.

Sababu nyingine ya kuteua mada hii ni kuwa swala la mhusika mkinzani halijatafitiwa kwa kina na watafiti wengine hasa katika tanzu mbalimbali za fasihi ya Kiswahili. Kuna haja kubwa ya kulizungumzia swala hili. Mada hii imebainisha vyema umuhimu wa kuwepo kwa mhusika mkinzani katika kazi za fasihi ambaye kupitia kwake ndipo migogoro mikuu na maudhui vinakuzwa.

## 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu swala la usawiri wa wahusika kwa kuzingatia mikabala tofautitofauti. Sehemu ifuatayo ni muhtasari wa tafiti za wasomi mbalimbali ambazo zilitoa mchango katika utafiti huu na kumwezesha mtafiti kubainisha pengo la utafiti.

Mukobwa (1985) ametafiti kuhusu swala la maudhui katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein ambazo ni *Mashetani, Kinjeketile*, *Wakati Ukuta, Alikiona na Arusi*. Katika utafiti wake, amebainisha maudhui yaliyoangaziwa na Hussein katika tamthilia hizo. Katika *Kinjeketile* amebainisha maudhui ya kihistoria kama maudhui makuu nayo *Arusi* ameielezea kama tamthilia ya kimafumbo inayoangazia maswala ya kisiasa, kiuchumi, kiitikadi na kitamaduni. Ufafanuzi wa tamthilia hizi kwa kina uliofanywa katika utafiti huo ulimsaidia mtafiti kufahamu ujumbe unaowasilishwa na Hussein katika tungo hizo.

Utafiti wa Mukobwa uliegemea kwa kipengele cha maudhui nao huu ukaegemea kwenye mhusika mkinzani katika tamthilia mahususi za Hussein ambazo ni *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi*.

Bowen (2003) ameshughulikia usawiri wa wahusika watoto katika *Visiki* (1984) na *Amezidi* (2000) katika utafiti wake. Kazi hii inabainisha kuwa usawiri tunaopata kuhusu mhusika fulani ni kutokana na kile anachokisema mwandishi kumhusu, wanachokisema wahusika wengine kumhusu na kile ambacho mhusika mwenyewe anasema na kutenda. Kipengele cha uhusiano kati ya mhusika na lugha kinabainika kuwa muhimu sana katika kumsawiri. Wahusika watoto wamesawiriwa kwa mbinu za maelezo ya mwandishi, wahusika kujielezea au kuelezewa na wengine pamoja na matumizi ya majina ya kimajazi kama Majaaliwa na Amina katika *Visiki* (1984). Utafiti huu ulikuwa na nafasi katika utafiti huu katika kuchanganua mbinu za kusawiri wahusika na uhusiano kati ya lugha na mhusika. Licha ya haya, utafiti wa Bowen ni tofauti na huu kwa kuwa amejikita katika usawiri wa wahusika watoto nao huu ulishughulikia usawiri wa mhusika mkinzani.

Arege (2012) ametafiti kuhusu naratolojia katika ushairi simulizi akijikita kwenye utenzi wa Rasi ʼ*Lghuli*. Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya Naratolojia ambapo alishughulikia vipengele vitatu vya naratolojia. Vipengele hivi ni pamoja na wakati, wahusika na uhusika, na nafsi. Hata hivyo kipengele cha wahusika ndicho muhimu kwenye utafiti wetu. Kipengele hiki kinashughulikia namna ya kuwasawiri wahusika ambapo Arege (2012) katika utafiti wake alibainisha kuwa wahusika husawiriwa aidha kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Ameweka wazi kuwa njia ya

moja kwa moja huhusisha anachokisema msimulizi au wahusika wengine kumhusu mhusika maalum. Kwa upande mwingine, njia isiyo ya moja kwa moja huhusisha matendo ya mhusika, usemi wake, mandhari anamopatikana, mwonekano wake na mengine. Utafiti huu kwa ujumla ulitoa mchango mkubwa kwetu kinadharia na vilevile katika utekelezaji wa malengo yetu ya mbinu za kumsawiri mhusika mkinzani na namna anavyokuza maudhui. Hata hivyo utafiti huu na wa Arege unatofautiana kwa kuwa wake umeshugulikia swala la naratolojia kwa ujumla katika ushairi nao huu unashughulikia usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia.

Barasa (2013) alichunguza wahusika na uhusika katika riwaya ya *Watu wa Gehena* (2012). Utafiti wake ulibainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa wahusika zikiwemo mbinu za kidrama, ulinganuzi na mgotanisho pamoja na majazi. Vilevile alibainisha kuwa mtindo wa riwaya umejengwa kwa kiasi kikubwa na wahusika. Majibizano na mazungumzo ya wahusika hawa yanaakisi uhalisia. Vilevile, lugha wanayoitumia imefungamanishwa na mazingira yao. Nadharia ya umtindo iliyotumika hapa imebainisha kuwa kupitia kigezo cha mazungumzo baina ya wahusika, usawiri wao unakuza mtindo na uwasilishaji wa maudhui katika utungo wa *Watu wa Gehena*. Mwandishi amewapa lugha teule na kuwasawiri kwa ubunifu mkubwa. Utafiti huu ulitoa mchango mkubwa kwetu katika kuelezea mbinu za usawiri wa wahusika na namna wanavyokuza maudhui. Hata hivyo, utafiti huu unatofautiana na wetu kwa kuwa Barasa (keshatajwa), alishughulikia utanzu wa riwaya na wahusika kwa ujumla ilhali wetu ulijikita katika tamthilia kwa kuegemea mhusika wa aina moja, yaani mkinzani.

Oiko (2017) ameshughulikia uhakiki wa mtindo katika tamthilia za Arege; *Kijiba cha Moyo* (2009), *Mstahiki Meya* (2009) na *Chamchela* (2011). Ameeleza kuwa msuko, dhamira, maudhui na wahusika ndizo nguzo zinazojenga fasihi. Hata hivyo itakuwa vigumu kuviwasilisha bila lugha. Haya yote yanafanikishwa na wahusika. Kwa kuongozwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo, amebaini kuwa mtindo wa kinaya na kejeli umetumiwa na Arege kuwasilisha ujumbe katika tamthilia zake zilizotafitiwa. Vilevile amebaini kuwa lugha ndicho chombo muhimu kinachoweza kutumiwa na waandishi kueleza ujumbe wao. Kazi hii ilichangia utafiti huu katika kueleza namna mhusika mkinzani anavyotumia lugha katika kuwasilisha ujumbe (maudhui) uliokusudiwa na mwandishi katika tamthilia teule.

Haji (2018) ametathmini mbinu za usawiri wa wahusika katika *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) na *Asali Chungu* (1978). Mbinu ya kidrama, kitaharuki, kuwatumia wahusika wengine, uzungumzi nafsi na nyinginezo ndizo alizobainisha katika riwaya hizo. Aligundua kuwa kulingana na hulka na matendo ya wahusika wenyewe, mbinu hizo huibua aidha matendo mema au maovu. Kutokana na uchunguzi huu mtafiti alipata ufahamu kuhusu mbinu za usawiri wa wahusika na jinsi zinavyoibua matendo ya wahusika. Tofauti iliopo kati ya utafiti wa Haji (keshatajwa) na huu ni kuwa yeye alishughulikia kutathmini usawiri wa wahusika kwa ujumla. Vilevile, alifanya utafiti katika riwaya nao huu ulihusu usawiri wa mhusika wa aina moja ambaye ni mkinzani katika tamthilia. Pamoja na hayo, utafiti wake uliongozwa na nadharia za fasihi-linganishi na nadharia ya mwitikio wa msomaji nao huu uliongozwa na nadharia ya Drama na ya Naratolojia.

Oluoch (2020) ametafiti kuhusu migogoro za kisaikolojia katika riwaya za *Mkama Ndume* (2004) na *Unaitwa Nani?* (2008). Uchunguzi wake ulibainisha kuwa ni vigumu kuwakuza wahusika bila kuwepo kwa migogoro. Aidha migogoro hii kati ya wahusika husaidia mwandishi katika kukuza maudhui na ploti ya kazi ya fasihi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mkama Ndume*, mtunzi ametumia migogoro ya kimawazo kukuza maudhui kama vile tamaa, unyanyasaji, kukata tamaa na mengine. Kazi hii ilitoa mchango kwa utafiti huu kwa kuwa inaweka msingi wa vyanzo vya migogoro baina ya wahusika na namna ambavyo inapelekea kuibua maudhui mbalimbali katika kazi ya fasihi. Utafiti wake unatofautiana na huu kwa kuwa ulijikita kwa mgogoro pekee nao huu unajikita kwenye mhusika mkinzani na namna anavyokuza migogoro na maudhui katika tamthilia teule.

Bakize (2021) ametafiti kuhusu usawiri chanya wa watoto katika fasihi ya watoto kama njia faafu ya kujenga jamii bora ya leo na kesho. Utafiti wake umeongozwa na nadharia ya Naratolojia na ya Kisosholojia. Kwa mujibu wa nadharia ya Naratolojia alijikita kwenye kipengele cha utazamishaji. Alibainisha kuwa waandishi wa baadhi ya vitabu teule vya watoto huwatazamisha watoto kuelewa kuwa wana nafasi kubwa ya kubadilisha jamii kwa nafasi zao tofautitofauti walizo nazo. Utafiti huu ulitoa mchango kwetu kinadharia ambapo ulitufahamisha zaidi kuhusu msingi wa nadharia ya Naratolojia. Hata hivo ilibainika kuwa utafiti wake uliegemea kwenye njia chanya za kuwasawiri wahusika watoto ilhali huu ukajikita kwenye mbinu za usawiri wa mhusika mkinzani. Utafiti wake vlevile umejikita kwenye kipengele cha Naratolojia cha utazamishaji nao huu ukajikita kwa kile cha wahusika.

Shavaughn (2022) amechunguza namna mwanamke mwendawazimu anavyozua ukinzani katika bunilizi za Kiingereza za ‘Kigothi’. Bunilizi alizoteua kutumia katika utafiti wake ni riwaya ya *Jane Eyre* (1847) ya Charlotte Bronte, *Rebecca* (1938) ya Daphne du Maurier na *The Thirteenth Tale* (2006) ya Diane Setterfield. Katika riwaya zote tatu, mwanamke mwendawazimu amebainika kuwa na matendo ya kuzua rabsha na yenye uharibifu dhidi ya wahusika wengine. Matendo haya yanazua ukinzani dhidi ya wahusika wengine. Changamoto za kiakili alizo nazo mwanawake mwendawazimu katika riwaya zote zinamfanya kutokuwa na uwezo wa kuelezea visa vyake vya maisha. Kutokana na hayo, usawiri hasi wa matendo yake ya kiharibifu pekee ndio unaoelezewa na watunzi hivyo kusawirika kama mhusika mkinzani. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa makubwa kwetu katika kuelewa dhana ya mhusika mkinzani na sura anazowasilishwa nazo. Vilevile ulichangia uelewa wa namna ya matendo ya mhusika yanavyomfanya kusawiriwa kama mhusika mkinzani. Hata hivyo, utafiti wake Shavaughn unatofautiana na huu kwa kuwa wake ulimlenga sana mhusika mwendawazimu na namna anavyozua ukinzani. Vilevile, ulilenga riwaya nao huu ulimlenga mhusika mkinzani kwa ujumla asiye mwendawazimu au razini katika utanzu wa tamhilia.

Bila shaka swala la usawiri wa wahusika limeshughulikiwa na wasomi mbalimbali huku kila mojawapo wa tafiti zao zikichukua mitazamo tofautitofauti. Nyingi yazo zimeshughulikia usawiri wa wahusika kwa ujumla na zingine aina nyinzine za wahusika kama watoto, wa kike, wa kiume wasio wakinzani. Kutokana na hayo, pengo la kuangazia usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia limeachwa hivyo kuchochea utafiti huu kufanywa.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Kwanza, wahusika wapo wa aina mbalimbali katika kazi za fasihi. Miongoni mwao ni wasaidizi, bapa, wakinzani, duara, nguli na wengine. Hata hivyo, utafiti huu ulijikita tu mhusika mkinzani. Licha ya haya, hatukuepuka kuwazungumzia wahusika wa aina nyingine kila ilipobidi.

Pili, Ebrahim Hussein ameandika tamthilia nyingi. Hizi ni pamoja na *Kinjeketile* (1969), *Mashetani* (1971), *Alikiona* (1972), *Jogoo Kijijini* (1976), *Arusi* (1980), na *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988). Licha ya haya, utafiti huu ulijikita kwenye tamthilia tatu za Ebrahim Hussein ikiwemo *Kinjeketile* (1969), *Jogoo Kijijini* (1976) na *Arusi* (1980). Tamthilia hizi zilichaguliwa kwa sababu zinawakilisha majaribio mbalimbali katika tamthilia za Hussein. Tamthilia ya *Kinjeketile* inawakilisha miundo ya Ki-Aristotle (Okwena 2020). *Jogoo Kijijini* inawakilisha vipengele vya sanaa za maonyesho ya Kiafrika. Nayo *Arusi* ni tamthilia ya kimafumbo kama *Mashetani* ilivyo. Mtafiti hakuteua *Mashetani* kwa sababu utafiti mwingi zaidi umeshafanywa kuhusu tamthilia hiyo ukihusisha wa Okwena (2019), Wafula (1999), na Mukobwa (1985).

Mbali na sababu hizo, mtafiti alilenga kumchunguza mhusika mkinzani katika sura mbili; yaani, mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa na mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Hivyo, tamthilia ya *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini* ziliteuliwa kumchunguza mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. *Arusi* nayo ikateuliwa kuchunguza mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa. Hili lilimwezesha mtafiti kubainisha namna ambavyo mkinzani anavyosawiriwa anapowasilishwa katika sura hizi mbili.

Kando na hayo, utanzu wa tamthilia ndio umechaguliwa kwa sababu swala la mhusika mkinzani linabainika vizuri katika tamthilia ikilinganishwa na tanzu zingine kama riwaya na hadithi fupi (Betti 2015). Mtaalamu huyu ameeleza kuwa swala la mhusika mkinzani lilianzia katika tamthilia za tanzia kisha kuingizwa katika aina nyingine za tamthilia na hatimaye katika utungo wa kinathari. Kutokana na sababu hizi zilizoelezwa, tamthilia zilizoteuliwa zilitupa data faafu kwa madhumuni ya kufanikisha utafiti huu.

### 1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili; Naratolojia na nadharia ya Drama. Naratolojia imetuongoza katika kubainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani na maudhui yanayoibuliwa na mhusika huyo katika tamthilia teule. Kutokana na Naratolojia kutoweza kufafanua swala la mgogoro vyema, nadharia ya Drama iliyokuwa faafu katika kutekeleza hili, ilitumiwa.

#### 1.8.1 Nadharia ya Naratolojia

Msingi wa nadharia hii ni Plato katika *The Republic* (1930) ambamo aliibua dhana mbili *mimesia* na *daigesia*. Alieleza *mimesia* kama uigaji na *daigesia* kama usimuliaji. Dhana hizi zilikuzwa na Aristotle katika kazi yake ya *The Poetics* (1920). Aristotle anasisitiza kuhusu wahusika kama nguzo ya ploti ya kazi ya kifasihi. Kulingana naye, ploti lazima iweke bayana tabia ya wahusika. Aristotle na Plato wanabainika kuwa waasisi wa nadharia ya Naratolojia. Baadaye ukuaji wa nadharia ya Naratolojia ulihusishwa na waitifaki mbalimbali wakiwemo Lord Raglan (1956), Viladmir Propp (1968) na Seymour Chatman (1978). Utafiti huu umeegemea mkondo wa Wananaratolojia wa hivi

punde kama Rimmon-Kennan (1983), Stanzel (1984), Phelan (1987), Keen (2003) na Griffith (2010).

**Mihimili ya Nadharia ya Naratolojia**

Nadharia hii inahusika na vipengele mbalimbali vya usimulizi vikiwemo wakati, nafasi, wahusika, pamoja na nafsi. Vilevile inashughulikia kipengele cha utazamishaji. Hata hivyo, tumejadili tu mihimili ambayo imetufaa katika utafiti huu. Mihimili hiyo ni usawiri wa wahusika na maudhui katika usimulizi.

**Usawiri wa Wahusika**

Rimmon-Kennan (1983) anaeleza kuwa wahusika wanaweza kusawiriwa kwa njia mbili; njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja. Kwa njia ya moja kwa moja, Rimmon-Kennan anasema kwamba, sifa za wahusika huelezwa kwa vivumishi vya sifa, nomino dhahania au aina nyingine za maneno kama viwakilishi vya sifa.

Kwa upande mwingine, Rimmon-Kennan anazidi kueleza kuwa njia isiyo ya moja kwa moja humuachia msomaji jukumu la kutambua sifa za mhusika kwa kuchunguza viashiria mbalimbali. Baadhi ya viashiria hivi ni kama vile mandhari aliyomo mhusika ambayo yanaweza kufichua jambo kumhusu. Kiashiria kingine ni maelezo ya matini kumhusu mhusika. Maelezo haya yanaweza kuwa kama vile matini elekezi (maelezo ya mabano) katika tamthilia. Kwa mfano, ‘akitabasamu,’ ‘kwa hasira’ na mengine. Zaidi ya hayo, Keen (2003) anafafanua kwamba, kwa njia isiyo ya moja kwa moja, maelezo ya mhusika mwingine au msimulizi kuhusu mhusika fulani yanaweza kumsaidia msomaji kubainisha sifa za mhusika mrejelewa. Rimmon-Kennan (1983) naye anaeleza

kuwa sifa za mhusika pia zinaweza kubainishwa kutokana na mazungumzo na matendo ya mhusika, maelezo kuhusu mwonekano wa nje wa mhusika, majazi na analojia. Mhimili huu ndio uliotuongoza katika kutekeleza lengo la kwanza la ubainishaji wa mbinu za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule.

**Maudhui katika Usimulizi**

Stanzel (1984) anaeleza kwamba, maudhui huweza kutambulishwa na msimulizi wa nafsi ya tatu. Anasema kwamba, msimulizi huyu huwakilisha na kuwasilisha usemi wa wahusika, matendo yao, pamoja na fikra zao. Hivyo, kutokana na maelezo ya Stanzel (keshatajwa) kuhusu vipengele hivi vya mhusika, msomaji au mhakiki ataweza kutambua maudhui anayoibua mhusika fulani. Griffith (2010) kwa upande wake anasema kuwa usimulizi unahusisha vipengele mbalimbali ambavyo huwasilisha maudhui. Vipengele hivi ni pamoja na wahusika, ploti na mandhari. Anazidi kusema kwamba Maudhui huwasilishwa kutokana na usemi wa wahusika, fikra zao na matendo yao.

Wahusika ni vyombo vya kuwasilisha maudhui au wazo fulani katika kazi ya fasihi. Matendo na usemi wa wahusika huwasilisha ujumbe fulani. Maudhui au ujumbe unaweza kubainishwa kulingana jinsi mhusika anavyotenda, anavyozungumza na alivyosawiriwa kijumla. Aidha, matendo na usemi wa mhusika huwasilisha ujumbe (maudhui) fulani ambao ndiyo dhamira ya mtunzi. Phelan (1987) anaeleza mhusika kama mshiriki katika mduara ya kimemesia (uigaji) kutokana na sifa na matendo yake na mshiriki katika mduara wa kimaudhui (kama mwakilishi wa ujumbe fulani). Hii ina maana kuwa mhusika anapoiga matendo huwasilisha maudhui fulani. Maelezo ya

mhimili huu yalituongoza katika utekelezaji wa lengo la tatu kwa kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule.

### 1.8.2 Nadharia ya Drama

Nadharia ya Drama iliasisiwa na Carl Jung (1964) ambapo alizungumzia hisia za kisaikolojia na misukumo ya ndani inayochochea matendo ya wahusika wa kidrama. Nadharia hii imekuzwa na mwitifaki Elam (1980) ambaye amezungumzia ukinzani na namna unavyokuza migogoro katika tamthilia.

#### Mihimili ya Nadharia ya Drama

Nadharia ya Drama ina mihimili miwili mikuu ambayo inahusisha msukumo wa ndani unaochochea matendo ya wahusika na namna matendo hayo yanavyokuza migogoro katika drama. Mihimili hii imejadiliwa kwa kina ifuatavyo.

#### Msukumo wa Ndani wa Matendo ya Wahusika

Jung (1964) anaeleza kuwa wahusika katika drama huwa na msukumo wa ndani ya nafsi unaochochea matendo yao. Kulingana na Jung, wahusika wa kimsingi katika drama yoyote ile ni nguli na mkinzani. Kila mmojawapo wa wahusika hawa huwa na sifa fulani za kisaikolojia zinazochochea matendo yao na ambazo huelezeka kupitia umbo lenye mshikamano. Sifa hizi ni pamoja na hofu ya ndani, hisia, kisa cha awali alichopitia mhusika na kilichofichika, imani, matendo, matamanio ya moyo na nia. Vipengele hivi ndivyo huendesha matendo ya mhusika katika drama kwa njia iliyoshikamana.

Hofu ya ndani huwa imefichika katika fikra za mhusika na ndiyo sifa ya kimsingi ya saikolojia ya mhusika. Hisia za mhusika nazo hubainika kupitia matendo yake. Kisa cha awali kinachomzunguka mhusika huweka msingi wa matendo yake na huelezea matatizo yake ya awali ambayo hayajasuluhishwa. Imani nayo ipo katika fikra za mhusika na inaweza kuwa ya hakika, isiyo ya hakika au yenye dukuduku. Hivyo, matendo ya mhusika huhusiana na imani yake ambayo huenda sawia na jinsi mhusika huyo anavyokabili hali au kukosa kukabili hali inayotokea mara kwa mara. Mfumo huu mzima wa imani ya mhusika huibua matamanio yake ya moyo na mhusika huamini kuwa matamanio hayo yatamlinda kutokana na matendo yake na kumuondolea mateso. Kati ya matamanio yake yote ya moyo, mhusika hujitahidi kuafikia angalau mojawapo ambayo sasa inakuwa nia yake. Maelezo haya yalitusaidia kubaini kichocheo cha matendo ya mhusika mkinzani yaani, kwa nini anatenda namna anavyotenda na ni jinsi gani matendo hayo yanasababisha kuzuka kwa migogoro.

**Mgogoro baina ya Wahusika**

Elam (1980) akimrejelea Polti (1921), anazungumzia ukinzani wa aina mbili na namna unavyokuza mgogoro. Anaeleza ukinzani wa kiitikadi ambapo mhuskika mkinzani hutofautiana na kuenda kinyume na itikadi za jamii yake jambo linalosababisha kuzuka kwa mgogoro. Pia, anazungumzia ukinzani wa mhusika mkinzani dhidi ya nguli ama wahusika wengine. Jung (1964) naye akielezea ukinzani wa mhusika mkinzani dhidi ya nguli na wahusika wengine, anasema kuwa, ili drama ing’oe nanga, nguli na mkinzani lazima wawe na fikra za kisaikolojia zinazoenda sambamba. Matamanio na nia ya nguli lazima vizindue hofu ya mkinzani. Vivyo hivyo, matamanio na nia ya mkinzani lazima

visisimue hofu ya nguli. Matokeo ya haya huwa ndio chanzo cha mgogoro baina yao. Katika tanzia, nguli na mkinzani huwa katika migogoro ambayo huishia katika suluhu, kutosuluhishwa au taharuki. Katika drama za futuhi mgogoro baina ya nguli na mkinzani mara nyingi huishia kutosuluhishwa. Mhimili huu na wa kwanza basi zilituelekeza kuchanganua lengo la pili kwa kutusaidia kuchunguza namna mhusika mkinzani anavyokuza migogoro katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein.

## 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inahusu eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji na uchanganuzi wa data pamoja na uwasilishaji wa matokeo.

### 1.9.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani ambapo mtafiti alisoma kwa kina tamthilia ya *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi* ili kupata data ya kimsingi hitajika. Pia, mtafiti alisakura mtandaoni kudurusu tasnifu na makala mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti ili kujifahamisha kuhusu yanayohusiana na mada, nadharia, mbinu za utafiti na dhana ya mhusika mkinzani kwa ujumla.

### 1.9.2 Uteuzi wa Sampuli

Tamthilia nyingi zimeandikwa na Ebrahim Hussein. Tamthilia hizi ni; *Wakati Ukuta* (1970), *Kinjeketile* (1969), *Alikiona* (1972), Jogoo *Kijijini* (1976*) Arusi* (1980) na *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988). Hata hivyo, sampuli iliteuliwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ambapo *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi* ziliteuliwa kimaksudi kwa kuwa zina data lengwa hitajika iliyomwezesha mtafiti kupata matokeo

yake. Hali kadhalika, *Kinjeketile* ni tamthilia ya kitanzia na yenye miundo ya Kiaristotle ilhali *Jogoo Kijijini* inabainika vizuri zaidi kwa vipengele vyake vya sanaa za maonyesho za Kiafrika. Hatimaye, *Arusi* ni tamthilia ya kimafumbo. Uteuzi umezingatia mikondo mbalimbali katika utunzi wa Hussein pamoja na sura alizomwasilisha nazo mhusika mkinzani za kuwepo na kutokuwepo kwenye jukwaa.

### 1.9.3 Ukusanyaji wa Data

Katika kukusanya data, mtafiti aliangalia namna ambavyo wahusika wanasemezana na kudondoa kauli za mhusika mkinzani anavyozungumza na wahusika wengine. Kwa upande mwingine kauli za wahusika wengine ama msimulizi kumhusu mkinzani zilikusanywa. Baada ya hayo, mtafiti alibainisha namna kauli hizo zinavyozua ukinzani hali kadhalika migogoro katika drama. Dondoo za mazungumzo hayo ya ukinzani zilinukuliwa na kukusanywa kwa madhumuni ya kuchanganuliwa. Maelezo ya ziada kama vile maelekezo ya jukwaa (maelezo ya mabano) yanayoeleza hisia na hali za mkinzani au za wahusika wengine kuhusu mkinzani yalikusanywa pia. Haya yalichangia uchanganuzi wa data hizi zilizosaidia katika utekelezaji wa malengo ya utafiti.

### 1.9.4 Uchanganuzi wa Data

Data zilizokusanywa kutoka tamthilia ya *Kinjeketile, Jogoo Kijijini* na *Arusi* zilipangwa, kuelezwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti ili kuipa kazi hii mpangilio faafu. Jambo hili lilimwezesha mtafiti kuhusisha uhakiki pamoja na malengo ya utafiti huku akijaribu kujibu maswali ya utafiti. Uchanganuzi huu ulifanyika kitaratibu kwa kuzingatia hatua mbalimbali madhubuti.

Kwanza, mtafiti alitumia data zilizokusanywa kwa kuangalia, kauli za mhusika mkinzani; namna anavyozungumza, namna anavyotenda na wanachokisema wahusika wengine au msimulizi dhidi yake. Haya yaliwekwa katika sentensi kwa kutilia maanani aya, mtiririko na mshikamano wake. Mchakato huu mzima uliongozwa na nadharia ya Naratolojia.

Pili, mtafiti alitumia kauli zilizosemwa na mhusika mkinzani au msimulizi kumhusu na kuziweka mkabala na za nguli pamoja na wahusika wengine. Baada ya hayo mtafiti alizichunguza kauli hizo na kuona namna ambavyo kauli za mkinzani zinajibizana na za nguli au wahusika wengine na namna zinavyozalisha migogoro na uhasama kati yao. Vilevile, alichunguza na kuchanganua namna ambavyo kauli hizo za mkinzani zinakiuka itikadi za jamii ambayo mwandishi wa tamthilia husika ameandikia. Mchakato huu mzima uliongozwa na nadharia ya Drama.

Mwisho, mtafiti alitumia dondoo za mazungumzo ya mkinzani, matendo yake, pamoja na wanachokisema wahusika wengine na msimulizi kumhusu na kuchunguza namna vinavyoibua maudhui mbalimbali. Hatua hii ilihusu kushirikisha yote yanayomzunguka mhusika mkinzani yakiwemo anayosema msimulizi na wahusika wengine kumhusu, mandhari anamopatikana, kauli zake dhidi ya wahusika wengine, matendo yake na mengine. Haya yote yalichanganuliwa kwa pamoja ili kubainisha maudhui aliyokuza mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Hatua hii iliongozwa na nadharia ya Naratolojia. Uchanganuzi wa data ulifanyika kwa utaratibu kwa kushughulikia tamthilia moja baada ya nyingine kwa kila hatua ya kuyaafikia malengo.

### 1.9.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya kimaelezo kwa kutumia maandishi ya matini ambayo yalipangwa katika aya. Kwa kila maelezo yaliyotolewa, dondoo za kauli za ukinzani kuhusu mhusika mkinzani dhidi ya nguli na wahusika wengine ziliambatanishwa huku zikichambuliwa kwa kina. Hali kadhalika, maelezo ya matokeo hayo yaliwasilishwa kwa njia iliyo wazi kubainisha namna maswali ya utafiti yalivyojibiwa kwa mujibu wa nadharia ya Drama na Naratolojia.

## 1.10 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alijukumika kupata vibali hitajika kabla ya kuzama katika utafiti mzima. Alitafuta vibali kutoka kwa shule husika, kitengo cha *Center for Research Ethics and Safety (C.R.E.S)*, pamoja na tume ya *National Council for Science, Technology and Inovation (NACOSTI).*

Aidha, mtafiti aliwatambua wataalam na watafiti wote ambao amewanukuu na kushirikisha mawazo yao katika utafiti wake. Hili limedhihirishwa kwa kuwaorodhesha katika sehemu ya marejeleo mwishoni mwa sura ya mwisho ya tasnifu hii. Vilevile mtafiti alizingatia haki za mwandishi wa tamthilia za *Kinjeketile*, *Jogoo Kijijini* na *Arusi* na vitabu vingine vyote vilivyomfaa kwa kutotolesha nakala.

# SURA YA PILI

# USAWIRI WA MHUSIKA MKINZANI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN

## 2.0 Utangulizi

Sura ya kwanza imeshughulikia utangulizi wa tasnifu hii unaojumuisha usuli wa mada, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia na mbinu za utafiti. Katika sura hii, tumezungumzia maisha ya mtunzi wa tamthilia teule kwa ufupi. Haya yamechangia kwa kiasi fulani kufahamu namna ambavyo mtunzi amemsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia zake teule. Vilevile, sura hii imezungumzia namna mhusika mkinzani anavyowasilishwa kama mhusika asiyekuwepo na aliyepo kwenye jukwaa. Muktadha huu ni muhimu kwa kuwa ndiyo njia ambayo Ebrahim Hussein alimuwasilisha mhusika mkinzani katika tamthilia ya *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini.* Aidha, muhtasari wa tamthilia teule umetolewa, mbinu mbalimbali za usawiri wa wahusika zimejadiliwa na namna zimetumika katika kumsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia teule kwa mujibu wa nadharia ya Naratolojia.

## 2.1 Maisha ya Ebrahim Hussein Yanavyoibua Muktadha wa Ukinzani katika Tamthilia zake Teule

Spector (1973) anaeleza kuwa kuchunguza maisha ya mtunzi na utunzi wake ni jambo muhimu sana katika kutathmini kazi zake. Hivyo, kuna umuhimu fulani kufahamu machache kumhusu Ebrahim Hussein ili kupata ufaafu wa uhakiki wa swala la mhusika mkinzani katika tamthilia zake teule. Ebrahim Hussein alizaliwa mwaka wa 1943 Lindi,

pwani ya Tanzania ambako alikulia na kusomea. Alisomea shule ya upili ya Aga Khan ilioko mjini Dar es salaam.

Alijiunga na chuo Kikuu cha Dar es salaam mnamo mwaka wa 1966 hadi mwaka wa 1969. Alisomea Thieta, Sosholojia na Kifaranza. Mbali na usomi, Hussein alikuwa mwanaharakati wa chama cha kisiasa cha *Tanganyika African National Union* ujanani mwake (Ricard, 2000). Mwaka wa 1970, alijiunga na chuo kikuu cha Humboldt kilichoko Ujerumani. Alikamilisha masomo yake chuoni humu na kuhitimu katika shahada ya uzamifu katika sanaa za maonyesho na historia ya tamthilia mnamo mwaka wa 1974.

Kipaji cha utunzi cha Ebrahim Hussein kilianza kudhihirika alipokuwa katika chuo kikuu cha Dar es salaam miaka ya sitini. Katika mwaka wa 1966 aliigiza na wenzake tamthilia za Kiswahili katika *Youth Drama Festival*. Tamthilia zake za kwanza alizotunga zilikuwa *Alikiona (*1968) na *Wakati Ukuta* (1968) ambapo aliathirika na utamaduni wa drama ya Kiafrika na thieta ya kimagharibi (Okwena, 2019). Utunzi wake haukuishia pale. Mnamo mwaka wa 1969, Ebrahim Hussein alitunga tamthilia ya *Kinjeketile* kisha kufuatisha tamthilia ya *Mashetani*. Mwaka wa 1976 alitunga tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ambayo ni ya kimafumbo kama ilivyo ya *Mashetani* na *Arusi*. Tamthilia za mwisho za Hussein ni *Arusi* (1980), *Kwenye Ukingo wa Thim* (1988) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Bloom (1997) anaeleza kuwa, waandishi waliotangulia huwaathiri wandishi wa baadaye. Yazdan (2008) naye kwa upande wake anasema kuwa kila mtu hujifunza kwa

kufuata mfano, majaribio au maagizo, kuiga, kuathirika na kuitikia. Kwa kigezo hiki tunaweza kusema kuwa Hussein aliathirika na kazi tangulizi kama za Bertolt Brecht. Tunapata idhibati ya kuathirika kwake kutoka kwa kazi tangulizi kwa kuzingatia kauli zake katika mahojiano aliyofanyiwa na Okwena (2016). Hussein katika mahojiano hayo alieleza kuwa fasihi wakati wa ukoloni ilikuwa ya Kiingereza. Waandishi wengi wa Kiafrika hawakuwepo na wale wachache waliokuwepo waliathiriwa na Uzungu katika utunzi wao. Alimweleza Okwena katika mahojiano hayo kwamba watunzi wa Kiafrika waliathirika sana na utunzi wa Kimagharibi. Hili ni dhibitisho tosha kuwa Hussein ni mmojawapo wa watunzi hawa wa Kiafrika walioathirika. Okwena (2019) aneleza kuwa kusomea kwa Ebrahim Hussein ughaibuni pia kuliathiri pakubwa utunzi wake. Kwa kuwa swala la kumtumia mhusika asiyekuwepo jukwaani kama kiini cha ukinzani katika drama lilianzishwa na watunzi wa Kimagharibi, ni dhahiri kuwa walimwathiri Hussein vilevile. Hivyo basi, Hussein anaonekana kuathirika na dhana hii katika tungo zake za *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini.*

Ebrahim Hussein katika utunzi wa *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini* vilevile umejengeka kwenye usuli wake. Yeye ameishi katika kipindi cha mikondo mbalimbali ya kisiasa; siasa za kipindi cha ukoloni na siasa za baada ya ukoloni. Hussein aliandika tamthilia zake kuanzia miaka za sitini hadi miaka za themanini. Katika tamthilia hizo, ameandika kuhusu uhuru wa Mwafrika. Mhakiki anapozisoma kwa makini ataweza kubaini kuwa Hussein anajaribu kutathmini iwapo uhuru ambao Mwafrika aliupata ni wa kweli au ni wa bendera tu. Ili kutekeleza haya, Hussein anawarejelea wahusika halisi wa kihistoria kama Kinjeketile (aliyepigana dhidi ya Wajerumani miaka za 1880-1919) ambao

walipigana dhidhi ya dhulma na unyanyasaji kutoka kwa wakoloni. Anawaumba upya kifasihi wahusika kama hawa na kudhihirisha kuwa ile dhulma na unyanyasaji waliopigania bado ipo. Anaeleza kuwa, katika harakati za kupigania ukombozi, nguli wa Kiafrika walipata ukinzani mkubwa kutoka kwa mkoloni. Licha ya hayo, walifanikiwa kumbandua mkoloni ila akawaachia 'sumu' mwilini iliyoendelea kuwaathiri hadi sasa. Kijazanda 'sumu' hii ni ukoloni-mamboleo ambao Hussein anazungumzia katika tamthiliza zake teule. Haya yamejadiliwa kwa kina katika sehemu ya maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule kwenye sura ya nne ya tasnifu hii.

Kando na hayo, katika kipindi cha baada ya ukoloni, jumuiya ya Afrika Mashariki iliundwa kwa uhusiano wa pamoja wa kiuchumi ila ulisambaratika mwaka wa 1977 (Mazrui, 1980). Hii ilipelekea kuwepo kwa mifumo kinzani za kiuchumi; ubepari (nchini Kenya) na Usosholisti (nchini Tanzania). Nchi ya Kenya ilijaribu kufufua uhusiano huu lakini haikufua dafu. Hali hii ilichochea Hussein Kubuni tamthilia ya kimafumbo *Arusi* ambapo ukinzani wake umejengwa kwa misingi hii ya mifumo kinzani za kiuchumi zinazowakilishwa na wahusika Bukini na Mwanaheri (Mukobwa 1985).

### 2.2 Mhusika Mkinzani kama Mhusika Asiyekuwepo kwenye Jukwaa

Mahfouz (2012) anasema kuwa mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa ni mhusika ambaye haonekani na hadhira kwenye jukwaa bali anafahamika kupitia mazungumzo ya wahusika wengine au ya msimulizi kumhusu. Mhusika huyu huathiri matendo ya wahusika wengine katika drama na kuibua mgogoro mkuu katika drama. Anaweza

kuwa kiumbe hai, kisicho na uhai, mnyama, zimwi au kitu chochote kile alichokusudia mtunzi kukitumia katika kazi yake.

Hammood (2020) naye anaeleza kuwa matumizi ya mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa yalianza kipindi cha fasihi ya Kigiriki. Mhusika wa aina hii alitumika kama nguvu kinzani zinazochochea na kuendesha matendo katika drama. Anatoa mfano wa kazi ya kidrama ya *Oedipus the King* (*Oedipus Rex)* ambayo imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili kama *Mfalme Edipode* (1971). Katika tamthilia hii, Laius, babake Oedipus ambaye alifariki, hatokei jukwaani ila ndiye mhusika mkinzani. Matukio yote na mgogoro mkuu unajengeka kupitia kwake katika drama hiyo. Baada ya Oedipus kumuua Laius, babake mzazi, jaaza ya Laius inakuwa nguvu kinzani katika maisha ya Oedipus. Inakuwa kikwazo kikubwa katika ufanisi wa maisha ya Oedipus na kuathiri mustakabali wake ambapo anaishia kujipofusha baada ya kugundua kuwa amemuoa mamake mzazi.

Matumizi ya mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa yaliendelezwa na watunzi mbalimbali. Kulingana na Mahfouz (2012) mtunzi kama William Shakespeare alitumia dhana hii ya mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa katika tamthilia yake ya *Romeo and Juliet*. Rosaline haonekani kwenye jukwaa katika mchezo huo wote ila ana athari kubwa dhidi ya wapenzi hawa wawili Romeo na Juliet. Mahfouz (keshatajwa) anazidi kueleza kuwa watunzi Henrik Ibsen na Chekhov ndio walifanikisha zaidi matumizi ya mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa katika drama.

Hammood (2020) anaeleza kuwa dhana hii vilevile iliendelea kutumika katika tungo za kidrama za kisasa za Kimarekani katika karne ya ishirini. Drama za kisasa za Kimarekani ni dhana iliyotumika kurejelea drama zenye athari kubwa katika tasnia ya maigizo katika karne ya ishirini. Ziliangazia mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni yaliyotokea baada ya vita vya kwanza vya dunia. Hammood (keshatajwa) anasema kuwa watunzi hawa waliwatumia wahusika wasiokuwepo kwenye jukwaa kuelezea msukumo wa ndani ya nafsi unaochochea matendo ya wahusika walioko jukwaani hivi kwamba wanaathiri matendo yao.

Shepard III (1943-2017) ni mmojawapo wa watunzi wa Kimarekani waliotumia dhana hii ya mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Shepard III katika drama yake ya *Buried Child* (1978) amemchora mtoto aliyezikwa kama mhusika mkinzani asiyekuwepo kwenye jukwaa (Hammood 2020). Msomi huyu anazidi kueleza kuwa mtoto huyu aliyezikwa ijapokuwa haonekani jukwaani, anaathiri matendo yote katika drama. Hakuna tukio lolote muhimu linalotendeka jukwaani lisilochochewa na jaaza ya mhusika huyu. Mtoto huyu ni mwanaharamu kwa kuwa ni zao la Tiden na mamake Halie. Anaishia kunyongwa na Dodge, babu yake. Mtoto huyu anasawiriwa kama mhusika mkinzani katika tamthilia hiyo licha ya kutoonekana jukwaani. Anasababisha kuzuka kwa mgogoro mkubwa katika familia hiyo, kuvurugika na kusambaratika kwa familia ya Dodge.

Morrow (2009) vilevile anafafanua kwa kina mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa kwa kusema kuwa mhusika huyu ni msababishi wa matukio katika drama na huondolewa kwenye upeo wa matendo yanayotendeka jukwaani ila kidhahania ndiye

anayesababisha matendo hayo. Bila yeye, matendo na mgongano unaotendeka jukwaani hauwezi kutokea. Katika kuifahamu dhana hii swali linaloulizwa hapa ni je, matendo yanayotendeka jukwaani yanasababishwa na mhusika au wahusika fulani wasiokuwepo jukwaani? Morrow anasema kuwa jibu hapa ni ndio. Hivyo, mhusika wa aina hii ndiye kiini cha mgongano wa matukio yote yanayotendeka kwenye jukwaa. Kupitia uchunguzi wa kina inabainika kuwa katika drama za aina hii, matendo yanayotazamwa na hadhira jukwaani yana msababishi wake ambaye ndiye mhusika huyu asiyekuwepo jukwaani.

Morrow (2009) anazidi kueleza kuwa wahusika halisi walioko kwenye jukwaa hufahamu kuhusu mhusika (au wahusika) asiyekuwepo kwenye jukwaa mwanzoni mwa mchezo. Hili huwawezesha kufahamu kiini cha ukinzani dhidi yao na namna nguli anaweza kukabiliana naye. Anasisitiza dhana hii kwa kusema kuwa wahusika walioko jukwaani humtaja mhusika huyu asiyekuwepo kwenye jukwaa mara kwa mara katika tamthilia nzima. Huku kumtaja kuna athari nyingi; kwanza hutangaza utambulisho wake na pili, huhuisha dhana ya mhusika huyo katika fikra za wahusika walioko jukwaani na hadhira. Hili huwafanya kutomsahau kama kiini cha kuwepo kwa matendo hayo. Wahusika wengine jukwaani na hadhira hutazama athari ya mhusika huyu asiyekuwepo jukwaani aidha moja kwa moja au kupitia wanachokisema wahusika wengine ama msimulizi kuhusu matendo yake.

Kutokana na muktadha uliowekwa dhahiri na Morrow (2009), ni wazi kuwa mhusika mkinzani anapowasilishwa kama asiyekuwepo kwenye jukwaa huwa ndiye nguzo inayoshikilia matendo yote katika tamthilia. Morrow, amemfafanua mhusika

asiyekuwepo kwenye jukwaa kama msababishi wa matendo kutokana na namna anavyosawiriwa katika drama. Tamthilia ya *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini*, ni kielelezo bora cha tamthilia zilizo na mhusika mkinzani kama asiyekuwepo kwenye jukwaa kwani ndiye msababishi wa matendo na mgogoro.

Mbinu hii ya kutumia mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa kama kiini cha ukinzani katika drama imewaathiri baadhi ya watunzi wa Kiafrika. Miongoni mwao ni Ebrahim Hussein, John Ruganda na Wole Soyinka. Ebrahim Hussein alitumia mbinu hii katika *Kinjeketile* (1969) na *Jogoo Kijijini* (1976). John Ruganda naye alitumia mbinu hii katika *The Burdens* (1972) na Wole Soyinka katika *The Trials of Brother Jero* (1963). Morrow (2009) anaeleza kuwa ukinzani wa mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa huweza kutokea kwa njia mbili. Njia ya kwanza ni pale ambapo mhusika huyu anazungumziwa na wahusika wengine katika drama na athari yake hudhihirika kupitia usemi wa wahusika hao kumhusu. Vilevile, athari yake hudhihirika kupitia wahusika wengine wanaohusiana naye au wanaomuunga mkono katika drama. Mhusika mkinzani katika *Kinjeketile* anabainika kupitia sura hii. Sura ingine ni ile ambayo mhusika huyu hatokei jukwaani ila huzungumziwa katika drama na msimulizi namna anavyoleta ukinzani moja kwa moja. Hii inabainika katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*. Haya yamefafanuliwa kwa kina katika sehemu ya utambuzi wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule.

## 2.3 Mhusika Mkinzani kama Mhusika Aliyepo kwenye Jukwaa

Tumemzungumzia kwa uchache mhusika aliyepo kwenye jukwaa kwa kuwa ndiyo njia ambayo watunzi wengi hutumia kuwawasilisha wahusika katika kazi zao za drama. Pia, tafiti zozote zile zinazohusu mhusika wa drama humzungumzia mhusika wa namna hii. Hata hivyo, inajuzu kufahamu kuwa mhusika aliyepo kwenye jukwaa hushiriki matendo na kuzungumza na wahusika wengine moja kwa moja jukwaani (Kott 1990). Mhusika wa aina hii hutagusana na wahusika wengine jukwaani na kudhihirisha mihemko, na hisia zake moja kwa moja. Beegle (2015) naye anamzungumzia mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa ambaye hujitokeza jukwaani na kushiriki matendo na mazungumzo pamoja na wahusika wengine kwenye jukwaa. Anazidi kueleza kuwa mhusika huyu huchangia pakubwa hadhira kuelewa ukuaji wa ploti, migogoro na maudhui kwani wao hutazama maigizo yake moja kwa moja. Mhusika mkinzani wa namna hii ndiye tuliyemfafanua katika tamthilia ya *Arusi.*

## 2.4 Mbinu za Usawiri wa Wahusika

Wamitila (2002) anaeleza kuwa mtunzi ana uhuru wa kuchagua namna ya kuwasilisha wahusika wake vilevile kuteua aina fulani ya wahusika wa kutumia katika kazi zake. Wahakiki na wasomi wa fasihi hutegemea sifa mbalimbali kuwaelewa wahusika katika kazi fulani ya kifasihi. Baadhi ya sifa hizi ni; hulka ya wahusika, uhusiano wa wahusika hao na wahusika wengine, lugha yao, matendo yao, hisia zao, nafsi yao miongoni mwa zingine. Wamitila (2002) anafafanua mbinu mbalimbali za kuwasawiri wahusika kama; mbinu za kuwatumia wahusika kuelezea, kupeana fununu ili msomaji mwenyewe ahitimishe sifa za mhusika, kuelezea moja kwa moja, kulinganisha na kulinganua,

kuweka katika mandhari ya kuigiza, kuwapa majina yanayofungamana na matendo na sifa zao, kutumia ritifaa, kutumia uzungumzi nafsia, kuashiria na kudhihaki.

## 2.5 Muhtasari wa Tamthilia ya *Kinjeketile*

Mchezo wa kuigiza unaanza Chausiku akimueleza Bi. Kitunda, mamake, kuhusu moshi unaofuka kutoka kwa nyumba ya Kinjeketile. Moshi ambao anashindwa kufahamu kiini chake. Chausiku anapojaribu kujongea karibu na nyumba ya Kinjeketile ili kuchunguza kiini cha moshi huu anafukuzwa na nyoka. Pia, tuaelezwa kuhusu Bi. Kinjeketile na Bi Kitunda ambao wanalalamikia hali ngumu ya maisha ya kukosa chakula inayoletwa na dhulma za Mjerumani. Kwa upande mwingine, Mkichi, Mgindo na Kitunda wanapanga kuhusu mbinu ya kumbandua Mjerumani (Udongo mwekundu) nchini mwao. Kupitia kwa maneno ya Mkichi tunafahamishwa kuhusu namna Mjerumani amewadhulumu Wamatumbi. Dhulma hii ni pamoja na Kutozwa kodi na  kufanyishwa kazi katika mashamba yao kwa malipo duni miongoni mwa mengine. Haya yanawachochea kuandaa mipango kabambe ya kumuondosha Mjerumani nchini mwao. Kitunda anasisitiza kuhusu kupata silaha kwanza kwani Mjerumani ana bunduki kubwa. Wamatumbi, Wazaramo na watu wa kabila nyingine wanakataa kutawaliwa na Mjerumani kwa kuwafanyisha wanaume wao kazi ngumu katika mashamba huku wakiwadhulumu.

Mkichi na Kitunda wanakosa kuelewana kwa kiasi fulani ila Kitunda anasisitiza kuhusu umoja. Wanapoandaa mipango ya kumuondosha Mjerumani, Kinjeketile, kiongozi wao amejibana chumbani mwake. Hili linajenga taharuki kwani watu wanataka kujua anachokifanya Kinjeketile humo alimojibana. Hatimaye anajitokeza bayana na

kuwaeleza dhahiri kuhusu vita dhidhi ya Mjerumani ambaye ndiye adui wao. Anawapa maji ambayo yangekuwa ngao ya kujikinga dhidi ya Mjerumani. Watu wanayapokea ila wanasubiri ruhusa kutoka kwa Kinjeketile ili waanze vita. Kinjeketile anahimiza umoja baina ya makabila yote ya Tanzania. Kitunda na wenzake wanaenda kwa watu wa kabila tofautitofauti jirani kama vile Wazaramo, Wagindo miongoni mwa wengine kuwajuza kuhusu kuungana vitani.

Watu wa makabila yote wanapokuwa tayari wanaenda kumsihi Kinjeketile awape ruhusa ya kuanza vita. Wanakosa subira wanapoambiwa na Kinjeketile wasubiri mwelekeo kutoka kwa *Kongo* (mungu wao). Wanaondoka na kuenda vitani kwa kuongozwa na Kitunda. Mjerumani anawaua weusi wengi vitani hadi mwishowe wanashindwa vita. Mjerumani anamkamata Kinjeketile na kumtesa zaidi huku akimlazimisha kukiri kuwa maji aliyowapa watu yalikuwa ya uongo ishara ya kukiri kushindwa. Hata hivyo, anakataa katakata kuitikia amri hiyo.

### 2.5.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Kutokana na muktadha ulioibuliwa mwanzoni mwa sura hii kuhusu mhusika asiyekuwepo jukwaani, Mjerumani ndiye mhusika mkinzani katika tamthilia hii. Japo hayupo jukwaani, ndiye kiini cha ukinzani katika tamthilia nzima. Ukinzani wake unadhihirika kupitia kwa namna wahusika wengine wanavyomzungumzia vilevile kupitia vibaraka wake. Vibaraka hawa wanaotumiwa na Mjerumani ni Mnyapala na Afisa wa Kijerumani. Haya yanadhihirika katika tamthilia hii kupitia Kitunda anaposema;

> Sisi sote tunataka Njelumani aodoke lakini tunamuondoaje? Kwanza yeye ana silaha, sisi hatuna. Jambo la kufanya ni kuanza kukusanyakusanya silaha – kuiba bunduki za askali, kunyang'anya, kufanya chini juu ili tupate silaha. Hili haliwezi kufanyika mala moja. Tena basi itakuwa vigumu kulifanya maana hivi sasa kuna vibalaka chungu nzima, utakachofanya akina Mnyapala keshasikia (uk.5).

Kutokana na dondoo hili ni dhahiri kuwa ukinzani mkuu unatoka kwa Mjerumani pamoja na vibaraka wake ambao ni Mnyapala na Afisa wa Kijerumani. Juhudi za nguli (Kinjeketile pamoja na wafuasi wake) za kupigania ukombozi zinadidimizwa na Mjerumani na vibaraka wake. Hivyo basi, utafiti huu umebainisha namna mhusika mkinzani (Mjerumani pamoja na vibaraka wake) amesawiriwa katika tamthilia hii.

## 2.6 Muhtasari wa Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

Usimulizi wake umetumia kunga za fasihi simulizi. Tamthilia hii imegawika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inazungumzia mkunazi rahmani ambao ulidumu kwa muda mrefu hadi kulipotokea mbuubuu ulioua mkunazi huo na kusababisha ukaufu kuingia mjini. Tunazidi kuelezwa kuhusu jogoo ambaye aliwika kuonyesha ishara ya mapambazuko. Hata hivyo mtu alalamikia sikio kuzuiliwa na unyayo asiweze kuona mapambazuko yenyewe. Mapambazuko hayo yanakosa kudumu kwani usiku wa haraka unaingia na kumkuta mtu huyo njiani. Anapokaribia ziwa anaanguka kifudifudi. Mtu huyu ni ishara ya giza kwa watu walio ndani. Kunapopambazuka siku inayofuata sikio lake linazinduka anaposikia radi ipitayo kwenye njia. Kunatokea kutoelewa kitendo cha jogoo kukosa kuwika siku hiyo kukaribisha mapambazuko.

Usimulizi mwingine unahusu kijana anayeshika kijiti na kukirusha na mlango anaojaribu kuupitia umeliwa na mchwa. Kuvunjika kwa mlango huu una maana kuwa hakuna mgawanyiko wa kitabaka wala watu wenye hadhi katika jamii hivyo mwanzo

wa utu. Kijana huyu anapofika nyumbani anakutana na ajuza ambaye anaishia kumsimulia kuhusu chanzo chao kufika kijijini pale. Ajuza anamweleza kuwa ni kutokana na madhambi waliyofanya ndipo wanajikuta pale walipo. Jambo hili linamfanya kijana huyu kujitoa kafara ili kulipiza dhambi hizo ndipo aikomboe jamii yake.

Sehemu ya pili ya tamthilia hii inasimulia kuhusu Masononi, kijiji kilichokuwa na mabinti wazuri na mali nyingi. Kunatokea joka liitwalo Sesota lenye vichwa sabini ambalo lina mazoea ya kuchukua mali na binti mmoja kila mwaka kutoka kitongoji hiki. Jambo hili linawaletea hofu kubwa wanakijiji hawa. Wanamasononi wanafanya mkutano wa namna ya kuliangamiza joka hili. Ajuza mmoja asiye na meno anapendekeza kuteuliwa kwa Mtemi atakayekabiliana nalo. Baada ya Mtemi kuteuliwa Wanamasononi wanafahamu nguvu na uwezo alio nao Sesota na kumtafutia Mtemi silaha. Anapewa mkuki wa miujiza na ngao ya jadi.

Joka hili linapoingia kitongojini, Mtemi anakabiliana nalo kwa awamu ya kwanza kwa kulirushia mkuki wa miujiza. Kukabiliana na Sesota kunalipandisha mori na kutoa miale ya moto ambayo inaleta maafa na uharibifu mkubwa kijijini. Wanyama na binadamu wanakufa navyo vibanda na mashamba vinateketea. Licha ya hayo, Mtemi anafanikiwa kulikata kichwa kimoja. Hili linasababisha kutoweka kwa joka hili na kuchezwa kwa ngoma mbalimbali. Mapambano hayo yanamwachia Mtemi sumu mwilini inayomfanya kujiondoa kwa ajili ya kujitakasa. Baada ya kuondoka kwake, ufisadi unakithiri kijijini na dalili ya kurudi kwa Sesota inapoonekana, watu wanajaribu

kumkimbilia Mtemi kwa msaada ila wanaishia kuvunja ngao ya jadi. Wanabaki tu kusubiri madhara ya Sesota.

Tamthilia hii ni mojawapo wa kazi za kijazanda za Ebrahim Hussein. Tumetoa ufasiri wa sehemu ya pili ya tamthilia hii kwa misingi ya wasomi na wahakiki mbalimbali ambao wameeleza kuwa imejengwa kwa misingi ya kisiasa. Baadhi ya wasomi hawa ni Okwena (2019) na Mukobwa (1985) wanaokubaliana kwamba, tamthilia hii inahusu siasa za ukoloni na ukoloni mamboleo. Wakoloni walipokuwa katika nchi za Afrika Mashariki waliendekeza uongozi wa kidhulma na wa kimabavu. Licha ya hayo, waling'atuliwa Afrika kwa juhudi za nguli wa Kiafrika na baadaye uhuru ukapatikana. Hata hivyo, ilidhihirika kuwa uhuru huo ulikuwa wa bendera tu kwani athari ya uongozi wao wa kidhulma uliendelea kudhihirika katika nchi za Kiafrika. Viongozi wa Kiafrika waliendeleza dhuluma hizo.

Kutokana na haya basi, Hussein aliweza kuisuka tamthilia hii kwa misingi hii. Kukuja kwa joka Sesota katika kitongoji cha Masononi  na kuchukua mabinti na mali kunawakilisha kukuja kwa Wakoloni Afrika na kuchukua mali na ardhi ya wenyeji. Kukabiliana kwa Mtemi na joka hili kunapelekea kuliondoa ila linamwachia sumu mwilini. Hili linawakilisha makabiliano kati ya viongozi wa Kiafrika na Wakoloni ambao waliishia kuondolewa Afrika bali wanawaachia viongozi hao 'sumu' mwilini. Sumu hii ni dhulma na unyanyasaji unaoendelezwa na viongozi wa Kiafrika dhidi ya Waafrika wenzao (ukoloni-mamboleo).

### 2.6.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

Muktadha uliowekwa dhahiri mbeleni umeeleza kuhusu mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Umeeleza kuwa mhusika huyu hatokei kabisa jukwaani ila anaelezwa na ama msimulizi au wahusika wengine kuhusu namna matendo yake yanavyoleta ukinzani katika drama. Pia matokeo ya matendo yake yanamtambulisha. Kutokana na hayo, joka linalojulikana kama Sesota ndiye mhusika mkinzani katika tamthilia hii. Sesota analeta ukinzani kutokana na matendo yake hasi yanayoelezwa na msimulizi ya kunyakua mali na binti kutoka kijiji cha Masononi. Mtemi naye ndiye mhusika nguli anayejaribu kukabiliana na joka hili. Tumembaini na kumzungumzia mhusika mkinzani katika sehemu ya pili ya tamthilia hii.

## 2.7 Muhtasari wa Tamthilia ya *Arusi*

Tamthilia hii inahusu ndoa kati ya vijana wawili Bukini na Mwanaheri. Wawili hawa wanafunga pingu za maisha kisha Bukini anaenda ughaibuni. Kabla ya kuondoka anamwahidi Mwanaheri kuwa angerudi baada ya mwezi wa pili ama angetuma nauli. Kunakosekana mawasiliano baina yao kwa muda mrefu jambo linalomfanya Mwanaheri kumsaliti Bukini licha ya Bukini kumwahidi kuwa angerudi punde. Mwanaheri anaingia katika uhusiano wa kimapenzi na Ali hadi anaishia kuambulia ujauzito.

Kutokana na ujauzito wa Mwanaheri, kunazuka mgogoro mkali baina yake na shangaziye. Kulingana na shangazi, Mwanaheri ameenda kinyume na maadili ya kijamii kwa kumsaliti Bukini mumewe na kupata ujauzito nje ya ndoa yao halali. Mwanaheri

anaonekana aliyekengeuka anapokiri wazi wazi kuwa hakuna lolote la kuficha kwa kuwa ujauzito u dhahiri na hajutii kumsaliti mumewe.

Mgogoro kati ya Mwanaheri na shangazi unazua mgogoro mwengine kati ya shangazi na Mama Mwanaheri. Mzee naye anapojaribu kuingilia kati anashindwa. Mama Mwanaheri anamlaumu Bukini kwa kutowasiliana na Mwanaheri baada ya kuenda ughaibuni naye shangazi anamlaumu Mwanaheri kwa kutokuwa mwaminifu kwa mumewe. Mgogoro mwingine ni kati ya Mwanaheri na Bukini ambapo Mwanaheri anaamua kumrudishia Bukini pete ya uchumba na kudai talaka.

Tamthilia hii nzima inahusu ndoa kati ya vijana wawili Bukini na Mwanaheri kama ilivyofafanuliwa hapo mwanzoni. Hata hivyo, kwa mujibu wa wahakiki wa awali, ukweli ni kwamba Ebrahim Hussein alitumia arusi kati ya hawa wawili kijazanda. Okwena (2019) akimrejelea Mukobwa (1985) anaeleza kuwa Hussein anatumia arusi kati ya Bukini na Mwanaheri kuelezea uhusiano wa kiuchumi kati ya nchi mbili (Kenya na Tanzania) zenye mifumo tofauti za kuzalisha mali. Ebrahim Hussein anajaribu kuelezea namna jumuiya ya Afrika mashariki ilivyoundwa kipindi cha wakoloni hadi iliposambaratika mwaka wa 1977 (Mazrui, 1980). Kwa mujibu wa historia, Kenya ilijaribu kufufua uhusiano huu na Tanzania lakini haikufaulu. Hii ndio arusi ambayo Bukini (ambaye anawakilisha nchi ya Kenya) anajaribu kumshawishi Mwanaheri (ambaye anawakilisha Tanzania) wafunge ndoa lakini ndoa hiyo inagonga mwamba.

### 2.7.1 Utambuzi wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi*

Kama ilivyofafanuliwa katika sura ya kwanza, mhusika mkinzani ni mhusika ambaye huenda kinyume na maadili ya jamii yake. Hivyo basi, Mwanaheri ndiye mhusika mkinzani katika tamthilia hii kwa sababu ameenda kinyume na maadili ya jamii yake kwa kujihusisha katika mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa yake na Bukini. Anaishia kupata ujauzito kutokana na mahusiano yake na Ali. Jambo hili linazua kutoelewana kati yake na shangazi vilevile mama yake.

## 2.8 Usawiri wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Katika sehemu hii, tumezitumikiza mbinu za usawiri wa wahusika kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia ili kubaini namna mhusika mkinzani amesawiriwa katika tamthilia hii. Hapa, mhusika mkinzani ambaye amejadiliwa ni Mjerumani pamoja na vibaraka wake wanaoshirikiana naye kuzua ukinzani ambao ni Mnyapala na Afisa wa Kijerumani.

**Mjerumani (Udongo Mwekundu)**

Rimmon-Kennan (1983), anaeleza kuwa wahusika wanaweza kusawiriwa kwa njia mbili; njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja. Kwa njia ya moja kwa moja, sifa za mhusika huelezwa kwa vivumishi vya sifa, nomino za dhahania au aina zingine za maneno. Kwa njia isiyo ya moja kwa moja, Keen (2003) anasema kuwa mhusika anaweza kusawiriwa kutokana na maelezo ya mhusika mwingine au msimulizi kumhusu. Kati ya mbinu za usawiri wa wahusika, njia hii isiyo ya moja kwa moja inaweza kuelezwa kupitia mbinu ya kuwatumia wahusika wengine. Kupitia usemi wa wahusika wengine, Mjerumani amesawiriwa kwa sifa anuwai.

Kupitia kwa maneno ya Mkichi Mjerumani amesawiriwa kama mnyanyasaji. Mjerumani alipoingia Tanzania Kusini aliwapokonya wenyeji (Wamatumbi) mashamba yao kwa nguvu na kuanzisha ukulima wa pamba. Aliwalazimisha Wamatumbi kufanya kazi katika mashamba yao na kuwatoza kodi. Huu ni unyanyasaji wa hali ya juu. Haya yanadhihirika kupitia maneno ya Mkichi yafuatayo.

> MKICHI: Udongo mwekundu bado upo nchini kwetu. Bado zaidi amechukua nchi yetu. Amechukua kwa nguvu. Sisi kama wanawake tunatazama tu. Anatulimisha kwa nguvu. Sisi tunatazama tu. Anatudai kodi, sisi tuna-ntazama tu. Anatudai sisi kodi? Ilikuwa sisi tudai yeye kodi, lakini apana! Sisi kama wanawake tumekaa tunatazama. Kuntazama huku mpaka lini? Tutakaa hivi hivi huku tukiteswa katika nchi yetu mpaka lini? (uk 4)

Katika utamaduni wa mtunzi, inabainika kutokana na maelezo ya Mkichi kwamba majukumu ya wanajamii yaligawanywa kijinsia. Wanaume walitazamiwa kuchukua silaha na kupigana na wavamizi au adui wao. Hii ndio sababu Mkichi anaonekana kushangazwa na namna hawachukui hatua kutokana na unyanyasaji kutoka kwa Mjerumani.

Aidha, kupitia kwa usemi wa Kitunda, Mjerumani amesawiriwa kama katili. Giardino (2009) anamfafanua katili kama mtu anayetenda matendo yanayomsababishia mwingine maumivu, majeraha au mateso. Wakati wa vita, Kitunda alidhihirisha wazi ukatili waliotendewa na Mjerumani kwa miaka mingi ambayo aliwatawala. Ukatili huu ndio uliowachochea Wamatumbi na kabila zingine kuingia vitani na Mjerumani ili walipize kisasi kwa ukatili waliotendewa. Yafuatayo ni maneno ya kitunda juu ya Mjerumani yanayodhihirisha ukatili aliowatendea.

> KITUNDA: Sikujua nini kilitokea. Sote tulikuwa mala moja tunataka damu tunataka kuua, tunataka kubomoa. Fikla zetu zililala na kisasi cha miaka mingi kilituvaa mala moja. Tulitaka malipizo. Na sisi tupige kama tulivyopigwa, tuue kama tulivyokuwa tunauliwa… (uk. 37)

Kutokana na kauli ya Kitunda katika dondoo hili; "Na sisi tupige kama tulivyopigwa, tuue kama tulivyokuwa tunauliwa," ni dhahiri kuwa Mjerumani alikuwa katili. Aliwapiga na hata kuwaua Wamatumbi pamoja na watu wa kabila zingine. Hali kadhalika, Kitunda anasisitiza ukatili aliouonyesha Mjerumani wakati wa vita. Watu wengi weusi waliuwawa. Kitunda anadhihirisha haya anapotaarifu watu kuhusu hali halisi ilivyokuwa vitani;

> KITUNDA: Watu wetu walizuka na lisasi sio wengi, lakini ilinitia wasiwasi. Kalibu kufika Nzizima tulipoteza tena watu katika mapigano… watu wamekufa (kur. 37-38).

Mjerumani vilevile amesawiriwa kama mwenye maarifa. Mjerumani anawazidi maarifa Wamatumbi na kabila zingine vitani. Mjerumani anajihami na bunduki nao Wamatumbi na wenzao wanajihami kwa maji waliopewa na Kinjeketile ambayo waliamini kwamba yalitoka kwa *Hongo* (mungu wao). Mjerumani ana maarifa ya kutumia bunduki kuwamiminia Wamatumbi risasi na kuwaua hadi kuishia kushinda vita:

> KITUNDA: … Lakini, lakini hapa ndio mahali penye bunduki kubwa; watu waliomo ndani ni kidogo. Wajelumani na wafwasi wao hawafiki hata lobo yetu. Lakini jambo la kuogopa ni bunduki kubwa.
>
> NGULUMBAYO: Kwa nini bunduki kubwa iogopwe na sisi tunayo silaha yetu kubwa vilevile – maji! hatu- kuambiwa kuwa mwenye kupata maji hatazulika na lisasi? Sasa unatuambia nini? Au huamini? (uk 42)

Licha ya Wajerumani kuwa wachache kuliko Wamatumbi na wenzao, kauli ya Kitunda katika dondoo hili inadhihirisha uwezo wa Mjerumani kimaarifa dhidi ya Wamatumbi

na kabila zingine. Wanawazidi maarifa ya kivita hadi wanawaua hatimaye kuvishinda vita. Kitunda anadhihirisha haya anaposema;

> KITUNDA: *(Kwa waliohudhuria)* Hivi ndivyo tulivyofikilia. Lakini tulikosa. Ngulumbayo na watu wake wakaanza kuvamia boma bila kuchukua nazali yoyote. Tulifikilia kuwa habali ya bunduki kubwa yote ilikuwa uongo mala ilianza kutema lisasi. Ngulumbayo na watu wake huku wanaimba *maji! Maji!* Hawakukimbia wala kuji- ficha. Walikwenda moja kwa moja. Mmoja baada ya mmoja- watu zaidi ya elfu walikufa (uk. 45).

Zaidi ya hayo, Mjerumani anasawiriwa kama fisadi. Rose-Ackerman (2016) anamfafanua mtu fisadi kama anayepata kitu kwa kutumia nafasi au raslimali alizo nazo kwa manufaa yake binafsi. Mjerumani anatumia raslimali alizo nazo kujifanikishia mipango yake ya kuendelea kutawala kwa udhalimu. Kupitia kwa usemi wa Mgindo na Mkichi, Mjerumani anatoa hongo ili kupata maslahi yake binafsi. Anazuia makabila anayoongoza kuungana ili wasije wakambandua nchini mwao kupitia vita.

> MNGINDO: Watu wanasema kama ukienda Kilwa na maelezo fulani anapewa chochote. Udongo mwekundu anatoa pesa nyingi kupata habali.
>
> MKICHI: Kuna watu wanalipwa kuzuia makabila yasi- ungane kufanya vita. (uk7).

Kutokana na kauli hizi, Mjerumani (ambaye amerejelewa katika dondoo kama Udongo mwekundu) anapogundua hatari ya kuungana kwa makabila haya anatumia pesa ili kudidimiza mipango yao. Analeta ukinzani kwa njia ya kuzuia umoja baina ya wapiganiaji haki. Hiki kinakuwa kikwazo kikubwa kwa Kinjeketile na wenzake kukabiliana na adui wao. Wanajawa na hofu na shauku ya uwezekano wa wao kufanikiwa katika mikakati ya kumkabili Mjerumani.

**Mnyapala**

Maendelezo sahihi ya jina hili ni 'Mnyapara'. Huyu ni mtu anayeangalia utekelezaji wa kazi kama za ukulima na za karakana bila yeye mwenyewe kushiriki. Anghalabu, huwakereketa na kuwaaibisha walio chini yake. Mnyapara ni kibaraka wa Mjerumani anayetumiwa na Mjerumani kudhulumu Wamatumbi. Analeta ukinzani katika tamthilia hii kwa kushirikiana na Mjerumani kudidimiza juhudi za nguli yaani Kinjeketile na wenzake. Anasitisha vita vya kuikomboa nchi ya Wamatumbi.

Kwa mujibu wa Keen (2003), inabainika kuwa Mnyapala amesawiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kutumia usemaji wa wahusika wengine. Kupitia usemi wa wahusika wengine, Mynapala anasawiriwa kama katili. Wafanyakazi wanapotoka kazini, wanazungumzia hali ya kazi ilivyokuwa katika shamba la Kinoo. Usemi ufuato wa Bwana wa Kwanza unamrejelea Mnyapala alivyo katili.

> BWANA WA KWANZA: Kitunda aliinuka kunyoosha mgongo,
> Mnyapala akampiga viboko (uk.3).

Kauli hii inadhihirisha namna Mnyapala anavyowadhulumu kwa kuwapiga wafanyakazi shambani. Anawasimamia nyuma wanapofanya kazi na haruhusu yeyote kunyoosha mgongo wake. Kumpiga mtu anapoitikia hali za kimwili kama kujinyoosha, kuenda myayo, ama kupangusa jasho ni ukatili usio na kifani.

Vilevile, Mnyapala amesawiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kinatiki. Natiki ni mbinu ambayo msanii hutumia kuwawezesha wahusika kushiriki mazungumzo na wenzao bila ufafanuzi na kumwachia msomaji au mtazamaji kujaliza sifa na hulka zao (Wamitila, 2002). Kutokana na mazungumzo ya Mnyapala na Kitunda, Mnyapala

anasawiriwa kama mwenye tamaa. Tamaa yake inatoka na kutambulika wakati anapomtamani Chausiku na kumuomba Kitunda amwazime;

MNYAPALA: Tuazime mtoto wako (uk. 9).

Mnyapala anamuona Chausiku kama kifaaa cha kuazimwa kitumiwe kisha kirudishiwe mwenyewe. Tamaa yake inamchochea kutoa kauli hii. Huu ni uovu wa hali ya juu kwa mwanamke ambao ni udhalimu wa wakinzani dhidi ya watawaliwa.

**Afisa wa Kijerumani**

Huyu ni mmojawapo wa wahudumu wa serikali ya Mjerumani. Anatumiwa na Mjerumani kudidimiza juhudi za kupigania ukombozi wa nchi ya Wamatumbi. Kwa mujibu wa Mwananaratolojia Rimmon-Kennan (1983), mhusika huyu amesawiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kinatiki. Kutokana na mazungumzo kati ya Afisa wa kijerumani na Kinjeketile, Afisa wa Kijerumani anatambulika kuwa mwenye hila. Mtu mwenye hila ni yule anayetumia uongo ili kupata matilaba yake. Afisa wa Kijerumani anatumia hila kumshawishi Kinjeketile kukiri kuwa maji aliyowapa watu yalikuwa ni uongo. Kwa Kinjeketile kukiri hili angekuwa anakiri kushindwa vita. Anamwahidi kuwa akikiri kwamba maji yalikuwa uongo watawaachilia huru watoto na wanawake waliowateka nyara.

AFISA: Ukisema kuwa maji ni uongo hawa watu wote- watoto na wanawake- tutawaachia (uk. 47).

Hii sio nia yake bali lengo lake ni kuona Kinjeketile akikiri kuwa maji yalikuwa uongo ishara ya kukubali kushindwa vita. Haya yanatupelekea kubaini kuwa amesawiriwa kama mwenye kuibusha vitimbi na au hila, pamoja na udanganyifu.

## 2.9 Usawiri wa Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

Nadharia ya naratolojia inaeleza njia mbili za usawiri wa mhusika, njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja. Rimmon-Kennan (1983) anaeeza kuwa, kwa njia ya moja kwa moja, sifa za mhusika huelezwa kwa kutumia vivumishi vya sifa, nomino za dhahania au aina zingine za maneno. Anafafanua njia isiyo ya moja kwa moja nayo kama inayohuhusisha maelezo ya wahusika wengine au msimulizi kuhusu mhusika fulani. Njia hizi zimedhihirika kupitia mbinu ya kimaelezo katika tamthilia hii.

Zaidi ya hayo, Rimmon-Kennan (1983) anasema kwamba, njia isiyo ya moja kwa moja inaweza kumwongoza msomaji kubainisha sifa za mhusika kwa kuchunguza mwonekano wake. Kwa kuzingatia mwonekano wa mhusika mkinzani katika tamthilia hii, njia hii imeelezwa kwa kutumia mbinu ya ulinganuzi na usambamba.

Msimulizi anaeleza sifa za joka Sesota kikamilifu kutokana na maneno aliotumia. Sesota anasawiriwa kama fisadi. Ufisadi wake unabainika kwa kuchukua visivyo vyake bila kujali madhara wanayopata wengine katika kitongoji cha Masononi. Joka hili lilikuwa na mazoea ya kuchukua mali na binti mmoja mzuri kutoka kitongoji cha Masononi. Msimulizi anasema;

> ‘Likuwa tabia makini
> Kila mwaka ukabaini
> Joka hushuka kijijini
> Kuchukua mali na binti mwema mmoja (uk. 35).

Vilevile, msimulizi anamrejelea Sesota moja kwa moja kama fisadi kutokana na hali anayoieleza kuwa;

Tena ilikuwa fisadi
Mali ya watu tangu jadi
Nao watoto wa Wadudi
Na mshenzi maluuni kuchukuliwa (uk. 36).

Pia, Sesota amesawiriwa kama maluuni. Kwa mujibu wa Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2013), maluuni ni afanyaye mambo kinyume cha jamii aishimo. Sesota ni kiumbe mlaanifu anayefanya mambo kinyume cha kaida za jamii. Anachukua mali na binti mwema kutoka kwa kijiji cha Masononi huku akiwasababishia hangaiko kubwa Wanamasononi. Sifa hii inatajwa moja kwa moja kikamilifu kutokana na maelezo yafuatayo ya msimulizi;

Hatua si hatua
Ni mdomo na pua
Lilishilo kitongojini
Sesota
Joka la vichwa sabini

Na kila aliyeona
Joka hilo maluuni
Moyo wake uliingiwa hofu
Na mashaka ya kiinsani (uk. 35).

Kutokana na dondoo hili, sifa ya Sesota ya kuwa maluuni inatajwa moja kwa moja na msimulizi. Msimulizi anamtaja kuwa maluuni kutokana na matendo maovu atendeao Wanamasononi kila mwaka. Anawatia uchungu kila mwaka Wanamasoni kwa kuwapokonya kilicho chao. Maangamizi haya yanayoletwa na Sesota yanawakosesha amani kwani yanatokea mara kwa mara.

Zaidi ya hayo, Sesota amesawiriwa kama mwenye hamaki. Gosling (2008) anaeleza kuwa, mwenye hamaki huonyesha kiwango cha juu cha mihemko na hisia zisizoweza kutabirika katika hali mbalimbali. Wanamasononi hawawezi kutabiri mihemko za

Sesota wakati wa kurudi kwake kijijini kwa awamu ya pili. Anapoingia katika kitongoji cha Masononi kwa mara ya pili anadhihirisha hamaki kubwa aliyokuwa nayo. Hamaki hii inatokana na majaribio ya Mtemi ya kukabiliana naye na kumkata kichwa kimoja. Hili linampandisha mori zaidi ndiposa anaporudi kwa awamu ya pili anakuja kwa hasira. Msimulizi anaeleza haya kupitia usemi ufuatao;

> Sesota kaja namna ya pili
> Kawa mkali ka' pilipili
> Kwa hamaki hasa ukatili
> Kitongoji kwa nguvu akajilia (uk 42).

Kutokana na dondoo hili, msimulizi anataja moja kwa moja sifa ya Sesota ya kuwa mwenye hamaki kutilia mkazo uovu wake aliokuwa anawaletea Wanamasononi. Kwa awamu ya pili anarejea katika kijiji hiki kwa hasira zaidi kuliko alivyokuwa mwanzo ili kuwatendea Wanamasononi madhila zaidi. Hali kadhalika, hamaki yake inamfanya kutenda vitendo vya kihayawani hivyo kusawiriwa kama hayawani. Sesota anadhihirisha uhayawani anapokivamia kitongoji cha Masononi na kusababisha maafa makubwa. Watu na wanyama kama paka wanakufa na kuwa majivu kutokana na moto alioutema. Moto huu vilevile unateketeza mashamba na vibanda vya Wanamasononi. Maelezo yafuatayo yanaonyesha uhayawani wa Sesota aliyowatendea Wanamasononi.

> Anapiga mikambi yake
> Anapumua moto wake
> Kuonyesha asili yake
> Ya ukatili usio na jinsia
>
> Vibanda moto vikawaka
> Mashamba yote karipuka
> Watu watoto pia paka
> Walikuwa majivu rundu kubwa moja (uk. 42).

Haya yanadhihirisha vitendo vya kinyama ambavyo Sesota anawatendea Wanamasononi. Vitendo hivi sio vya utu bali ni vya madhila makubwa na vyenye kugharimu uhai hivyo kumfanya mhusika huyu kusawiriwa kama hayawani.

Vinginevyo, Sesota amesawiriwa kama haini. Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004), haini ni mshiriki katika jambo baya. Sesota anaonekana kushiriki katika mambo mabaya katika jamii ya Wanamasononi. Msimulizi anataja sifa hii ya Sesota moja kwa moja anaposema;

> Tukangoja humu hofuni
> Kichwa cha pili cha mal'uni
> Kichwa cha Sesota haini
> Mbali ukingoni kujitokelezea (uk. 49).

Sesota anashiriki mambo mabaya kwa kuwaletea Wanamasononi maafa na mahangaiko makubwa kutokana na mavamizi yake katika kitongoji chao. Kila anapovamia kitongoji hicho, huchukua mali ya Wanamasononi pamoja na binti mmoja mwema. Mbali na hayo, anasababisha vifo vya watu, wanyama kama paka na uharibifu mkubwa wa mali. Haya yote ni mambo mabaya anayoshiriki Sesota hivyo kuwa haini.

Vilevile, Sesota amesawiriwa kama mwenye kisasi. Kisasi kinaweza kuzusha mgogoro mkali au kuleta madhara kwa yule anayetendewa. Wakati wa mapambano kati ya Mtemi na Joka hili, Mtemi anafanikiwa kulinasa na kulikata kichwa kimoja hadi likatokomea. Miaka kadhaa inapita na kunatokea ishara kuwa Sesota angerudi na kichwa cha pili. Hii inadhihirisha kisasi ambacho anawania kulipiza kwa Wanamasononi baada ya kukatwa kichwa kimoja na Mtemi. Wanamasononi wanapoona ishara ya kiwingu wanabaini fika kuwa Sesota anarejea. Maelezo yafuatayo ya msimulizi yanambainisha Sesota kuwa mwenye kisasi.

...Kilikuja kitongojini
Kiwingu kile cha haini
Na watu walisha baini
Kuwa hii ishara imewakabilia

Wale watu wal'ojuwa
Ishara 'kaitambua
Yakini wakajua
Sesota kichwa cha pili awaletea (uk. 48).

Mbali na hayo, msimulizi ameweka sambamba Joka Sesota na nyoka wa kawaida mwenye sifa kinyume na za Sesota. Ili kuwafahamisha Wanamasononi kuhusu taswira kamili ya joka Sesota, msimulizi anamweka kwenye mizani na nyoka wa kawaida. Ulinganuzi wa wahusika hawa wawili unabainisha sifa ya Sesota kuwa mwenye kutisha. Msimulizi anasema;

Huyu nyoka ndugu zanguni
Si nyoka wa hii mitini
Ajifichae majanini
Kugonga apitaye mmoya mmoya

Huyu nyoka ndugu zanguni
Siyo nyoka wa chini duni
Au yule nyoka wa majani
Mwenye sumu 'lo hafifu 'sojipandia

Huyu nyoka na'mbieni
Ni joka kubwa la zamani
Linavyo vichwa sabini
Na kila shingo yake lina lake koya (uk. 36-37).

Kutokana na dondoo hili, sifa ya Sesota inatokana na kuwepo kwa mhusika mwingine (nyoka wa kawaida) dhaifu, sifa iliyo kinyume na ya Sesota. Kutokana na mwonekano wa Sesota, msimulizi ameweka sambamba sifa za joka Sesota na nyoka wa kawaida ambaye amebainishwa kama duni na hafifu nalo Sesota ni joka kubwa lenye maumbile ya kutisha. Ulinganishaji wa wahusika hawa wawili, umeweka wazi haya na kubainisha

sifa ya Sesota kama ya mwenye kutisha na anayehitaji mikakati maalumu kuangamizwa.

Hatimaye, Sesota ni mhusika wa kimajazi anayewakilisha Wakoloni. Hawa Wakoloni walilinyakua bara la Afrika na kulitawala kwa miaka sabini. Jambo hili linadhihirika kutokana na ukweli kwamba Sesota alikuwa na vichwa sabini. Udhalimu wote ambao unafanywa dhidi ya wanakikiji na joka hili unalingana na mateso waliopitia Wafrika chini ya utawala wa kikoloni.

### 2.10 Usawiri wa Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi*

Maelezo ya Keen (2003) kuhusu usawiri wa mhusika kwa njia isiyo ya moja kwa moja yametuwezesha kutambua kuwa mhusika mkinzani katika *Arusi* amesawiriwa kupitia mbinu ya kuwatumia wahusika wengine. Maelezo ya wahusika wengine kumhusu Mwanaheri yametuwezesha kubainisha sifa zake. Mbali na kuwatumia wahusika wengine, mbinu ya kinatiki imetumika pia kubainisha usawiri wa Mwanaheri kwa kutathmini mazungumzo na matendo yake na wahusika wengine.

Kutokana na matendo na mazungunzo ya Mwanaheri na wahusika wengine, mtafiti ameweza kutathmini sifa mbalimbali za mhusika huyu. Mwanaheri amesawiriwa kama msiri. Mwanaheri anaweka siri kuhusu mahusiano yake ya kimapenzi na Ali kwa kuwa anafahamu ni haramu. Hataki Shangaziye awaone pamoja. Ali anapomtembelea, Mwanaheri anaonekana kutofurahishwa. Kutokana na mazungumzo yake na Ali, anabainika kuwa msiri:

ALI: Psst
MWANAHERI: Nani?

| | |
|---|---|
| | Ala! Wewe! mimi nimekwambia- |
| ALI : | Shh |
| | Polepole |
| MWANAHERI: | Mimi nimekwambia usije hapa. |
| | Akituona - (uk. 21). |

Mwanaheri anaposema, “akituona” inadhihirisha usiri wake ambapo hataki uhusiano wao uwe bayana. Anafahamu fika kuwa kitendo anachojihusisha nacho cha uhusiano nje ya ndoa yake halali ni haramu. Iwapo kingegundulika basi angekuwa mashakani. Hii ndio maana anazuia maongezi zaidi na Ali katika maeneo yale. Anaishia kukatiza mazungumzo yake na Ali na kumtaka aondoke ili wazungumze baadaye mbali na nyumbani kwa shangazi. Haya yanadhihirika katika mazungumzo yafuatayo;

| | |
|---|---|
| MWANAHERI: | We nenda |
| | N’takwambia baadaye |
| ALI: | Baadaye lini? |
| MWANAHERI: | Mi n’takwambia |
| ALI: | Utaniambia lini? |
| MWANAHERI: | Ntakwambia |
| ALI: | Njoo basi nyumbani (uk. 21). |

Mwanaheri vilevile amesawiriwa kinatiki kama mwongo. Anamhadaa Shangazi kuwa barua aliyo nayo imeletwa na mtoto. Anaporejea nyumbani baada ya kusemezana na Ali, hataki kusema ukweli kuwa barua anayoizungumzia Shangazi imeletwa na Ali ambaye wanachumbiana kisiri. Haya yanadhihirika kupitia mazungumzo yafuatayo;

| | |
|---|---|
| SHANGAZI: | Na hiko ni nini mikononi |
| MWANAHERI: | Hii? Barua |
| MWANAHERI: | Yako |
| SHANGAZI: | Sasa mbona umeshikilia wewe? |
| | *(Kimya, anachukua barua)*. |
| SHANGAZI: | Amekupa nani? |
| MWANAHERI: | Amenipa… |
| | Ameileta mtoto (uk. 22). |

Aidha, Mwanaheri amesawiriwa kama mwenye kutojali. Mwanaheri hajali Bukini mumewe wa ndoa atakavyohisi baada ya kurejea na kupata kuwa amemsaliti. Kitendo anachokifanya cha kuenda nje ya ndoa yake ni cha kuajabiwa hasa baada tu ya arusi yake na Bukini. Mwanaheri anaenda kinyume na maadili ya jamii yake kwa kujihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na Ali. Licha ya hayo, haonekani kama aliyetishika wala kujali hisia za Bukini, mumewe halali baada yake kurudi kutoka ng'ambo. Kupitia mazungumzo yake na Ali, tunabaini kuwa, Mwanaheri ni wa kutojali.

> ALI: Bado unaamini?
> Bukini atarudi?
> MWANAHERI: *(Anaitikia)*
> ALI: Na akirudi?
> MWANAHERI: Sijui
> Wala sitaki
> kujua hivi sasa (uk. 41).

Hatimaye, kupitia usemi wa wahusika wengine kuhusu Mwanaheri, tunabaini sifa yake kama msaliti. Anamsaliti Bukini kimapenzi anapoenda nje ya ndoa na kujihusisha katika mahusiano ya kimapenzi na Ali. Baada ya kuvikwa pete ya uchumba na kufunga arusi na Bukini, anamsaliti kimapenzi muda mfupi tu baada ya Bukini kusafiri. Licha ya Bukini kumwahidi kuwa angerudi au kumtumia tikiti baada ya miezi miwili, Mwanaheri anakosa kuwa mwaminifu. Uhusiano wake na Ali unampelekea kuambulia ujauzito nje ya ndoa. Kupitia usemi wa Shangazi, Mwanaheri anabainika kuwa msaliti.

> SHANGAZI: Na mke huyo
> Mke jina
> Maana huyo katuletea mimba sasa
> Hiyo imejaa tele. Tuseme kuwa
> mimba hiyo ya mtoto wetu hata
> siku moja…
>
> Cha kusema hapa nini?
> Cha kusema hakuna,

Hiki kitu dhahiri
Huyu mtoto ana mimba;
Mi mba hii haiwezi kuwa
Ya mumewe (uk. 27-28).

Mbali na usaliti wa njia hiyo, Mwanaheri anasaliti tena Bukini waziwazi anapoivua pete ya uchumba na kumrejeshea. Baada ya Bukini kurejea kutoka ng'ambo anashiriki mazungumzo na Mwanaheri yanayoishia katika usaliti.

BUKINI: Mbona unauvua?
MWANAHERI: Si mchezo umekwisha
BUKINI: A- a- a- a vaa-
MWANAHERI: Hata *(Anampa Bukini pete)*
Naogopa. (uk. 50).

*Arusi* pia ni tamthilia ya kijamazi inayoibua maswala ya uhusiano kati ya mifumo tofauti ya kuzalisha mali. Mifumo miwili ya kuzalisha mali inayowakilishwa kijazanda ni ujamaa iliyoendekezwa na Tanzania na ubepari iliyoendekezwa na Kenya kipindi cha baada ya ukoloni. Hii mifumo kama uhusiano kati ya Bukini (anayewakilisha Kenya) na Mwanaheri (anayewakilisha Tanzania) haitangamani.

## 2.11 Hitimisho

Sura hii imetoa maelezo kuhusu maisha ya Ebrahim Hussein namna yanavyoibua muktadha wa ukinzani katika tamthilia teule. Aidha, imeshughulikia ubainishaji wa muktadha wa mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Sehemu hii ni muhimu katika tasnifu hii kwa kuwa ndiyo sura ambayo Ebrahim Hussein amemwasilisha nayo mhusika mkinzani katika tamthilia ya *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini*. Muhtasari wa tamthilia teule umetolewa pamoja na ufasiri wake ili kurahisisha uchanganuzi wa data. Mwisho, Mbinu za usawiri wa mhusika zimejadiliwa na namna zilivyotumika kumsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia tatu teule kwa mujibu wa

nadharia ya Naratolojia. Sura ifuatayo imeshughulikia mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia teule.

# SURA YA TATU

# MHUSIKA MKINZANI NA UKUZAJI WA MGOGORO KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN

## 3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilishughulikia mbinu mbalimbali za kumsawiri mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Sura hii inashughulikia mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia teule. Dhana ya mgogoro na aina zake na namna mhusika mkinzani amekuza migogoro katika tamthila teule imeangaziwa. Katika kumzungumzia mkinzani nguli na wahusika wengine hawawezi kuepukika kwa kuwa mgogoro huhusisha mgongano baina ya pande mbili au zaidi za wahusika.

## 3.1 Dhana na Aina za Migogoro

Mgogoro ni mvutano, mkinzano, mgongano au kutoelewana kati ya mhusika mmoja na mwingine, mhusika na nafsi yake au mhusika na nguvu nyingine (Wamitila, 2003). Mgogoro ndio mhimili wa drama na bila huo basi drama haipo. Ili kueleza swala la ukuzaji wa migogoro na mhusika, inajuzu kuelewa aina mbalimbali za migogoro. Hizi zimejadiliwa kwa kina ifuatavyo.

Abrams (1999) anazungumzia mgogoro kati ya mhusika na nafsi yake. Anasema kuwa, huu ni mgogoro ambao unahusu mapambano ambayo mhusika hukabiliana nayo katika nafsi yake. Mgogoro huu unaweka wazi kuwa binadamu ana mapungufu mengi na katika harakati za kujisaka, hukumbana na vikwazo vingi. Katika hali ya kujiboresha hukinzana na vikwazo vyenyewe hivyo basi kuwa katika mgogoro wa kinafsi. Ili kusuluhisha mgogoro huu, mhusika huyu atahitaji kufanya uamuzi bora, kukashifu hofu

iliyo ndani yake, kudhibiti matamanio yake na kukabiliana na mitanziko iliyo mbele yake. Wakati mwingine wahusika wengine humsaidia kusuluhisha mgogoro huu.

Pia, kuna mgogoro kati ya binadamu na binadamu mwenzake. Garcia (2024) anasema kuwa katika mgogoro wa aina hii, nguli na mkinzani huwa na uwezo unaotofautiana. Nguli hujitahidi ili kumfikia mkinzani na kuzuia juhudi zake ili hatimaye ushindi upatikane. Anazidi kueleza kuwa mtunzi anaweza kumuumba mkinzani aliye na mapungufu ambayo nguli huyatumia kama njia ya kuibukia mshindi. Kwa upande mwingine, mtunzi humuumba mkinzani aliye na uwezo unaomzidi nguli na wafuasi wake. Mkinzani kwa ushirikiano na wanaomuunga mkono huingia katika mgogoro na nguli na wafuasi wake. Mkinzani huishia kushinda kutokana na uwezo alio nao zaidi ya nguli na wenzake. Huu ndio mgogoro uliojadiliwa katika tamthilia ya *Kinjeketile* katika sura hii kwa kina.

Vilevile, Abrams (1999) anabainisha mgogoro baina ya binadamu na maumbile ya ulimwengu. Hapa, nguli huwa binadamu naye mkinzani wake huwa maumbile ya ulimwengu kama vile mazingira yanayomzunguka binadamu. Iwapo mazingira yatakuwa nguvu kinzani, basi mtunzi atamweka nguli (binadamu) katika mazingira geni asiyofahamu na yenye kutisha. Kujinasua kutoka hali hii, atahitajika kubuni mipango kabambe na faafu ili kuibuka mshindi. Ukinzani unaozua mgogoro wa aina hii hulenga kuonyesha uwezo wa binadamu kuwa mbunifu, kukabiliana na hofu, na kuwa mvumilivu.

Madsen (2009) naye anaelezea mgogoro baina ya binadamu na malimwengu. Anasema kuwa mkinzani huwa viumbe vya kimalimwengu nje ya upeo wa ulimwengu wa kawaida ambao hukuza mgogoro dhidi ya binadamu. Viumbe hawa ni pamoja na mazimwi, miungu, pepo, malaika, jaaza na vingine. Ukinzani unaoletwa na viumbe wa kutisha au mazimwi hujengwa kwa misingi ya siri ambayo huwa ndicho kikwazo kinachojenga mgogoro na nguli au wahusika wengine. Siri hiyo inapogunduliwa ndipo inabainika kuwa nguli anaweza kukabiliana na viumbe hao na kuwashinda hivyo kutatuliwa kwa mgogoro. Aidha, maangamizi wanayosababisha hukuza mgogoro baina yao na binadamu. Ukinzani unaozua mgogoro wa aina hii ndio unaopatikana katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini* na umejadiliwa kwa kina katika sura hii.

Mwisho, Jameson (2005) anabainisha mgogoro baina ya binadamu na jamii. Anasema kwamba, mhusika hasi anapoenda kinyume na maadili ya jamii yake, husababisha kutoelewana au kukinzana baina yake na jamii inayomzunguka. Jamii inapopinga matendo ya mhusika huyu yaliyo kinyume na maadili ndipo kunapozuka mgogoro. Aina hii ya mgogoro ndio inayopatikana katika tamthilia ya *Arusi* na imejadiliwa kwa kina katika sura hii.

## 3.2 Hali Zinazochochea Mgogoro baina ya Wahusika

Mckee (2020) Anaeleza kuwa chanzo cha mgogoro katika tabia, dhima na mwelekeo wa mhusika ni nguvu zinazokinzana nafsini mwake.  Hofu, matamanio ya moyo, na visa vya awali visivyosuluhishwa humsukuma mhusika kutenda matendo ambayo humwathiri au kuwaathiri wahusika wengine wanaomzunguka. Haya husababisha migororo baina yake na wahusika wengine.

Ackenman (2022) kwa upande wake naye anabainisha vipengele vitano vinavyosababisha migogoro baina ya wahusika. Kwanza, anazungumzia swala la hofu. Anaeleza kuwa hofu ya kutofanikiwa, ya kuwa pweke, ya kumpoteza mpenzi miongoni mwa zingine, humchochea mhusika kutenda matendo ambayo yanaleta mgogoro baina yake na wengine. Mathalaan, kadri mhusika anavyokuwa na hofu ya kusababisha kushindwa kwa wenzake anaowaongoza, ndivyo atakavyofanya kila awezalo kufaulu katika kuepuka hili. Haya humsukuma mhusika kutenda matendo yanayolenga kumboresha, jambo linalomsababishia kuingia katika mgogoro na wahusika wengine. Aidha, mkinzani anapokuwa na hofu ya kushindwa na nguli pamoja na wafuasi wake, hubuni mikakati kabambe ya kudidimiza juhudi za nguli na wenzake dhidi yake.

Isitoshe, imani kuhusu maadili ya jamii huweza kuibua mgogoro. Mkinzani hutenda matendo ambayo yanaenda kinyume na maadili ya jamii yake. Maadili haya huhusisha amali za jamii ambazo zinashikilia jamii na matendo ambayo yanakubalika kuwa bora katika jamii. Hivyo, mkinzani anapoenda kinyume na maadili haya ya jamii, mgogoro baina yake na jamii huzuka.

Kadhalika, Ackenman (2022) anazungumizia kuhusu siri. Wahusika huwa na juhudi za kusitiri siri zao zisibainike kwa wahusika wengine. Kwa kufanikisha hili, mhusika anaweza kujitenga na wahusika wengine kuepuka kudadisiwa au kuchunguzwa zaidi kuhusu mambo yake yasiyojulikana. Mbali na kujitenga, mhusika huyu atabadili mienendo yake ili kuisitiri siri yake. Katika kufanya hivi kunazuka mgogoro baina yake na wahusika wengine wanaomzunguka.

Mwisho, anafafanua kipengele cha kuweka dhahiri kisa cha awali. Katika kutekeleza hili, makovu huzinduliwa na hali mbaya ya awali aliyopitia mhusika humjia katika fikra zake. Haya huwa kichocheo cha mhusika kuingia katika mgogoro na wahusika wengine. Mfano mwafaka ni mhusika Edipode katika tamthilia ya *Mfalme Edipode* (1969).

Kwa ujumla, maelezo ya Mckee na Ackenman yanarejelea msukumo wa ndani ya nafsi ambao humchochea mhusika kuingia katika mgogoro na mhusika mwingine. Msukumo huu huhusisha hofu ya ndani, shinikizo la kutaka kuzingatia au kutozingatia maadili ya jamii, haja ya kutaka kusitiri siri na matamanio ya moyo ya mhusika. Msukumo wa ndani wa mkinzani ni kukiuka maadili ya jamii yake na matamanio yake ya moyo hulenga kudidimiza juhudi za nguli pamoja na wafuasi wake dhidi yake.

### 3.3 Namna Mkinzani Anavyokuza Mgogoro

Laura (2016) anabainisha vigezo mbalimbali vya kuzingatia katika kuchunguza na kuchanganua namna mkinzani anavyopelekea kuwepo kwa mgogoro katika drama. Miongoni mwa vigezo hivi ni uchunguzi wa kichocheo cha mkinzani. Hapa, hulka ya mkinzani hutuelekeza kuchunguza anachokithamini mkinzani na namna kinavyomchochea kutenda namna anavyotenda. Aidha, kinachomchochea mkinzani kutenda matendo anayotenda hutuwezesha kufahamu mambo anayopania kutimiza na jinsi yanavyoathiri uamuzi wake. Katika kutekeleza haya mkinzani hujikuta katika migogoro na wahusika wengine halikadhalika jamii inayomzunguka.

Pia, mhakiki anaweza kuchunguza mtatizo ambayo mkinzani anamsababishia nguli na wafuasi wake. Mkinzani anapowasababishia wahusika wengine matatizo, wahusika hao

hupata msukumo wa kujitahidi ili kukabiliana na matatizo hayo. Katika juhudi za kutekeleza haya, mgogoro huzuka baina yao. Hivyo, mhakiki huanza na kubainisha tatizo kuu ambalo mkinzani anazusha, namna linavyomwathiri nguli na wafuasi wake kisha jinsi nguli na wafuasi wake wanavyokabiliana na tatizo hilo.

Mbali na hayo, Laura  anasema kuwa, mhakiki anaweza kuchunguza namna mkinzani anavyotagusana na nguli pamoja na wahusika wengine. Katika kukuza mgogoro, mhusika mkinzani hutagusana na nguli pamoja na wahusika wengine aidha moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Iwapo mhusika mkinzani amewasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa, mtagusano wake na wahusika wengine ni wa moja kwa moja. Kwa upande mwingine, iwapo mkinzani amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa, mtagusano wake ni wa njia isiyo ya moja kwa moja (Laura, 2016). Anazidi kueleza kuwa tunavyochunguza mtagusano wa mhusika mkinzani na wahusika wengine, huwa tunaongozwa na nguzo madhubuti. Nguzo hizi ni ubainishaji wa aina ya mtagusano, sifa za mkizani zinazotokana na mtagusano huo, matendo yanayoibuka kutokana na mtagusano na namna yanavyokuza mgogoro.

Vilevile, mhakiki anaweza kuchunguza mandhari anayoumba mhusika mkinzani. Mandhari ambayo mhusika mkinzani huumba huweza kuwa kichocheo cha mgogoro katika drama. Katika kufanikisha hili, kinachochunguzwa ni aina ya mandhari ambayo mkinzani anaumba, namna yanavyowaathiri wahusika wengine na namna mandhari hayo yanachochea matendo ya mkinzani na wahusika wengine. Iwapo mkinzani ataumba mandhari ambayo yanamfanya kuwa mwenye uwezo zaidi ya wahusika

wengine, basi hili litawachochea wahusika hao kutafuta mbinu ya kukabiliana naye ili kuibukia washindi. Katika kufanya hili, kutazuka mgogoro baina yao.

Isitoshe, mhakiki anaweza kuchunguza nguvu kani za ndani au za nje ambazo zinabainika kama nguvu kinzani. Katika kazi zingine za drama, ukinzani huwa nguvu fulani kutoka ndani au nje ya mchezo ambazo huwa kikwazo kwa nguli na wahusika wengine katika juhudi zao za kutenda mema (Laura 2016). Tunapochunguza hili, huwa tunaongozwa na vipengele mbalimbali, ambavyo ni pamoja na ubainishaji wa nguvu kinzani katika drama na namna nguvu hizi zinavyowazuia wahusika wengine kuyaafikia malengo yao ya kutenda mema. Pia, kuna uchunguzi wa hofu ambayo nguvu hizi zinawasababishia wahusika wengine na namna hofu hiyo inavyowachochea kutenda matendo ya kudidimiza juhudi za nguvu hizo kinzani. Mchakato huu unasaidia kubaini mgogoro unavyozuka kati ya pande hizi kinzani.

Mwisho, Laura (2016) anasema kwamba mhakiki anaweza kuchunguza nafasi ya mhusika mkinzani katika ukuzaji wa ploti. Katika kuelezea ploti ya drama, migogoro iliyomo hushughulikiwa moja kwa moja kwani ukuaji wa ploti hujumuisha migogoro. Tunachunguza namna mkinzani anavyoanzisha migogoro katika drama, namna anavyoikuza na nafasi yake katika kuisuluhisha migogoro husika.

Kwa muhtasari, Laura amebainisha vipengele muhimu vya kumuongoza mhakiki katika uchanganuzi wa mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia. Vipengele hivi ni pamoja na uchunguzi wa kichocheo cha mkinzani, mandhari anayoumba mkinzani, matatizo ambayo mkinzani anawasababishia wahusika wengine, mtagusano

wa mkinzani na wahusika wengine na namna mkinzani anavyokuza ploti. Vipengele hivi kumhusu mkinzani huchochea matendo yake na ya wahusika wengine ambayo yanakuza mgogoro katika drama. Haya yamejadiliwa kwa kina kwa mujibu wa tamthilia teule kwa kuongozwa na nadharia ya Drama katika sehemu ifuatayo.

### 3.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro Katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Jung (1964) anaeleza kuwa wahusika katika drama huwa na msukumo wa ndani ya nafsi zao unaochochea matendo ambayo husababisha mgogoro. Msukumo huu hutokana na sifa fulani za kisaikolojia ambazo ni hofu ya ndani, hisia, kisa cha awali cha mhusika kilichofichika, imani, matendo, matamanio ya moyo na nia. Matamanio na nia ya mkinzani vinatazamiwa kusisimua hofu ya nguli na wenzake. Vivyo hivyo matamanio na nia ya nguli vinatarajiwa kuzindua hofu ya mkinzani. Matokeo yake ndicho kiini cha mgogoro baina yao. Mihimili hii ndiyo imetuongoza katika kuchunguza na kuchanganua mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia teule huku tukizingatia na kuvitumikiza vipengele alivyoeleza Laura (2016). Haya yamejadiliwa kwa kina katika sehemu zifuatazo.

#### 3.4.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani

Katika kuchunguza hili, tumebainisha anachokithamini mhusika mkinzani kwa kuwa ndicho kinachomchochea kuchukua uamuzi wa kutenda matendo yanayoibua mgogoro kati yake na wahusika wengine. Vilevile, mambo anayopania kutimiza mkinzani humchochea kutenda matendo yanayomwingiza katika mgogoro na nguli pamoja na wahusika wengine. Katika *Kinjeketile*, Mjerumani ambaye ndiye mkinzani anathamini

ukulima wa pamba. Hili linamchochea kuchukua uamuzi wa kunyakua ardhi ya Wamatumbi na kuanzisha ukulima wa pamba. Tunaelezwa katika kitangulizi kuwa;

> Hapo mwanzo wa karne hii, mabepari wa Kijerumani walianzisha kulimisha pamba huko Tanzania Kusini. Waliwalazimisha Wamatumbi kufanya kazi katika mashamba yao. Pamba iliyopatikana ilipelekwa Ujerumani (kur. v-vi).

Kitendo cha kunyakua ardhi ya Wamatumbi kinafuatiwa na udhalimu ambapo Mjerumani anawalazimisha Wamatumbi kufanya kazi za shokoa katika mashamba ya pamba. Kazi hizi zinaandamana na dhulma kwani vibaraka wa Mjerumani; Mnyapala na Jumbe wanawasimamia wafanyakazi wanapokuwa shambani huku wakiwachapa. Bwana wa kwanza anadhihirisha haya anaposema;

> BWANA WA KWANZA: Kitunda aliinuka kunyoosha mgongo Mnyapala akampiga kiboko (uk.3).

Dhulma hii ya vibaraka wa mkinzani inachochea hasira na msisimko mioyoni mwa Wamatumbi hivyo kuwa na msukumo wa kuingia vitani na Mjerumani. Wamatumbi hawapo tayari kustahimili unyanyasaji huu kutoka kwa Mjerumani. Mgindo anasema;

> MGINDO: Tumwondoe – Tukate shauri sasa hivi – Vita. Akuna jingine (uk. 4).

Kichocheo cha Mjerumani kinampelekea kutenda kitendo cha kunyakua ardhi ya Wamatumbi huku akiwadhulumu. Baadaye kinakuwa kichocheo cha Wamatumbi kuungana na kuanzisha vita dhidhi ya Mjerumani. Hivyo, kunazuka mgogoro wa kivita kati ya Wamatumbi kwa ushirikiano na kabila zingine dhidi ya Mjerumani.

### 3.4.2 Matatizo Anayosababisha Mhusika Mkinzani

Chanzo kingine cha mgogoro katika drama ni matatizo ambayo mkinzani anawasababishia wahusika wengine. Kulingana na Laura (2016), matatizo yanayoletwa na mkinzani huzindua hofu ya wahusika wengine na kuwafanya kutafuta mbinu ya kukabiliana nayo. Katika kufanya hili, mgogoro unazuka kati yao na mkinzani. Mjerumani anawasababishia Wamatumbi matatizo kadha wa kadha. Miongoni mwa hayo ni kuwadai wenyeji kodi ilhali ndiye mgeni nchini humo. Mkichi analalamikia matatizo haya yanayoletwa na Mjerumani anaposema;

> MKICHI: …Anatudai sisi kodi. Sisi tuna- ntazama tu. Anatudai sisi kodi? Ilikuwa sisi tudai yeye kodi (uk. 4).

Mbali na kuwadai kodi, Mjerumani anashirikiana na vibaraka wake kuwachukua wanawake kwa nguvu kwa lengo la kuwadhulumu kimapenzi. Mjerumani anaonyesha ubabe wake kwa walio wanyonge hasa wanawake ambao hawawezi kuwalimia mashambani kama wanavyofanywa wanaume. Kupitia mazungumzo kati ya Kinjeketile na Kitunda, Tunaona dhulma kutoka kwa Mjerumani na vibaraka wake dhidi ya wanawake.

> KINJEKETILE: Usinidanganye, huna lolote. Mtoto wako wa kike kachukuliwa kwa nguvu na askali juzi juzi… (uk. 25).

Kutokana na dondoo hili, ni mwanawe Kitunda, Chausiku, ambaye anachukuliwa kwa nguvu na vibaraka wa Mjerumani; Mnyapala na Askari. Kitendo cha kumchukua Chausiku kwa nguvu kinasababisha kuzuka kwa mgogoro baina ya Bi. Kitunnda na watu wanaokuja kumsaidia. Bi. Kitunda anapandwa na mori na kuwafukuza waliokuja kumsaidia.

BI. KITUNDA: Tokeni! Tokeni! Wanawake wakubwa nyi! Vijitu viwili vinawatisheni – nyinyi nyote. Mmetawaliwa miili mpaka mioyo. Eti nyinyi wanaume kweli. Kweli Wamatumbi. Hata kidogo. Wanawake tu, nyinyi mnalimishwa – ndiyo. Wake zenu wanachukuliwa - ndiyo. Watoto wenu wanachukuliwa – ndiyo. Watu wa ndiyo. Sasa mmekuja kufanya nini? ... Sitaki msaada wenu. Tokeni! (uk. 9).

Zaidi ya hayo, Mjerumani anawasababishia Wamatumbi njaa. Kitendo cha kunyakua ardhi ya Wamatumbi na kuwalazimisha wanaume kufanya kazi shambani humo kinawasbabishia matatizo ya njaa. Wanaume wenye kutafuta riziki wanashinda shambani kwa malipo duni sana jambo linalowafanya kushindwa kuwajibikia familia zao. Kutokana na mazungumzo kati ya Bi. Kitunda na Bi. Kinjeketile tatizo la njaa linaloletwa na vitendo vya madhila vya Mjerumani linabainika.

BI. KINJEKETILE: Kweli Bi. Kitunda. Hata mimi naona taabu kupata chakula. Njaa.

BI. KITUNDA: Isiwe njaa namna gani, wanaume wenyewe wote wanalima shambani kwa Bwana Kinoo? Njaa itakosa wapi? (uk. 2).

Matatizo ya njaa, utozwaji wa kodi, dhulma kwa wanawake na mengine yote yanaletwa na Mjerumani kwa ushirikiano na vibaraka wake. Matatizo haya yanazindua hofu ya Wamatumbi jambo linalowafanya kuwa na nia ya kuungana na watu wa makabila mengine ili kuingia katika mgogoro wa kivita na Mjerumani.

### 3.4.3 Mtagusano wa Mkinzani na Wahusika Wengine

Kama ilivyobainishwa mbeleni, mhusika mkinzani ambaye ni Mjerumani katika tamthilia ya *Kinjeketile* amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa hivyo anatagusana na wahusika wengine kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Anatagusana

na nguli ambaye ni Kinjeketile pamoja na wafuasi wake kupitia vibaraka wake pia kupitia athari ya matendo yake. Mtagusano huu unazua mgogoro kati ya pande hizi mbili kwa njia mbalimbali. Mjerumani anawatumia vibaraka wake kama Mnyapala na Askari kupata habari muhimu kuhusu mipango ya Wamatumbi ya kuwakabili kwa njia ya vita. Kitunda anadhihirisha hili anaposema;

> KITUNDA: Kusema maneno unayosema ni lahisi. Sote sisi tunataka Njelumani aondoke. Lakini tutamuondoaje?
> Kwanza yeye ana silaha, sisi atuna. Jambo la kufanya ni kuanza kukusanyakusanya silaha – kuiba bunduki za askali, kunyang'anya, kufanya chini juu ili tupate silaha. Hili haliwezi kufanyika mala moja. Tena basi itakuwa vigumu kulifanya maana hivi sasa kuna vibalaka chungu nzima. Utakachofanya, akina askali au Mnyapala kesha sikia… (uk.5).

Zaidi ya hayo, Mjerumani anawahonga vibaraka wake ili apate habari kuhusu mipango ya Wamatumbi dhidi yao. Anatumia mbinu hii kuwafahamu wapinzani wake ili alemaze juhudi zao. Mgindo anasema;

> MGINDO: … Udongo Mwekundu anatoa pesa nyingi ili kupata habali. (uk. 6).

Wamatumbi wanapofahamu kuhusu njama anayotumia mkinzani wao kutagusana nao, wanachochewa kuandaa mpango kabambe wa kukabiliana naye. Wanapanga njama ya kuungana na makabila mengine ili kukabiliana na Mjerumani kwa njia ya vita vinavyoishia kwa mgogoro mkali baina ya pande hizi mbili.

### 3.4.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Kinjeketile*

Katika kuelezea ukuaji wa ploti ya drama, swala la mgogoro haliepukiki kwa kuwa vyote hivi vinaenda sambamba. Ukuaji wa ploti unajumuisha mwanzo wa mgogoro, ukuaji wake, kilele cha mgogoro na suluhisho lake. Katika kuelezea swala la ploti na

mgogoro, mtaalamu Freytag Gustav anajitokeza kuwa na nafasi kubwa kutokana na ufafanuzi wake kulihusu. Freytag (1863; 1997) ameelezea ploti na mgogoro katika drama akitumia umbo la piramidi. Hivyo, tumeitumia piramidi ya Freitag kuelezea namna mhusika mkinzani anavyokuza mgogoro katika tamthilia ya *Kinjeketile*.

Umbo hili la piramidi ya Freytag linabainisha sehemu tano zinazoelezea mgogoro. Sehemu hizi ni utangulizi, utata, kilele, mshuko na kiliwazo. Katika utangulizi, Freytag (1863; 1997) anaeleza kuwa, tunafahamishwa kuhusu wahusika, visa vyao vya awali na uhusiano baina yao. Pia, mgogoro wa kimsingi unatambulishwa hivi kwamba kiini cha ukinzani au kutoelewana baina ya mhusika mkinzani na wahusika wengine kinawekwa wazi. Katika *Kinjeketile*, tunafahamishwa kuhusu wahusika na uhusiano wao. Tunaelezwa kuhusu Mjerumani ambaye hana uhusiano mwema na Wamatumbi na watu wa kabila zingine kutokana na matendo yake ya kidhalimu. Anashirikiana na vibaraka wake kama vile Myapala na Askari kuwadhulumu wengine. Mjerumani anabainika kuwa chanzo cha mgogoro baina yake na Wamatumbi pamoja na watu wa kabila zingine kutokana na dhulma ya kuwapokonya ardhi, kuwatoza kodi na kuwatesa shambani.

Sehemu ya pili ya piramidi ya Freytag ni utata. Hapa, Freytag anasema kwamba kuna kupanda kwa wasiwasi au msisimko wa wahusika wengine kutokana na matendo ya mkinzani. Mhusika mkinzani anaweka vikwazo vingi dhidi ya nguli na wafuasi wake katika mipango yao ya kuyaafikia malengo yao. Wapo wahusika wengine wanaoungana na mhusika mkinzani katika kuweka vikwazo hivi. Katika tamthilia ya *Kijeketile*, Mjerumani anamwekea nguli (Kinjeketile) na wafuasi wake vikwazo vingi ili

kudidimiza mipango yao dhidi yake. Anawahonga vibaraka wake kama 'Askali' na Mnyapala ili kufahamu kuhusu mipango yao. Pia anawatumia vibaraka wake kutia woga katika mioyo za nguli na wafuasi wake kwa kuwachukua mabinti wao kwa nguvu na kuwadhulumu kingono. Hili linazidisha wasiwasi halikadhalika msisimko miongoni mwa Kinjeketile na wenzake na kuwa kichocheo cha mgogoro wa kivita dhidi ya Mjerumani**.**

Sehemu ya kilele ambayo ndiyo ya tatu kwenye umbo hili inazungumzia kufika kwa mgogoro kwenye kilele. Katika sehemu hii, mkinzani anaathiri mustakabali wa nguli na wote wanaomuunga mkono. Mkinzani anatenda matendo ambayo yatapelekea kushindwa kwa nguli na walio upande wake. Mwelekeo wa nguli unaanza kuonekana kutokana na matendo ya mkinzani. Mgogoro wa kivita unaohusisha Mjerumani dhidi ya Wamatumbi na makabila mengine unafikia kilele ambapo Mjerumani anawaua watu wengi sana vitani. Haya yanadhihirika kupitia usemi wa Kitunda;

> KITUNDA: … Tulipoteza katika kikundi chetu watu zaidi ya elfu moja
> na mia mbili… (uk. 45).

Mbali na kuwaua watu wengi, Mjerumani anamkamata Kinjeketile (nguli) hivyo kuonyesha mustakabali wake katika mgogoro baina yao. Kinjeketile anaelelezea hili anapoulizwa na Kitunda namna alivyofika katika ngome ya adui wao.

> KINJEKETILE: Wiki baada ya kuanza vita, Wajerumani walikuja
> kunikamata Nikahamishwa boma mbili – hii ya pili
> (uk. 48).

Sehemu ya nne inahusu mshuko. Katika sehemu hii, mgogoro uliokuzwa na mkinzani unaanza kukaribia suluhisho. Kulingana na Freytag (keshatajwa) katika tamthilia

zingine mgogoro unaweza kukosa kufikia suluhisho na kuacha wasomaji katika hali ya taharuki. Katika tamthilia ya *Kinjeketile,* Mjerumani anabainika kama mshindi wa mgogoro wa kivita kwani anapomkamata Kinjeketile kiongozi wa watu, matumani ya watu wake yanafifia. Watu wanamshinikiza Kinjeketile akiri anachoamriwa na Askari kuwa maji aliyowapa yalikuwa uongo. Hii ni ishara ya kukubali kushindwa na Mjerumani.

> AFISA: Ukisema kuwa maji ni uwongo hawa watu wote - watoto na wanawake – tutawaachilia.
> MTU I: Sema kama utasema! Au kwa sababu sisi si Wamatumbi wenzio?...
> MTU III: Sema! Tuna watoto sisi. Tufikirie. Wafikirie watoto (kur. 47-48).

Sehemu ya mwisho piramidi ya Freytag inahusu kiliwazo. Mwisho unaweza kuwa kushinda kwa mkinzani au kushindwa kwa nguli. Matendo ya mkinzani husababisha kushindwa kwa nguli jambo linalompa mkizani utulivu. Kitendo cha wafuasi wa Kinjeketile kumgeukia Kinjeketile na kumshinikiza kukiri kuwa maji aliyowapa yalikuwa ya uongo kinadhihirisha kushindwa kwao hivyo kumpa Mjerumani utulivu.

### 3.5 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro katika *Jogoo Kijijini*

Kama ilivyobainishwa katika sura ya pili kuwa mhusika mkinzani katika tamthilia hii ni Sesota, joka lenye vichwa sabini. Mhusika huyu amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa ila matendo anayotenda, kama yanavyoelezwa na msimulizi, yanawaathiri Wanamasononi moja kwa moja. Hili linawafanya Wanamasononi kutafuta mbinu ya kukabiliana naye, hivyo kuzuka kwa mgogoro. Kwa kuongozwa na nadharia ya Drama, tumezingatia vipengele vilivyoelezwa na Laura na kumfafanua mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia hii.

### 3.5.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani

Laura (2016) anasema kwamba kichocheo cha mkinzani kinatokana na kile anachokithamini pamoja na nia yake. Haya yanamfanya kuchukua uamuzi wa kutenda matendo ambayo yanachochea mgogoro baina yake na wahusika wengine. Sesota anachochewa na tamaa. Joka hili lina tamaa ya kupora mali na kunyakua mabinti kutoka kitongoji cha Masononi. Tamaa hii inamsukuma kutenda kitendo hiki kinachowaathiri Wanamasononi pakubwa. Anathamini sana kujinufaisha bila kujali athari anayowaletea Wanamasononi. Kila mwaka joka hili linaongozwa na tamaa na kukivamia kijiji cha Masononi huku likinyakua mali na binti mmoja mwema. Msimulizi anasema;

> Kwani
> ‘Likuwa tabia makini
> Killa mwaka ukibaini
> Joka hushuka kijijini
> Kuchukua mali na binti Mwema mmoya (uk. 35).

Tamaa hii ya Sesota inasisimua hofu ya Wanamasononi. Kupoteza kwa mali na mabinti kila mwaka ni jambo la kuogofya kwa Wanamasononi. Wanaamua kukabiliana na Joka hili ili kuepusha madhara zaidi. Wanaandaa mkutano ambapo wanamteua Mtemi wa kukabiliana na Joka hili. Msimulizi anasema;

> Ama
> Yafaa sana tutafuteni
> Sisi wetu hapa Mtemi
> Kijana; wala siye mimi
> Atakayepambana na Joka pamoya (uk. 37).

Hatua hii wanayoichukua inahusisha kupanga njia mwafaka ya kukabiliana na Joka lenyewe. Wanatafuta silaha na ngao ya jadi ambazo Mtemi angejihami nazo vitani. Nia ya Wanamasononi kuingia vitani na Sesota inatokana na matendo maovu ya Joka hili.

Hili linadhihirisha kuwa Sesota ndiye chanzo cha mgogoro wa kivita baina yake na Wanamasononi.

### 3.5.2 Matatizo Yanayoletwa na Mhusika Mkinzani

Matatizo yanayoletwa na mkinzani yanachangia kuzuka kwa mgogoro. Sesota anwaletea Wanamasononi maangamizi makubwa kutokana na kimbunga anachozusha. Anapokivamia kijiji cha Masononi, anazusha kimbunga kikubwa. Kimbunga hiki kinasababisha kuteseka kwa watoto. Mateso haya yanadhihirishwa na msimulizi anaposema;

> Watoto wakaachama
> Wakaachama aaah' wakaachama
> Basi hapo hapo
> Katika kimbunga wakajikaukia (uk. 41).

Pia, Sesota anautema moto ambao unawaletea Wanamasononi maafa ya watoto na wanyama pamoja na kuteketea kwa vibanda na mashamba. Joka hili linapoonyesha dalili za kurudi tena kuwaletea matatizo mengine, hofu ya Wanamasononi inapanda na kuwasababishia mgogoro wa kinafsi. Wanajikuta katika hali ya mtanziko na ukinzani nafsini mwao wanapoona kiwingu kinachoonyesha dalili ya kurudi kwa Sesota. Msimulizi anasema;

> Watu akili zikawapaa
> Hapa
> Jambo gani la kufaa? (uk. 48).

Maneno ya msimulizi katika dondoo hii kwamba akili za watu ziliwapaa na kushindwa jambo la kufanya lililo bora yanaonyesha mgogoro wa kinafsi waliokuwa nao kutokana na matatizo ya Sesota. Ishara ya kurudi kwa Sesota kupitia kiwingu kilichoonekana inawejengea taswira ya woga kutokana na matendo ya madhila ya Sesota. Wanabaki

kuwazia kwa hofu kubwa kiwango cha mateso wanachotarajia kupata Sesota atakapotua kijijini mwao tena.

### 3.5.3 Mandhari Anayoumba Mhusika Mkinzani

Mandhari ni mahali ambapo wahusika hukaa na kuingiliana katika kazi ya fasihi (Njogu na Chimerah, 1999). Hutcheon (2000) anaweka bayana aina za mandhari ambayo ni halisi na ya kufikirika. Anafafanua kuwa, mandhari halisi ni mahali ambapo ni pa kawaida panapoweza kupatikana katika ulimwengu wa kawaida. Hapa ni kama porini, ufuoni, nyumbani, sokoni miongoni mwa kwingine.

Kwa upande mwingine, anaeleza mandhari ya kufikirika kama mandhari ambayo hayawezi kufasirika katika ulimwengu halisi. Kutokana na matendo ya kiajabu ya mhusika na maumbile yake ya kiajabu, anaumba mandhari ambayo ni ya kuwaziwa au kufikirika tu. Aina hii ya mandhari ndiyo anayoumba Sesota katika tamthilia hii. Joka hili lina maumbile ya kiajabu ambayo hayawezi kufasirika katika ulimwengu halisi. Kiumbe chenye vichwa sabini ni cha kufikirika au kuwaziwa tu. Msimulizi anaeleza maumbile ya Joka hili anaposema;

> Hatua si hatua
> Ni midomo na pua
> Liliishi kitongojini
> Sesota
> Joka la vichwa sabiini (uk. 34).

Mandhari haya anamopatikana Sesota, yanamfanya kuwa mwenye nguvu na uwezo zaidi kuliko Wanamasononi. Hili linasisismua hofu ya Wanamasononi na kuwachochea kupanga mikakati ya namna ya kukabiliana na Joka hili. Huku wakizingatia kuwa mkinzani wao ana nguvu zaidi kuwaliko, wanatafuta ngao ya jadi na mkuki wa miujiza

ili kuweza kukabiliana nalo. Wanakuwa tayari kwa mgogoro wa kivita na Joka hili wakiongozwa na Mtemi ambaye walimteua na kumpa silaha hizi. Msimulizi anasema;

> Ngao ya jadi
> hadharani ikaletwa
> Mkuki janabi
> Vumbi ukafutwa
> Na watu wakaahidi
> Mtemi zana kampatia (uk. 38).

Mandhari ya kufikirika anayoumba Sesota yanachagia ukuaji wa mgogoro baina yake na Wanamasononi kwa kuwa yanamchora kuwa mwenye nguvu na uwezo zaidi. Hili linawachochea Wanamasononi kutafuta mbinu bora ya silaha ya kukabiliana nalo kutokana na uwezo wao duni. Wanapopata silaha hizi wanajihisi kama waliopigwa jeki kidogo hivyo kuingia katika mgogoro wa kivita na joka hili wakiongozwa na Mtemi.

### 3.5.4 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Jogoo Kijijini*

Ili kueleza namna mhusika mkinzani anavyokuza ploti ya tamthilia hii, piramidi ya Freytag inayoeleza ukuaji wa ploti katika drama imetuongoza. Nguzo inayojenga ploti ni mgogoro hivyo mwanzo wa mgogoro, kilele chake na suluhisho vimejadiliwa. Tumerejelea vitengo vitano vya umbo la piramidi aliloumba Freytag (1863; 1997) kuelezea ukuaji wa ploti ya tamthilia ya *Jogoo Kijijini.*

Sehemu ya kwanza ya piramidi ya Freytag ni utangulizi. Katika kitengo hiki tunafahamishwa kuhusu wahusika, uhusiano wao na visa vyao vya awali. Pia mgogoro wa kimsingi unatambulishwa. Katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*, tunafahamishwa kuhusu wahusika ambao ni Wanamasononi na mkinzani wao ambaye ni Sesota. Uhusiano wao si mwema kwani Sesota anawatesa Wanamasononi kwa kuwapora mali

na mabinti wao. Sesota ametia hofu mioyoni mwa Wanamasononi kutokana na madhila anayowatendea. Mgogoro wa kimsingi unaotangulizwa katika sehemu hii unatokana na matendo haya maovu ya Sesota dhidi ya Wanamasononi. Matendo ya Sesota yanaleta msisimko wa Wanamasononi kuingia katika mgogoro wa kivita na Sesota. Msimulizi anadhihirisha haya anaposema;

> Hapo
> Umati uliamua
> Ikawa hakuna kurudi nyuma
> Hata vilevile nyuma
> Jiwe au mtoto walijibebea (uk. 35).

Sehemu ya pili ya umbo hili ni utata. Katika kitengo hiki mkinzani anawasababishia wahusika wengine hofu zaidi. Vikwazo vya mkinzani vinabainika wazi na vinamzuia pakubwa nguli na wahusika wengine kuafikia malengo yao. Katika tamthilia hii Sesota anawazidishia hofu nyingi Wanamasononi kutokana na kitendo cha kuchukua mali na binti kila mwaka. Msimulizi anasema;

> Na killa aliyeona
> Joka hilo maluuni
> Moyo wake ‘liingiwa hofu
> Na mashaka kiinsani  (uk. 35).

Aidha, vikwazo vya Sesota vinabainika kutokana na uwezo wake wa kimaumbile unaomfanya kuwazidi nguvu na maarifa Wanamasononi. Maumbile ya kiajabu ya joka hili yanamfanya Ajuza katika kitongoji hiki kuyaona kama kikwazo kikubwa wanapojiandaa kukabiliana nalo. Ajuza huyu anasema;

> Huyu nyoka na’ambieni
> Ni joka kubwa la zamani
> Linavyo vichwa sabiini
> Na killa shingo yake ina koya (uk. 37).

Sehemu ya tatu ya umbo hili ni kilele. Hapa, mgogoro unafikia kilele. Katika makabilino, mkinzani anaibukia mshindi. Matendo ya mkinzani yanaonyesha mustakabali wa nguli na wenzake. Mgogoro wa kivita kati ya Mtemi na Sesota unafikia kilele wakati Mtemi analikata Joka hili kichwa kimoja nalo linaitema sumu kali mwilini mwa Mtemi. Hili linaonyesha mustakabali wa Mtemi kwani ndiye anayeathirika kutokana na makabiliano yao.

> Tena alibaini
> Sumu ya Joka
> Kumbe ilibakia pale kijijini
> Mwake mwilini
> Harufu chafu na najisi ilibakia!
>
> …Ukweli huu ulimchoma sana
> Humo rohoni ukachochota sana… (kur. 46-47).

Kutokana na dondoo hili, kitendo cha Sesota kuitema sumu kali mwilini mwa Mtemi kinamwathiri sana Mtemi. Aidha, kinaonyesha mustakabali wake kwani anaonekena aliye na maumivu makubwa moyoni na kuanza kutafuta njia ya kuondoa najisi hiyo iliyomwingia.

Sehemu ya nne ni mshuko. Katika kitengo hiki, hatima ya matukio inaanza kubainika. Mgogoro uliozushwa na mkinzani unaanza kufikia suluhisho. Katika tamthilia hii, hatima ya mgogoro wa kivita kati ya Mtemi na Sesota inaanza kubainika. Sesota anapomwachia Mtemi sumu mwilini mwake wakati wa makabiliano, Mtemi analazimika kujiondoa kwa ajili ya utakaso. Anaonekana kusikitishwa sana na kitendo hiki cha Sesota kumtia najisi ya sumu mwilini mwake.

> Akazingatia akazingatia na akaona
> Atafute maji ya kujitakasa (uk.47)

Mwisho ni sehemu ya kiliwazo. Hii ndio sehemu inayoonyesha hatima ya matendo. Matendo ya mkinzani yanaleta utulivu aidha kwake, kwa upande wa nguli au yawakoseshe nguli na wenzake utulivu (Freytag, 1863; 1997). Katika *Jogoo kijijini* Sesota anabainika kama mshindi wa makabiliano baina yake na Mtemi hadi kutishia kurudi tena kijijini kwa awamu nyingine. Dalili za kurudi tena zinadhihirisha ushindi wake katika makabiliano ya awali. Hata hivyo, matukio ya tamthilia hii yanaishia katika taharuki ambapo hali ya sintofahamu inabainika miongoni mwa Wanamasononi wanapoona dalili ya kurudi kwa Sesota huku wakifahamu kuwa Mtemi wa kukabiliana naye hayupo. Haya yanadhihirishwa na maneno yafuatayo ya msimulizi.

> Tukangoja humu hofuni
> Kichwa cha pili cha mal'uni
> Kichwa cha Sesota haini
> Mbali ukingoni kujitokelezea (uk.49).

**3.6 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Mgogoro katika Tamthilia ya *Arusi***

Kama ilivyobainishwa katika sura ya pili, Mwanaheri ndiye mhusika mkinzani kwa kuwa anaenda kinyume na maadili ya jamii yake. Elam (1980) anamrejelea Polti (1921) na kuchangia nadharia ya Drama kwa kufafanua ukinzani wa aina mbili na namna unavyokuza mgogoro. Anaeleza ukinzani wa kiitikadi ambapo mhuskika mkinzani hutofautiana na kuenda kinyume na itikadi za jamii yake jambo linalosababisha kuzuka kwa mgogoro. Katika *Arusi*, maadili ya jamii ya Mwanaheri hayamruhusu mtu kujihusisha katika mahusiano ya kimapenzi nje ya ndoa. Punde tu baada ya arusi yake na Bukini, Mwanaheri anajihusisha katika uhusiano wa kimapenzi na Ali na kuishia kupata ujauzito. Kitendo hiki kinakuza mgogoro mkubwa katika tamthilia hiyo. Katika

kukuza mjadala wa haya, tumevitumikiza vigezo alivyoeleza Laura (2016) kuhusu mgogoro kwa kuongozwa na maelezo wananadharia ya Drama.

### 3.6.1 Kichocheo cha Mhusika Mkinzani

Kichocheo cha Mwanaheri kinatokana na kile anachokithamini na kinamsukuma kutenda matendo yanayoibua mgogoro kati yake na wahusika wengine. Matendo anayoamua kutenda Mwanaheri yanawaathiri wahusika wengine hivyo kusisimua hofu ya ndani ya nafsi zao jambo linalosababisha kuwepo kwa mgogoro. Mwanaheri anaonekana kama anayethamini sana mapenzi. Wanapofunga ndoa na Bukini, Mwanaheri anaonekana mwenye wasiwasi kutokana na mpango wa Bukini kwenda ng'ambo. Kwa kuwa anathamini sana uhusiano wao wa kimapenzi, hamtaki Bukini awe mbali na upeo wa macho yake. Hili linadhihirika waziwazi kutokana na kauli ya Mwanaheri ya hofu ya kuachwa Bukini aondokapo. Anasema;

MWANAHERI: M'kshafika huko ng'ambo huko
Mnatusahau, siyo huku (uk.1).

Kauli hii inadhihirisha kuwa Mwanaheri anathamini sana kuwa karibu na mchumba wake. Nia yake ni kuwa wawe pamoja katika ndoa wala sio kutenganishwa na umbali. Hatimaye, Bukini anapoenda ng'ambo, Mwanaheri anaishia kupoteza anachokithamini na kushindwa kustahimili hali ya upweke. Hili linamchochea kuchukua uamuzi wa kuingia katika mahusiano mengine ya kimapenzi na Ali kudhihirisha namna anavyothamini kuwa karibu na mchumba wake. Hatua hii anayoichukua inamweka hatarini kwa kuwa ni kinyume na maadili ya jamii yake. Kwa kujua kuwa ameenda kinyume na maadili ya jamii yake, anaamua kuuweka uhusiano huu wa kimapenzi kuwa siri. Mgogoro unazuka baina yake na Ali wakati Ali anamtembelea bila kutoa taarifa

mapema na kuhatarisha kugundulika kwa uhusiano wao. Mwanaheri anaonekana kugadhadhabishwa na hatua hiyo anaposema;

MWANAHERI: Mimi nimekwambia usije hapa
Akituona-
ALI: S'kiza.
MWANAHERI: Nis'kize nini?
ALI: Shhhh.
Polepole.
MWANAHERI: Nis'kize nini?
Akituona-
ALI: Ulikwenda hospitali?
MWANAHERI: *(Anaitikia.)*
ALI: Ehe?
MWANAHERI: We nenda (uk. 21).

Kutokana na dondoo hili, mgogoro kati ya Ali na Mwanaheri unazuka kwa sababu ya uamuzi ambao Mwanaheri anauchukua wa kujihusisha katika mahusiano ya kimapenzi yasio halali. Kunatokea majibizano kati yake na Ali kwa sababu Ali hajui hatari ambayo mahusiano yao yanaweza kuwasongomezea. Kauli ya Mwanaheri: "we nenda" inaashiria tahadhari anayochukua ili wasije wakafumaniwa na Shangazi.

Zaidi ya hayo, uamuzi huu aliouchukua Mwanaheri wa kuingia katika uhusiano wa kimapenzi nje ya ndoa unamtia katika hatari kubwa zaidi anapoambulia ujauzito. Hili linakuza mgogoro mwingine mkubwa kati ya Mwanaheri na Shangazi yake. Shangazi anapogundua kuwa Mwanaheri ni mjamzito, anaamua kumdadisi ili ajue mwanaume anayehusika na ujauzito huo. Katika kufanya hili, mgogoro mkubwa unazuka kati yao unaoishia katika Shangazi kumpiga Mwanaheri. Mgogoro huu unadhihirika kupitia majibizano yao yafuatayo;

MWANAHERI: Sina haja ya kukataa
Cha kukataa nini?
*(Anampiga)*

SHANGAZI: Wewe unaweza
kunijibu
ufedhuli namna hii?... (uk. 24).

Dondoo hili linadhihirisha mgogoro mkali baina ya Mwanaheri na Shangazi yake kutokana na kitendo cha Mwanaheri kuenda kinyume ya maadili ya jamii yake. Habari za Mwanaheri kupata ujauzito nje ya ndoa zinaonekana kumghadhabisha sana Shangazi na kuamua kumzomea Mwanaheri hadi kuishia kumpiga.

### 3.6.2 Mtagusano wa Mhusika Mkinzani na Wahusika Wengine

Beegle (2015) anaeleza kwamba, Mhusika mkinzani anapotagusana na wahusika wengine anakuza mgogoro kwa njia moja au nyingine. Mkinzani anaweza kutagusana na wahusika wengine kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja. Katika tamthilia ya *Arusi*, Mwanaheri amewasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa hivyo mtagusano wake ni wa njia ya moja kwa moja. Mtagusano huu wa moja kwa moja unatuonyesha matendo yake pamoja na mazungumzo yake na wahusika wengine anaotagusana nao na namna yanavyokuza mgogoro. Anatagusana na Ali moja kwa moja Kichochoroni na kumweleza kuhusu hali yake ya ujauzito. Mwanaheri anapomtajia Ali kuhusu ujauzito wake, anasisimua hofu ya Ali jambo linalomfanya kuhisi kuwa wametenda kitendo haramu katika jamii. Mgogoro unazuka kati yao kuhusu namna jamii itakavyolichukulia swala hili la uhusiano haramu utakaoleta kuzaliwa kwa mwanaharamu katika jamii. Vilevile mgogoro zaidi kati yao unahusu hali itakavyokuwa Bukini arudipo kutoka ng'ambo.

ALI: Na akirudi?
MWANAHERI: Sijui wala sitaki
kujua hivi sasa.
ALI: Hutaki kujua?

vile vile kuwa
Mtaani ishaenea?
MWANAHERI: Acha ienee… (uk.41).

Mgogoro huu unaishia katika kutoelewana ambapo Mwanaheri anaamua kuondoka maeneo yale. Mwanaheri hajali namna jamii itakavyochukulia ujauzito wake nje ya ndoa naye Ali anaonekana mwenye wasiwasi mno. Mwanaheri anakatiza mgogoro huu anapoamua kuondoka. Anasema;

MWANAHERI: Mi nakwenda
ALI: Sasa unakwenda!
… Namna…
vipi?
MWANAHERI: Naona mazungumzo yetu hayafiki mahali. (uk. 41).

Mbali na hayo, Mwanaheri anatagusana na Shangazi nyumbani moja kwa moja na kuchochea mgogoro baina yao. Namna Mwanaheri anavyomjibu Shangazi inasisimua hasira ya shangazi na kuchochea mgogoro mkali kati yao.

MWANAHERI: Sina haja ya kukataa
Cha kukataa nini?…
SHANGAZI: Wewe unaweza kunijibu
Ufidhuli namna hii
basi siyo mimi
Huyo huyo mumeo
Kwangu mimi utashika
Adabu yako, ala! (uk. 24).

Nia ya Mwanaheri ni kutaka kumfahamisha Shangaziye kuwa tayari maji yameshamwagika na hayawezi kuzoleka tena. Anataka shangazi alichukulie swala la ujauzito wake kama swala lisiloweza kufichika tena wala kufutika. Ijapokuwa kitendo hicho ni kinyume na maadili ya jamii yake, Mwanaheri anakikubali na kumtaka kila mmoja kukikubali ndiposa anamjibu Shangazi kuwa hana sababu ya kukataa.

### 3.6.3 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Ploti ya *Arusi*

Katika kuelezea Ploti ya tamthilia, unajikita kwenye kiini cha mgogoro, kukua kwa mgogoro, kilele chake na suluhisho lake. Ili kuyafafanua haya, kielelezo cha piramidi ya Freytag kimetuongoza kuelezea nafasi ya Mwanaheri katika ukuzaji wa ploti ya *Arusi*.

Sehemu ya utangulizi kulingana na Freytag (1863; 1997) kwenye umbo lake la piramidi imetuelekeza katika kufahamu utambulisho wa wahusika, uhusianao baina yao na visa vyao vya awali. Pia, utambulisho wa kuanza kujengeka kwa mgogoro umebainika. Mtunzi anatambulishia wahusika wakuu; Mwanaheri na Bukini ambao wamo katika uhusiano wa kimapenzi. Mgogoro wa kimsingi unaanza kujengeka wakati Mwanaheri anaanza kulalamikia mpango wa Bukini wa kuenda ng’ambo. Hiki kinakuwa kichocheo cha uamuzi wa matendo yanayofuatia ya Mwanaheri.

Utata kama sehemu ya pili kwenye piramidi ya Freytag, unatuelekeza kwenye vikwazo anavyokuza Mwanaheri ambavyo vinachochea mgogoro katika drama. Kitendo cha Mwanaheri kuenda kinyume na maadili ya jamii yake na kujihusisha katika mapenzi na Ali kinajenga kikwazo kikubwa baina yake na wahusika wengine. Shangazi ndiye anayeathirika na kikwazo hiki kwani kwake, Mwanaheri amemletea yeye na jamii yake aibu kubwa sana. Kitendo hiki kinasisimua hofu ya Shangazi na kuamua kumdadisi Mwanaheri.

Kilele cha mgogoro mkuu katika tamthilia ya *Arusi* kinafikia wakati Shangazi anampiga Mwanaheri kutokana na kitendo chake haramu. Shangazi anapomdadisi Mwanaheri

kunatokea majibizano ambayo yanaishia katika shangazi kumpiga Mwanaheri. Yafuatayo ni majibizano baina yao.

SHANGAZI: Sasa utanitajia
Jina la huyo mwanaume wako
Nani?
Utaniambia leo au haramu…
*(Shangazi anampiga Mwanaheri)* (uk. 35).

Sehemu inayofuata ni ya mshuko ambapo suluhisho la mgogoro kati ya Mwanaheri na shangazi linaanza kupatikana. Mama Mwanaheri anaingilia kati mgogoro huu na kumushtumu Shangazi kwa kumpiga Mwanaheri. Kitendo cha Shangazi kumpiga Mwanaheri kinasisimua hisia za hasira za Mama Mwanaheri na kumtaka Shangazi akome kabisa kumpiga mwanawe hadi anakuwa tayari kurudisha mahari waliyopewa.

MAMA MWANAHERI: Sasa hivi na aachwe
Hatujashindwa sisi
Na mahari tutayarudisha (uk. 28).

Hatua ya Mama Mwanaheri kuingilia kati na kutuliza joto la mvutano kati ya Mwanaheri na Shangazi inaonyesha kuanza kupatikana kwa suluhu la mgogoro. Wote wanaonekana kukubali kuwa maji yaliyomwagika hayawezi kuzoleka tena kwani tayari mimba ya Mwanaheri imeshakuwa bayana.

Sehemu ya mwisho ya piramidi ya Freytag ni kiliwazo. Hatima ya matendo inaonekana katika sehemu hii ambapo Mwanaheri anaonekana aliyeshinda katika uamuzi wake aliochukua licha ya kuwa ulikuwa nje ya maadili ya jamii. Anaonekana kuushinda mgogoro aliouanzisha na kupata utulivu hatimaye. Mwishoni mwa mchezo Mwanaheri anamrudishia Bukini pete aliyomvika ishara ya kuondoka katika ndoa yao na kuwa huru kufunga ndoa ingine na Ali.

BUKINI: Mbona unaivua?
MWANHERI: Mchezo si umekwisha?
BUKINI: A -a –a- a vaa-
MWANAHERI: Haha!

**3.7 Hitimisho**

Sura hii imeshughulikia ufafanuzi wa dhana ya mgogoro na aina mbalimbali za migogoro. Imebainika kuwa kuna mgogoro baina ya mhusika na nafsi yake, baina ya mhusika binadamu na mhusika mwingine, baina ya binadamu na maumbile ya ulimwengu, baina ya binadamu na malimwengu na baina ya binadamu na jamii. Mbali na hayo, mambo mbalimbali yanayochochea mgogoro yamejadiliwa. Uchunguzi na uchanganuzi wa mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro kwa kuongozwa na vipengele mbalimbali viliyowekwa bayana na Laura (2016) umetekelezwa. Vipengele hivi ni pamoja na kichocheo cha mhusika mkinzani, matatizo anayozua, mandhari anayoumba, matagusano wake na wahusika wengine na ukuzaji wake wa ploti kwa ujumla. Haya mambo yanaonesha kuwa huyu ni mhusika muhimu na anachangia pakubwa katika muundo wa tamthilia teule na pengine tamthilia zozote zile. Sura ifuatayo imeshghulikia maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthlia teule.

# SURA YA NNE

# MAUDHUI YANAYOIBULIWA NA MHUSIKA MKINZANI KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA EBRAHIM HUSSEIN

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilishughulikia mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Sura hii nayo imejikita kwenye kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Kama ilivyofafanuliwa awali, maudhui ni ujumbe unaojitokeza katika kazi za kifasihi. Katika tungo za kisanaa, mtunzi hataji maudhui moja kwa moja bali huyawasilisha kupitia vyombo vya kuwasilishia ujumbe ambavyo ni wahusika. Haya hubainika kupitia kwa mazungumzo, matendo na hata kinachosemwa na wahusika wengine au msimulizi kuhusu mhusika fulani. Hivyo basi, katika sura hii tumetathmini matendo, mazungumzo na maelezo kuhusu mhusika mkinzani na kuweka bayana maudhui yanayojitokeza kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia.

## 4.1 Mhusika Mkinzani na Ukuzaji wa Maudhui

Mbatiah (2011) anafasili maudhui kama jumla ya maswala yanayoshughulikiwa katika kazi yoyote ya fasihi. Kwa upande mwingine, Njogu na Chimerah (1999) wanafafanua dhana ya maudhui kama mawazo ya mtunzi kwa mkabala wa muktadha fulani. Kwa ujumla maudhui ni jumla ya mawazo, maswala au ujumbe wa mtunzi ambao hujitokeza katika kazi ya fasihi. Maudhui hayatajwi au kuzungumziwa moja kwa moja na mtunzi bali hubainika kupitia vyombo vya kuwasilishia ujumbe wa kisanaa yaani wahusika. Gultom (2022) anaeleza kwamba ili kuelewa maudhui mhakiki anapaswa kwanza

kuelewa vipengele muhimu kama hisia, usemi na matendo ya wahusika. Katika sura ya pili, utafiti umefafanua kuwa hisia za ndani humsukuma mhusika kutenda matendo fulani. Ni kupitia matendo hayo ndipo tunafahamu ujumbe (maudhui) unaojitokeza.

Mhusika mkinzani anapotenda matendo yanayodidimiza juhudi za nguli au yanayoenda kinyume na maadili ya jamii yake, huibua ujumbe muhimu. Zaidi ya hayo, mhusika huyu anapokuza mgogoro katika drama hadhira hupata ujumbe kutokana na migogoro hiyo. Ni kutokana na haya ndipo Gultom anasema kuwa kazi ya drama sio tu msururu wa matendo bali ujumbe madhubuti unaojitokeza. Kwa kutathmini haya, msomaji anapata mawazo ambayo aliyadhamiria mtunzi katika kazi husika.

Mbali na hayo, Gultom (2022) anaelezea kipengele cha matendo ya mhusika. Katika drama, wahusika wengine au msimulizi husema kuhusu matendo ya mhusika fulani. Haya hujitokeza aghalabu wakati mhusika mkinzani amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Kinachosemwa kuhusu mhusika mkinzani wa aina hii kinaweza kufichua ujumbe muhimu kama vile kero lake, matamanio yake, hisia zake na hata sifa zake kwa ujumla. Hili humpa mhakiki ujumbe fulani kumhusu mhusika huyu. Hivyo, utafiti umeyatathmini haya kuhusu mhusika mkinzani ambaye amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa katika tamthilia za *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini* na kuweka bayana maudhui anayoibua. Naye mkinzani katika *Arusi* ambaye amewasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa amejadiliwa kwa kutathmini mazungumzo yake pamoja na wanachokisema wahusika wengine kumhusu ili kubainisha maudhui anayoibua. Mchakato huu mzima umeongozwa na nadharia ya Naratolojia.

## 4.2 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Kinjeketile*

Mwananaratolojia Stanzel (1984) anaeleza kwamba msimulizi hutambulisha maudhui katika kazi ya kisanaa. Yeye huwakilisha na kuwasilisha, usemi wa mhusika, fikra zake matendo yake pamoja na mihemko yake. Kutokana na haya, mhusika fulani anavyosimulia kuhusu matendo, hisia, pamoja na nia ya mhusika mwingine, maudhui anayoibua mhusika mrejelewa huibuka. Tumetathmini wanachokisema wahusika wengine kuhusu Mjerumani, yaani; matendo yake, hisia zake na nia yake na kubainisha maudhui anayoibua.

Zaidi ya hayo, Griffith (2010) anasema kuwa maudhui huwasilishwa kupitia vipengele mbalimbali vya kisanaa vikiwemo wahusika. Wahusika wanatumiwa na mtunzi kama vyombo vya kuwasilishia ujumbe. Mwananaratolojia huyu anazidi kufafanua kwamba, kupitia usemi wa wahusika, fikra na matendo yao, msomaji ataweza kupata maudhui aliyodhamiria mtunzi kuyawasilisha. Kutokana na haya, usemi na matendo ya Mjerumani pamoja na vibaraka wake umetathminiwa na kuweka bayana maudhui wanayoibua.

### 4.2.1 Dhulma na Unyanyasaji

Kulingana na Young 2011, dhulumu ni kitendo cha kuonea, kunyanyasa au kumnyan’anya mtu kilicho chake. Ni kitendo cha kumnyima mtu haki, raslimali na hata fursa muhimu. Anazidi kusema kuwa vitendo hivi viwili; dhulma na unyanyasaji huenda sambamba katika matumizi yake. Katika tamthilia ya *Kinjeketile*, Mjerumani pamoja na vibaraka wake wamewatendea Wamatumbi vitendo visivyo vya haki

vilivyojaa dhulma na unyanyasaji. Kutokana na wanachosema wahusika wengine kuhusu matendo ya Mjerumani, pamoja na usemi wa vibaraka wake, dhulma na unyanyasaji imejitokeza kwa namna mbalimbali. Mjerumani anawanyang'anya Wamatumbi ardhi yao na kuanzisha ukulima wa pamba. Anawalazimisha Wamatumbi kufanya kazi katika mashamba yao huku mazao ya pamba yakipelekwa Ujerumani. Mkichi anadhihirisha haya anaposema;

> MKICHI: … Udongo mwekundu bado yupo nchini mwetu bado zaidi amechukua nchi yetu. Ameichukua kwa nguvu… (uk. 4).

Kitendo hiki cha Mjerumani kuchukua ardhi ya Wamatumbi kwa nguvu kinadhihirisha dhulma na unyanyasaji. Anaichukua ardhi yao kwa nguvu na kuzidisha unyanyasaji kwa kuwafanyisha Wamatumbi kazi za shokoa humo kwa lazima. Aidha, kitendo cha Mjerumani kuwadai Wamatumbi kodi ni unyanyasaji. Mjerumani anapofika Tanganyika Kusini anaanza kuwadai Wamatumbi kodi bila misingi yoyote. Hiki ni kinaya kwa kuwa Mjerumani ndiye mgeni katika nchi hii na ndiye anayestahili kudaiwa kodi. Kinyume cha haya ni kwamba, Mjerumani anapowasili ugenini anawalazimisha wenyeji kulipa kodi. Mkichi anadhihirisha unyanyasaji huu anaposema;

> MKICHI: …Anatudai sisi kodi. Sisi tuna- ntazama tu. Anatudai sisi kodi? Ilikuwa sisi tudai yeye kodi (uk. 4).

Kutokana na dondoo hili, Mkichi anaonekana kushangazwa na kitendo hiki cha unyanyasaji kutoka kwa Mjerumani cha kuwadai wenyeji kodi ilhali yeye ndiye mgeni. Anauona kuwa unyanyasaji wa hali ya juu ndiposa anawazindua wenzao kutoka usingizini ili waweze kutambua maovu haya na kutafuta mbinu ya kuyasitisha.

Zaidi ya hayo, kuna dhulma ya kimapenzi kutoka kwa Askari wa Kijerumani. Kutokana na mazungumzo ya Kinjeketile na Kitunda, dhulma ya kimapenzi na ya kijinsia

inabainika kutoka kwa vibaraka wa Mjerumani. Kauli ya Kinjeketile imetathminiwa na kuweka wazi kuwa Askari wa Kijerumani wanawachukua kwa nguvu wanawake na kuwadhulumu kimapenzi. Kinjeketile anamjibu Kitunda kwa kusema;

> KINJEKETILE: Usinidnganye huna lolote. Mtoto wako wa kike kachukuliwa kwa nguvu na askali juzi juzi, sasa wataka kulipa kisasi (uk. 25).

Kutokana na dondoo hili, Chausiku, mwanwe Kitunda ndiye aliyechukuliwa na Askari wa Kijerumani kwa ushirikiano na Mnyapala. Anachukuliwa kwa nguvu ili kutumiwa kama chombo cha mapenzi na burudani. Bi. Kitunda anadhihirisha kero lake juu ya dhulma hii kwa mwanawe anaposema;

> BI. KITUNDA: … Nnalimishwa – ndiyo. Wake zenu wanachukuliwa – ndiyo. Watoto wenu wanachukuliwa – ndiyo. Watu wa ndiyo. (uk. 9).

Haya yanaweka bayana kuwa watoto wa kike na wanawake kwa ujumla ndio wanaoathirika kwa kudhulumiwa kimapenzi kutokana na mapambano dhidi ya Mjerumani. Mjerumani na vibaraka wake wanawachukua wanawake kwa nguvu na kuwadhulumu kimapenzi kudhihirisha nguvu na mamlaka yao dhidi ya wenyeji. Mjerumani na vibaraka wanamwona mwanamke kama kiumbe dhaifu na chombo cha starehe na burudani ya kimahaba. Hii ni dhulma ya hali ya juu ya mhusika mkinzani dhidi ya jinsia ya kike.

Hali kadhalika, Mjerumani anamdhulumu Kinjeketile kwa kumkamata na kumtesa kutokana na hatua yake ya kuongoza watu kwa vita dhidi yao. Mbali na kushindwa vita na Mjerumani, Kinjeketile anakamatwa na kulazimishwa kukiri kuwa maji aliyowapa watu yalikuwa uongo. Kauli ifuatayo ya Kinjeketile inadhihirisha haya.

KINJEKETILE: Wiki baada ya kuanza vita, Wajerumani walikuja kunikamata…(uk.48).

Usemi huu umetathminiwa kuwa unaodhihirisha unyanyasaji dhidi ya wanyonge. Mjerumani anatumia mbinu ya vitisho na ya kutia woga mioyoni mwa wapinzani wake. Anapomkamata Kinjeketile kiongozi wa watu na kumtesa anafahamu kwamba ni mbinu mwafaka ya kuwatishia na kuwanyamazisha wafuasi wa Kinjeketile. Hatimaye Kinjeketile na wafuasi wake wanashindwa katika makabiliano yao na Mjerumani. Lengo la Mjerumani ni kutaka kuendelea kuwatawala huku akiwadhulumu na kuwanyanyasa ambayo ndiyo nia ya kimsingi ya mkinzani.

**4.2.2 Ukatili**

Kama ilivyoelezwa mbeleni, ukatili ni hali ya kumsababishia mtu maumivu au majeraha katika mwili ama matendo yanayoweza kumsababishia mtu mateso kwa njia moja au nyingine (Giardino, 2009). Kuna uhusiano wa karibu baina ya ukatili na dhulma bali ukatili unahusisha mapigo ya moja kwa kwenye mwili wa mtu au mnyama. Kutokana na wanachokisema wahusika wengine kumhusu mkinzani na vibaraka wake katika *Kinjeketile*, maudhui ya ukatili yanajitokeza. Wakati wa kulima katika mashamba yao, Wamatumbi wanapigwa kikatili na Mnyapala. Wanapokuwa wakilima shambani, wanasimamiwa na Mnyapala nyuma yao ambaye kazi yake ni kuwapiga. Bwana wa Kwanza analalamikia hali hii.

BWANA WA KWANZA: Kitunda aliinuka kunyoosha mgongo
Mnyapala akampiga kiboko (uk.3).

Dondoo hili linatuonyesha kuwa, Wamatumbi wanapolima shambani hawapaswi kusimama na kuvuta pumzi wala kujinyoosha. Wanafanya kazi katika mashamba yao

huku wamesimamiwa na Mnyapala, Jumbe na Kinoo. Kufanyishwa kazi ngumu huku wakichapwa ni kitendo cha ukatili.

Pia, wakati wa vita kati ya Mjerumani na makabila ya Tanganyika, Mjerumani anadhihirisha ukatili kwa kuwapiga viboko na risasi jambo linalosababisha kuuwawa kwa wengi wao. Kitunda anasema;

> KITUNDA: …Mjerumani alivulumisha kiboko
> katika ngozi nyeusi…watu wetu walizulika na lisasi
> sio wengi lakini ilinitia wasiwasi. Kalibu kufika Nzizima
> tulipoteza tena watu katika mapigano (uk. 37).

Kuwamiminia watu risasi na kusababisha vifo vya wengi ni kitendo cha ukatili. Mbali na kuwanyang'anya ardhi yao wanawapiga vitani ili waendelee kuwatawala kimabavu. Katika ukatili huu wa kuwapiga, watu zaidi ya elfu moja na mia mbili wanakufa. Kitunda anatoa ripoti hii anaposema;

> KITUNDA: …tulipoteza katika kikundi chetu watu zaidi ya elfu moja na
> mia mbili (uk.45).

### 4.2.3 Ufisadi

Ufisadi ni kupata kitu kwa kutumia nafasi au raslimali alizo nazo mtu kwa manufaa yake binafsi (Rose-Ackerman, 2016). Inahusisha hali ya kupata kitu kwa kutozingatia madili ya jamii. Katika mpango wa kutaka kuendelea kutawala, Mjerumani anazua ukinzani dhidi ya Kinjeketile na wenzake kwa kuwalipa watu (vibaraka wake) ili kupata habari muhimu. Mjerumani anapofahamu kuwa Wamatumbi na wenzao wana mpango wa kuwafurusha, wanatumia pesa kuwalipa watu ili kupata habari mhuhimu kwa lengo la kudidimiza juhudi zao. Mgindo anatuarifu haya anaposema;

> MGINDO: …Udongo Mwekundu unatoa pesa nyingi kupata habali
> (uk.7).

Aidha, Makabila ya Tanganyika Kusini kupitia kwa Kinjeketile wanafahamu fika kuwa ili kufanikiwa katika kumfurusha Mjerumani ni sharti waungane. Mjerumani naye anapogundua mpango huu anatumia pesa ili kuzuia makabila yasiungane. Huu ni ufisadi. Hili linadhihirika kupitia kauli ifuatayo;

> MKICHI: Kuna watu wanalipwa kuzuia makabila yasiungane kufanya vita (uk.7)

**4.2.4 Usaliti**

Kulingana na Smith (2021), usaliti ni ukiukaji wa kukusudia au bila kukusudia wa uaminifu baina ya pande mbili za watu au jamii. Ukiukaji huu unaweza kujitokeza kwa njia tofauti, kama vile udanganyifu, ukosefu wa uaminifu, au ufichuaji wa habari za siri. Smith anazidi kueleza kuwa hali ya usaliti inaweza kutokea katika miktadha mbalimbali, ikijumuisha mahusiano ya kibinafsi, mipangilio ya kitaaluma, au mwingiliano mpana zaidi wa jamii. Katika *Kinjeketile*, Mnyapala anawasaliti wenzake wanapopanga kuungana ili kumbandua Mjerumani nchini. Mnyapala ni kibaraka wa Mjerumani kwani anatumiwa kuzua ukinzani kwa kufanikisha malengo yao ya utawala dhalimu. Usaliti wa Mnyapala unadhihirika kupitia usemi ufuatao wa Kitunda.

> KITUNDA: …Utakachofanya, kina askali au Mnyapala kesha sikia. Tumeshikwa na njaa, na njaa hii inatufanya tuuzane. Kwa hiyo kuyapeleka mambo hayo mbio haifai. Tuna maadui na katika sisi wenyewe kuna maadui (uk. 5).

Adui mkuu wa Kinjeketile na wenzake ni Mjerumani. Ndiye wanayekabaliana naye ili kumwondoa nchini. Hata hivyo, miongoni mwao wenyewe wana maadui ambao wanawasaliti kwa mpinzani wao mkuu ambaye ni Mjerumani. Katika mipango yao ya

kuungana Mnyapala anawasaliti kwa kufichua siri zao kwa Mjerumani. Hakuna lolote wanalopanga baina yao likakosa kumfikia adui wao mkuu ambaye ni Mjerumani.

### 4.3 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani Katika Tamthilia ya *Jogoo Kijijini*

Kulingana na Mwananaratolojia Stanzel (1984) msimulizi wa nafsi ya tatu ambaye huwakilisha usemi, matendo na hisia za wahusika, huwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi. Anachoeleza msimulizi kumhusu mhusika humsaidia msomaji kutambua maudhui anayoibua mhusika mrejelewa. Maelezo ya msimulizi kuhusu matendo na mihemko ya Sesota yametathminiwa na kubainisha maudhui mbalimbali anayoyaibua.

#### 4.3.1 Mateso

Kulingana na anachoeleza msimulizi kuhusu matendo ya Sesota, utafiti ulibaini kuwa joka hili linawasababishia Wanamasononi mateso makubwa kwa njia mbalimbali. Kwanza, Wanamasononi wanapata mateso kila mwaka kutokana na kitendo cha Sesota kuvamia kijiji chao na kuchukua mali na binti mwema mmoja.

> Kwani
> ‘Likuwa tabia makini
> Killa mwaka ukabaini
> Joka kushuka kijijini
> Kuchukua mali na binti Mwema mmoya (uk. 35).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa Wanamasononi wanateseka kila mwaka kwa kupoteza mali na binti mwema mmoja kutokana na madhila ya Sesota. Msimulizi anazidi kusisitiza hali hii ya mateso anaposema;

> Maana ilikuwa dhiki
> Kitongoji hakukaliki
> Maisha yalikuwa siki
> Machungu na makali kwa kila mmoja (uk. 36).

Sesota anawaletea Wanamasononi mateso na kuwanyima raha kwa kitendo hiki haini. Anawafanya kuona kijiji chao mahali pabaya pa kuishi palipojaa mateso. Sesota anawaletea Wanamasononi mateso zaidi mbali na kuchukua mali na binti kwani anawasababishia kimbunga kikali. Maelezo fafuatayo ya msimulizi kuhusu matendo ya Sesota yanabaini ujumbe wa mateso dhidi ya Wanamasononi.

> Watoto wakaachama
> Wakaachama aaah' wakaachama
> Basi hapo hapo
> Katika kimbunga wakajikaukia (uk. 41).

Mbali na kimbunga, Sesota anapumua moto mkali ambao unateketeza vibanda, mashamba, watu na wanyama. Moto huu unapelekea kifo cha watoto na wanyama kama paka.

> Akapiga mikabi yake
> Akapumua moto wake
> Kaonyesha asili yake
> Ya ukatili usio jinsia
>
> Vibanda moto ukawaka
> Mashamba yote 'karipuka
> Watu watoto pia paka
> Walikuwa majivu rundu kubwa moya (uk.42).

Maelezo haya kuhusu matendo ya Sesota yanadhihirisha mateso ya aina mbalimbali anayowaletea Wanamasononi. Wanakadiria hasara kubwa kutokana na kimbunga kinachosababishwa na Sesota. Kando na hayo, mauti ya watoto na wanyama yanawaandama kutokana na moto anaoutema Sesota katika kijiji hiki.

Mtemi vilevile haepuki mateso kutoka kwa Joka hili wakati wa makabiliano yake nalo. Msimulizi anatueleza kuwa katika kikao cha wanakijiji wa Masononi, Mtemi anapewa jukumu la kukabiliana na joka hili. Wakati Joka hili linavamia Kitongoji cha Masononi, Mtemi anakabiliana nalo na kufanikiwa kulikata kichwa kimoja ila anapata mateso

linapomwachia sumu mwilini mwake. Mateso ya Mtemi yanabainika kutokana na usemi wa msimulizi ufuatao;

> Punde si punde
> Wak'ti si wakti
> Alibaini
> Tena alibaini
> Sumu ya Joka
> Kumbe ilibakia pale kijijini
> Mwake mwilini
> Harufu chafu na najsi ilibakia! (uk. 46).

Wanamasononi wanapata amani na uhuru Mtemi anapofanikiwa kumkata Sesota kichwa kimoja na kumtokomeza. Hata hivyo, amani hii na uhuru havidumu kwa muda mrefu kwani sumu ambayo Sesota alimwachia Mtemi mwilini inamlazimu kuenda mbali na kijiji kwa ajili ya kujitakasa. Msimulizi anaelezea hali hii.

> Kwani
> Katika mapambano na ukatili
> Nafsi takatifu najsi huingia
> Ukweli huu ulimchoma sana
> Humo rohoni ulichochota sana
> Akazingatia akazingatia na akaona
> Atafute maji ya kujitakasa (uk. 47).

Mateso ambayo Sesota anamsababishia Mtemi ni makubwa na yenye athari kubwa kwake na kwa wanakijiji. Mwili wake unaingia najisi kutokana na sumu ya Joka jambo linalomlazimu kutafuta njia ya kujitakasa. Kwa wanakijiji, athari inayowapata ni kumpoteza mwokozi wao, Mtemi ambaye alikuwa na uwezo wa kukabiliana na Sesota.

### 4.3.2 Mashaka (Hofu)

Mashaka ni wasiwasi au hofu aliyo nayo mtu kutokana na jambo fulani. Kulingana na anachoeleza msimulizi kuhusu Sesota, tunabaini kuwa ujumbe unaojitokeza ni hofu miongoni mwa Wanamasononi. Kitendo cha kuogofya cha Sesota cha kuchukua mali

na binti mwema mmoja kila mwaka kutoka kijiji hiki, kinawasababishia Wanamasononi hofu nyingi. Msimulizi anasema;

> Na killa aliyeona
> Joka hilo maluuni
> Moyo wake 'liingiwa hofu
> Na mashaka kiinsani (uk. 35).

Hofu hii ndiyo inayowapelekea kuungana ili kutafuta suluhisho na tatizo hili lao. Wanaandaa mkutano na kumteua Mtemi kama nguli atakayekabiliana na Joka hili ili wapate utulivu kijijini mwao.

Wanamasononi wanapata utulivu baada ya Mtemi kukabilina na Joka hili na kulitokomeza ila wanaingiwa na hofu nyingine ya kurudi tena kwa Sesota. Wakati wa makabiliano baina ya Mtemi na Sesota, Mtemi anafanikiwa kumkata kichwa kimoja na kumtokomeza. Hili linawaletea Wanamasononi furaha na utulivu kwani hofu yao kuu imeondolewa. Hata hivyo, wanajisahau na kuruhusu ufisadi kukita mizizi kitongojini mwao. Muda mchache baadaye, kiwingu kinaonekena kitongojini kuashiria kurudi tena kwa Sesota. Haya yanawarejeshea hofu kubwa waliokuwa nayo mwanzoni. Msimulizi anadhihirisha hofu hii anaposema;

> Tukangoja humu hofuni
> Kichwa cha pili cha Mal'uni
> Kichwa cha Sesota haini
> Mbali ukingoni kutokelezea (uk. 49).

Haya yanaweka wazi kuwa, maisha ya Wanamasononi yalikuwa katika hali ya ati ati. Tatizo ambalo lilikuwa limewasumbua kwa kipindi kirefu linapotatuliwa na Mtemi, wanapata amani na utulivu huku hofu ikijitenga nao. Hata hivyo wanajitia kitanzi wenyewe wanaporuhusu ufisadi kujipenyeza kitongojini. Hofu ya kurudi tena kwa

Sesota ni ya kutamausha kwani nguli wao wa kukabiliana na Sesota amejiondoa kwa ajili ya utakaso wa sumu aliyoachiwa mwilini na Joka.

### 4.3.3 Ubinafsi

Ubinafsi ni mtazamo wa ulimwengu unaothamini uhuru wa mtu binafsi na ambao unatetea uwajibikaji wa kibinafsi na uamuzi wa kibinafsi (Taylor, 2020). Mtazamo huu mara nyingi husababisha kuzingatia haki na uhuru wa mtu binafsi, na hutofautiana na itikadi za wanajumuiya zinazotanguliza malengo ya kikundi na maelewano badala ya matamanio ya kibinafsi. Taylor (2020) anazidi kueleza kuwa katika jamii iliyotawaliwa na ubinafsi, wahusika hujijali na kufanikisha mafanikio ya kibinafsi na kujieleza bila kujali ustawi wa pamoja wala athari itakayowapata wengine. Katika tamthilia hii, matendo anayotuelezea msimulizi juu ya Sesota yametathminiwa na kubainisha ubinafsi. Hulka hii ya Sesota ya kuchukua mali na binti mwema mmoja ni ubinafsi. Maneno ya msimulizi yafuatayo yanashadidia haya.

> Kwani
> Likuwa tabia makini
> Killa mwaka ukabaini
> Joka hushuka kijijini
> Kuchukua mali na binti mwema mmoya (uk. 35).

Kutokana na dondoo hili, hali ya kujijali inadhihirishwa na mhusika huyu Sesota. Hajali athari ya masikitiko na mashaka anayowaletea Wanamasononi. Dhamira yake ni kujinufaisha tu kwa mali na binti mwema.

### 4.3.4 Ukoloni na Ukoloni Mambo-leo

Kwa mujibu wa Ashcroft, Griffiths na Tiffin (2013), ukoloni ni utawala wa kisiasa na kiuchumi wa nchi moja juu ya nchi nyingine na aghalabu husababisha ukandamizaji wa

utamaduni wa wenyeji na unyonyaji wa rasilimali. Kwa upande mwingine, ukoloni-mamboleo ni mwendelezo wa desturi na athari za kikoloni katika muktadha wa baada ya ukoloni, ambapo udhibiti rasmi wa kikoloni umeisha lakini utawala wa kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni unaendelea. (Nkrumah, 1965).

Kwa kurejelea tamthilia hii, wataalam wengi wanafikiria ya kwamba, Ebrahim Hussein ni mmojawapo wa waandishi ambao wametumia jazanda katika utunzi wao. Wataalam hawa ni pamoja na Olali (2004), Mukobwa (1989) na Kitsao (1982). Wanasema kwamba, Hussein ametumia jazanda katika tamthilia za *Mashetani* (1971), *Jogoo Kijijini* (1976) na *Arusi* (1980). Wanazidi kueleza kuwa tamthilia ya *Jogoo Kijijini* imejengwa kwa misingi ya utawala wa ukoloni na ukoloni-mamboleo. Wakoloni walipokuja Afrika, walinyakua ardhi na mali ya Waafrika. Wilikaa Afrika kwa kipindi cha miaka karibu sabini. Waliwalimisha Waafrika katika mashamba yao huku wakiwadhulumu. Kuja kwao kuliwaletea Waafrika dhiki nyingi. Nguli wa Kiafrika walijitokeza kukabiliana na Wakoloni hao kwa njia ya vita. Wakoloni walipoondolewa, Wafrika walipata amani na utulivu. Hata hivyo, Wafrika waliingia katika ufisadi na kuwadhulumu Wafrika wenzao. Hii inadhihirisha kuwa walitoka katika utawala wa kikoloni na kupisha ukoloni-mamboleo. Hili linawapa watawaliwa hofu ya kurejea tena kwa utawala wa kikoloni.

Kutokana na haya, sehemu ya pili ya tamthilia hii inaonyesha kuwa, kupitia kwa mhusika Sesota, maudhui ya utawala wa ukoloni na ukoloni mambo leo yanajitokeza kama ifuatavyo. Kuja kwa Sesota, joka lenye vichwa sabini katika kitongoji cha Masononi ni jazanda inayowakilisha uvamizi wa Wakoloni barani Afrika na kukaa

takriban miaka sabini. Kitendo cha Sesota kuchukua mali na binti katika kitongoji hiki kinawakilisha kijazanda jinsi Wakoloni walivyochukua mali na ardhi ya Waafrika. Ikumbukwe kuwa, lugha ya Kiingereza hurejelea nchi kwa kutumia kiwakilishi cha jinsia ya kike. Hivyo basi, binti anayechukuliwa na Sesota anawakalisha nchi za Kiafrika zilizochukuliwa na Wakoloni. Mbali na hayo, Mtemi ankabiliana na Sesota. Hili igizo linaashiria Wafrika waliokabiliana na Wakoloni hadi kuondoka kwao Afrika. Kitendo cha Wasamasononi kushiriki ufisadi ni jazanda ya ukoloni-mamboleo ambapo viongozi wa Kiafrika waliifufua na kuidhibiti enzi alioiacha Mkoloni.

## 4.4 Maudhui Yanayoibuliwa na Mhusika Mkinzani katika Tamthilia ya *Arusi*

Phelan (1987) anaelezea mhusika kama mshiriki katika uigaji vilevile mwakilishi wa ujumbe fulani. Mhusika fulani anavyoiga matendo na usemi katika drama huwakilisha ujumbe fulani ambao ndio maudhui. Hivyo, kutokana na uigaji wa matendo na mazungumzo wa mhusika mkinzani (Mwanaheri) katika tamthilia hii, maudhui mbalimbali yanajitokeza. Stanzel (1984) naye anasema kwamba mhusika anaposimulia kuhusu mhusika mwingine, huwasilisha maudhui fulani yanayoibuliwa na mhusika mrejelewa. Hivyo, maelezo ya wahusika wengine kuhusu Mwanaheri yanawasilisha maudhui ambayo anaibua. Haya yote yamejadiliwa kwa kina ifuatavyo.

### 4.4.1 Ndoa

Mwanaheri anafunga ndoa na Bukini ambapo inahalalishwa na pete ambayo Bukini anamvika Mwanaheri. Bukini ana mpango wa kusafiri kuenda ng’ambo ila anamtaka Mwanaheri afahamu kuwa ndoa hiyo ni hai na angerejea baada ya miezi miwili au

angemtumia nauli ili amfikie. Kupitia mazungumzo yafuatayo baina ya Mwanaheri na Bukini tunadhihirishiwa kufungwa kwa ndoa ya wawili hawa.

BUKINI: We lete mkono kwanza
Wa kushoto. Lete wa kushoto
Haya nyosha vidole
Nyosha vidole basi
Sasa fumba macho
MWANAHERI: Nini sasa?
BUKINI: We fumba. Si utaona hapo hapo.
*(Anamvisha pete).*

Shuguli hii ya uvikwaji pete inafuatiwa na arusi kisha Bukini kuenda ng'ambo. Hata hivyo, ndoa hii haidumu kwa muda mrefu kwani Mwanaheri anakosa subira na kuanza mahusiano ya kimapenzi na Ali. Mazungumzo yafuatayo baina ya Mwanaheri na Ali yanadhihiriasha uhusiano huu.

ALI: Shhh
Polepole
MWANAHERI: Mimi nakwambia usije hapa.
Akituona-

Kutokana na mazungumzo haya, tunabaini kuwa Mwanaheri amejiondoa katika ndoa yake ya awali na Bukini na kuingia katika mahusiano na Ali. Hii sio ndoa halali inayotambulika na jamii yake ndiposa wanaiweka siri. Mwanaheri anaogopa shangazi yake kumfumania akiwa na Ali, ushahidi kwamba kitendo anachofanya na Ali ni kinyume namaadili ya jamii yake ndiposa amebainishwa kama mhusika mkinzani.

### 4.4.2 Utamaduni

King'ei (2010) anafafanua utamaduni kama tajriba maarifa, ujuzi au hekima fulani anayojifunza mtu katika jamii aishimo na kuuchukua kama mwongozo wake wa maisha. Anazidi kueleza kuwa utamaduni unaweza kujadiliwa kwa viwango mbalimbali ambavyo ni; imani, desturi sanaa, amali, falsafa vifaa, fasihi na lugha. King'ei (2010)

anafasiri desturi kuwa itikadi ambazo huwaongoza wanajamii katika maswala yao ya kila siku. Maswala haya yanahusu namna jamii fulani huendesha shughuli zao kama vile ndoa, jando, unyago, mazishi, matambiko miongoni mwa zingine. Kipengele hiki cha desturi ndicho ambacho utafiti huu umejikita kwacho kwa kurejelea maudhui ya utamaduni. Mazungumzo ya Mwanaheri na Somo wake yametathminiwa na kubaini kuwa ujumbe unaojitokeza ni wa utamaduni.

> SOMO: Tayari?
> MWANAHERI: Mi tayari
> SOMO: Haya kaa basi
> *(Mwanaheri anakaa juu ya kiti).*
> Kaa ee somo yangu. Mama we ni somo yangu.
> … Mapenzi somo yangu, hayataki
> Bayana; yanataka siri. Maisha usifanye
> kuyadhihirisha… (kur. 10-11).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa Mwanaheri anazingatia desturi ya jamii yake ambayo inamtaka mwanamwari yeyote kabla ya kufunga ndoa kirasmi lazima apate mafunzo ya somo (kungwi). Kabla ya arusi yake na Bukini, Mwanaheri anapokea mafunzo ya unyago kutoka kwa somo wake. Anafundishwa maswala ya unyumba kwa ujumla yaani namna anvyopaswa kujiedesha kama mke na namna ya kuhusiana na mumewe kimahaba. Huu ni utamaduni wa jamii yake kwa misingi ya desturi ambao hana budi kuuzingatia.

Hata hivyo, licha ya Mwanaheri kupokea mafunzo haya kutoka kwa somo, anadhihirisha ukinzani anapoenda kinyume na utamaduni huu. Punde tu baada ya kutekeleza desturi hii, anaiasi ndoa yake na Bukini na kuingia katika uhusiano haramu wa kimapenzi na Ali. Anakosa kutilia maanani maadili mema ya ndoa anayofundishwa na Somo na kuishia kuvunja ndoa yake halali.

### 4.4.3 Usaliti

Usaliti ni hali ya kuenda kinyume na mkataba au matarajio ya kimsingi ya watu (Smith, 2021). Jamii haimtarajii Mwanaheri kuenda kinyume na ndoa yake na Bukini punde tu baada ya arusi. Kitendo hiki kinafasiriwa kuwa usaliti. Bukini anamvisha Mwanaheri pete ya uchumba na kumwahidi kuwa licha ya yeye kuenda ng'ambo, angerudi baada ya miezi miwili au angetuma tikiti. Licha ya hayo, Mwanaheri anakosa subira na kuingia katika uhusiano mwingine ya kimapenzi na Ali hadi anaambulia ujauzito. Mazungumzo yafuatayo baina ya Mwanaheri na Shangazi yanadhibitisha usaliti huu.

> MWANAHERI: Sina jambo la aibu
> Wala sina jambo la kuficha.
> SHANGAZI: Unataka kunidanganya ni
> Wawe…
> Wewe
> Wewe naweza kukuzaa.
> Wima basi si Mungu
> Hakunijaalia kupata mtoto
> Wewe unaweza kukataa
> Kama huna mimba wewe?
> Unakataa?… (uk. 24).

Kutokana na dondoo hili, Mwanaheri amegundulika kuwa mjamzito na Shangazi anamtaka akiri hilo. Anachosisitiza Shangazi ni kwamba mimba hiyo si ya Bukini kwani hayupo karibu naye. Shangazi anasema;

> SHANGAZI: Na mke huyo
> Mke jina
> Maana huyo katuletea mimba sasa
> Hiyo iimejaa tele. Tuseme kuwa
> Mimba hiyo ya mtoto wetu. Hata
> siku moja (kur. 27-28).

Usaliti wa moja kwa moja unadhihirika wakati Bukini anarejea kutoka ng'ambo. Anapokutana na Mwanaheri, wanajihusisha katika mazungumzo kama wapenzi ila Mwanaheri anaishia kuivua pete na kumrejeshea Bukini.

BUKINI: Mbona unauvua?
MWANAHERI: Si mchezo umekwisha
BUKINI: A- a- a- a vaa-
MWANAHERI: Hata *(Anampa Bukini pete)*
Naogopa.

Mbali na usaliti wa kimapenzi, kitendo hiki cha Mwanaheri ni usaliti kwa jamii. Mwanaheri ameenda kinyume na madili ya jamii yake kwani hayamruhusu kuenda nje ya ndoa hasa baada ya arusi. Aidha amali za jamii yake hazimruhusu mtoto wa kike kupata ujauzito akiwa mwanamwali ambaye bado anaishi nyumbani kwao. Kulingana na jamii ya Shangazi, ujauzito halali ni ule anaoupata mwanamke akiwa ndoani. Kutokana na mazungumzo ya Shangazi, inabainika kuwa Mwanaheri kupata ujauzito haramu, ni usaliti kwa familia yake na jamii kwa ujumla. Shangazi anasema;

SHANGAZI: Ikisha kuwa mtoto
Si mtoto, Malaya
Akichukua mimba za watu akituletea humu
Nyumbani (kur. 28-29).

Kulingana na shangazi, Mwanaheri alipofunga ndoa na Bukini, alistahili kuwa mwaminifu kwake licha ya Bukini kwenda ng'ambo. Kulingana na Shangazi, kitendo cha Mwanaheri kupata ujauzito kutokana na uhusiano wake na Ali ni aibu kwa familia na usaliti kwa mumewe na jamii nzima. Katika kufanya hivyo, Mwanaheri anabainika kuwa mhusika mkinzani.

### 4.4.4 Ukatili

Kama ilivyoelezwa mbeleni, ukatili ni kitendo cha kumsababishia mtu maumivu kwenye mwili au akili. Chanzo cha ukatili katika *Arusi* ni kitendo cha Mwanaheri kuenda nje ya ndoa yake na Bukini. Shangazi anapogundua ujauzito wa Mwanaheri,

anapandwa na mori na kumpiga. Haya yanajitokeza kutoka kwenye maelekezo ya jukwaa yafuatayo;

> *(Shangazi anampiga Mwanaheri. Mwanaheri hajikingi.*
> *Anampiga mpaka anaanguka chini. Shangazi anamkalia juu.*
> *Mwanaheri anapiga ukulele- 'Aaaaaa!' Giza) (uk.25).*

**4.4.5 Siasa**

Tamthilia hii nzima ya *Arusi* inahsu ndoa baina ya vijana wawili Bukini na Mwanaheri. Hata hivyo, mhakiki anapoisoma kwa jicho la upekuzi na kwa mtazmo wa kihistoria atagundua kwamba ni tamthilia ya kijazanda inayozungumzia nchi mbili zenye mifumo tofauti na kinzani ya kiuchumi. Wahakiki wengi wa tamhilia hii wakiwemo Kitsao (1982), Mukobwa (1985) na Olali (2004) wanakubaliana ya kwamba Ebrahim Hussein alitunga tamthilia ya *Arusi* kijazanda kwa misingi ya kisiasa na kiuchumi. Kihistoria, nchi ya Kenya ilikuwa na mfumo wa uchumi wa kibepari nayo Tanganyika (kwa sasa Tanzania) ikawa na mfumo wa ujamaa kipindi cha wakoloni wa Kiingereza. Wasomi hawa wanasema kwamba Bukini ametumika kijazanda kuwakilisha mfumo wa kiuchumi wa kibepari (ulioendekezwa na Kenya) naye Mwanaheri ametumika kuwakilisha mfumo wa ujamaa (ulioendekezwa na Tanzania).

Kitsao (1982) anaeleza kuwa wakoloni wa Kiingereza walipokuja kutawala Tanganyika waliunda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kusudi lao kuu la kuiunda jumuiya hii lilikuwa kwamba iwarahisishie utawala wao wa nchi tatu za Afrika Mashariki; Kenya Uganda na Tanganyika. Mazrui (1980) anasema kuwa jumuiya hii ilivunjika mnamo mwaka wa 1976 kisha nchi ya Tanzania ikafunga mpaka wake. Kutokana na hali hii, nchi ya Kenya ilijaribu kuishawishi Tanzania kufungua mpaka wake ila juhudi hizo hazikufua dafu.

Wahakiki hawa wanasema kuwa juhudi hizi za nchi ya Kenya kujaribu kuishawishi Tanzania kufungua mpaka wake bila mafanikio zimewakilishwa kijazanda na Bukini kumshawishi Mwanaheri wafunge ndoa bali jaribio hilo linagonga mwamba. Hivyo, Mwanaheri amekuza maudhui ya siasa kwa misingi hii kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Zaidi ya hayo anazua ukinzani kijazanda kwa kukataa muungano wa mataifa ya Kenya na Tanzania.

## 4.5 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia maudhui yanayokuzwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Aidha, mtafiti amejadili dhana ukuzaji wa maudhui na mhusika mkinzani. Sehemu ya mwisho imehusisha tathmini ya maudhui ambayo yamekuzwa na mhusika mkinzani kwa mujibu wa nadharia ya Naratolojia katika tamthilia zote tatu teule.

Maudhui ambayo yameibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia ya *Kinjeketile* ni ukatili, ufisadi, usaliti pamoja na dhulma na unyanyasaji. Aidha, maudhui ambayo yameibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini* ni mateso, mashaka, ubinafsi na ukoloni na ukoloni mamboleo. Kisha, katika *Arusi* mkinzani ameibua maudhui ya usaliti, ukatili, ndoa, utamaduni na siasa. Inajitokeza wazi kwamba mhusika mkinzani ameibua maudhui hasi katika tamthilia zote tatu teule.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilishughulikia maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Sura hii inahusu muhtasari wa matokeo na mapendekezo ya utafiti. Imegawika katika sehemu tano; muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, changamoto za utafiti, na mapendekezo kuhusu utafiti unaoweza kufanywa baadaye.

## 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Mtafiti alikuwa na malengo matatu ambayo alipania kuyatimiza. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein; *Kinjeketile, Jogoo Kijijini* na *Arusi*. Nalo la pili likawa kuchunguza namna mhusika mkinzani anavyokuza mgogoro katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein; *Kinjeketile, Jogoo Kijijini* na *Arusi*. Lengo la tatu lilihusu kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein Hussein; *Kinjeketile, Jogoo Kijijini* na *Arusi*. Tamthilia hizi ziliteuliwa kwa mbinu ya kimaksudi ambapo mtafiti alikusudia kuchunguza namna ambavyo mhusika mkinzani husawiriwa kama mhusika aliyepo na asiyekuwepo kwenye jukwaa. Tamthilia ya *Arusi* iliteuliwa kuchunguza sura hii ya mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa. Kwa upande mwingine, tamthilia ya *Kinjeketile*

na ya *Jogoo Kijijini* ndizo zilizoteuliwa kuchunguza mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa.

Tasnifu hii imewasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza ilishughulikia sehemu ambazo ziliupa msingi utafiti wetu. Sehemu hizi ni pamoja na usuli wa mada ambao ulifafanua dhana ya mhusika mkinzani kwa upana. Pia, suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti vilishughulikiwa. Sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka pamoja na tahakiki kuhusu mada viliangaziwa. Nadharia mbili zilizoongoza utafiti huu zilijadiliwa; Naratolojia na nadharia ya Drama. Zaidi ya hayo, mbinu za utafiti zilishughulikiwa pamoja na maadili ya utafiti.

Sura ya pili ilishughulikia ubainishaji wa mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Sura hii ilianza kwa kuangazia namna maisha ya mtunzi wa tamthilia teule yanavyoibua muktadha wa ukinzani. Kisha, sehemu iliyofuata ikafafanua sura ambazo mhusika mkinzani huweza kuwasilishwa nazo. Isitoshe muhtasari wa tamthilia teule ulitolewa pamoja na ufasiri wake kisha kufuatiwa na utambuzi wa mhusika mkinzani katika kila tamthilia. Sehemu ya mwisho ya sura hii ilihusisha mjadala kuhusu mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia.

Sura ya tatu ilichunguza namna mhusika mkinzani amekuza mgogoro katika tamthilia teule. Sura hii ilianza kwa kufafanua dhana ya mgogoro na aina zake kwa mujibu wa wataalamu mbalimbali. Sehemu iliyofuata iliangazia namna ambavyo mhusika mkinzni hukuza mgogoro katika tamthilia. Hatimaye, sura hii ikakamilishwa na uchunguzi wa

mhusika mkinzani na ukuzaji wa mgogoro katika tamthilia teule kwa kuongozwa na nadharia ya Drama.

Sura ya nne ilijihusisha na tathmini ya maudhui mbalimbali yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Dhana ya maudhui kwa mujibu wa wataalam mbalimbali imeelezwa. Aidha, mtafiti alifafanua namna ambavyo mkinzani hukuza maudhui katika kazi za kisanaa. Hatimaye, maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule yalijadiliwa kwa kuongozwa na nadharia ya Naratolojia.

Mwishowe, sura ya tano imeshughulikia hitimisho la utafiti mzima.  Hitimisho hili limehusisha kutoa muhtasari wa sura zote zilizomo katika utafiti. Pia linajumuisha matokeo ya utafiti kwa mujibu wa malengo, changamoto zilizokumba utafiti kwa ujumla na mchango wa utafiti. Sura hii imekamilika kwa kutoa mapendekezo kuhusu tafiti zinazoweza kufanywa na watafiti wengine katika siku za baadaye.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti kwa Mujibu wa Malengo

Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Hapa, utafiti ulitambua kuwa, mhusika mkinzani katika tamthilia ya *Kinjeketile* na *Jogoo Kijijini* amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa. Katika tamthilia ya *Arusi*, mhusika mkinzani amewasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa. Utafiti uligundua kwamba, mhusika mkinzani anapowasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa, husawiriwa kwa upekee fulani ikilinganishwa na namna anayosawiriwa kama aliyepo kwenye jukwaa.

Katika tamthilia ya *Kinjeketile*, mhusika mkinzani alibainika kuwa Mjerumani. Amekuza ukinzani katika tamthilia hii kutokana na namna wahusika wengine wanavyoeleza kuhusu matendo yake na vilevile kupitia vibaraka wake. Usawiri wake ni wa kipekee kutokana na sura aliyowasilishwa nayo ya kutokuwepo kwenye jukwaa. Amesawiriwa kupitia njia isiyo ya moja kwa moja ambayo imeelezwa kwa mbinu ya kuwatumia wahusika wengine. Kutokana na mbinu hii, Mjerumani amesawiriwa kama fisadi, katili, mnyanyasaji, na mwenye maarifa.

Pia, imebainika kwamba, Mjerumani ana wafuasi wake (vibaraka) wanaoungana naye kufanikisha ukinzani dhidi ya Kinjeketile na wenzake. Vibaraka hawa ni Myapala na Afisa wa Kijerumani ambao wanatumiwa na Mjerumani kudidimiza juhudi za Kinjeketile na wenzake kuikomboa nchi ya Wamatumbi. Kutokana na ushirikiano wao na mkinzani (Mjerumani), utafiti umewaangazia kama wakinzani vilevile na kugundua kuwa wamesawiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Njia yenyewe imeelezwa kupitia mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na ya kinatiki. Mbinu hizi walizosawiriwa nazo zimetuwezesha kubaini kuwa Myapala amesawiriwa kama katili na mwenye tamaa naye Afisa wa Kijerumani kama mwenye hila.

Katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini*, mtafiti aliangazia sehemu ya pili ya tamthilia hii na kubaini kuwa, mhusika mkinzani ni Sesota, joka lenye vichwa sabini. Analeta ukinzani kutokana na namna msimulizi anavyoelezea kuhusu matendo yake. Utafiti umetambua kuwa Sesota amesawiriwa kwa njia ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja ambazo zimefafanuliwa kupitia mbinu ya kimaelezo na ya ulinganuzi na usambamba. Kutokana na mbinu ya kimaelezo, imebainika kuwa Sesota amesawiriwa kama fisadi,

maluuni, hayawani, haini, mwenye hamaki na mwenye kisasi. Mbinu ya ulinganuzi na usambamba nayo imetuwezesha kubaini kuwa Sesota ni mwenye kutisha.

Katika tamthilia ya *Arusi*, utafiti ulitambua kuwa Mwanaheri ndiye mhusika mkinzani kwa kuwa ameenda kinyume na maadili ya jamii yake. Mwanaheri analeta ukinzani kutokana na matendo yake hasi na namna anavyozungumza moja kwa moja na wahusika wengine katika drama. Utafiti vilevile uligundua kuwa Mwanaheri amesawiriwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Njia yenyewe imeelezwa kupitia mbinu ya kuwatumia wahusika wengine na ya kinatiki. Kutokana na mbinu ya kuwatumia wahusika wengine, Mwanaheri amesawiriwa kama msaliti. Kwa upande mwingine kupitia mbinu ya kinatiki, Mwanaheri amesawiriwa kama msiri, muongo na mwenye kutojali.

Lengo la pili lilikuwa kuchunguza namna mhusika mkinzani anavyotumiwa na mwanafasihi kukuza mgogoro katika tamthilia teule. Utafiti uligundua kuwa mhusika mkinzani huwa na msukumo fulani wa ndani ya nafsi ambao humchochea kutenda matendo yanayokuza mgogoro na wahusika wengine. Mhusika mkinzani hukuza mgogoro katika tamthilia kutokana na kichocheo cha matendo yake, mandhari anayoumba, mtagusano wake na wahusika wengine, matatizo anayowasababishia wahusika wengine na nafasi yake katika ukuzaji wa ploti.

Imebainika kuwa kichocheo cha matendo ya mkinzani kinatokana na kile anachokithamini ambacho humsukuma kutenda matendo fulani. Katika kutenda matendo hayo, kunatokea kutoelewana (mgogoro) baina ya yake na wahusika wengine. Pia, matatizo ambayo mkinzani anawasababishia wahusika wengine huwachochea

kutafuta mbinu ya kukabiliana nayo. Katika kufanya hivi, mgogoro unaibuka baina yao. Hili limedhihirishwa katika tamthilia ya *Kinjeketile* ambapo Mjerumani anawaletea Wamatumbi na wenzao matatizo mengi yakiwemo njaa, utozwaji wa kodi, dhulma na unyanyasaji miongoni mwa mengine. Haya yanawasisimua Wamatumbi na wenzao kuingia katika mgogoro wa kivita na Mjerumani ili kumbandua nchini mwao. Kutokana na sura aliyowasilishwa nayo Mjerumani, anatagusana na wahusika wengine kupitia vibaraka wake ambao anawatumia kudidimiza juhudi za kivita dhidi yake. Kwa kutenda hivi vibaraka hawa wanawatendea wahusika wengine vitendo viovu vinavyokuza mgogoro baina yao.

Kwa upande mwingine, matendo ya mkinzani katika *Jogoo Kijijini* yanaelezwa na msimulizi na kudhihirishwa namna yanavyowachochea Wanamasononi kuingia katika mgogoro wa kivita naye. Katika *Arusi*, mkinzani anatagusana na wahusika wengine moja kwa moja kupitia matendo na mazungumzo yake nao. Kitendo cha Mwanaheri kuenda kinyume na maadili ya jamii yake, kinachochea mgogoro kuzuka kati yake na wahusika wengine kama Shangazi, Ali, na Bukini.

Pamoja na hayo mtafiti ametumia piramidi ya Freytag kuelezea nafasi ya mkinzani katika ukuzaji wa ploti. Imebainika kuwa katika kuelezea ukuaji wa ploti, mgogoro hushughulikiwa moja kwa moja kwa sababu hivi ni vipengele viwili vinavyotegemeana na kukamilishana. Katika tamthilia tatu teule, imebainika kuwa mkinzani ndiye chanzo cha kuwepo kwa mgogoro katika drama na anachangia katika ukuaji wake, kilele na mshuko.

Lengo la tatu lilihusu kutathmini maudhui yanayoibuliwa na mhusika mkinzani katika tamthilia teule. Utafiti uligundua kuwa mtunzi huwatumia wahusika kama vyombo vya kuwasilishia ujumbe. Katika kazi za kisanaa, ujumbe huu ndio maudhui. Zaidi ya hayo utafiti uligundua kuwa iwapo mkinzani amewasilishwa kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa, basi wanachokisema wahusika wegine au msimulizi kumhusu ndicho hutathminiwa ili kubainisha maudhui anayoibua. Kwa upande mwingine, iwapo mhusika mkinzani amewasilishwa kama mhusika aliyepo kwenye kwenye jukwaa, basi matendo na mazungumzo yake ndiyo hutathminiwa ili kubainisha maudhui anayoibua.

Kutokana na hayo, katika tamthilia ya *Kinjeketile*, tulitathmini walichokisema wahusika wengine kumhusu Mjerumani na kubainisha maudhui mbalimbali anayokuza. Maudhui haya ni pamoja na; ukatili, ufisadi, dhulma na unyanyasaji. Pia tulitathmini usemi na matendo ya vibaraka wa Mjerumani na kubainisha maudhui ya usaliti, ukatili, na tamaa.

Katika tamthilia ya *Jogoo Kijijini* tulitathmini anachokisema msimulizi kuhusu matendo ya Sesota na kubainisha maudhui mbalimbali. Maudhui haya ni pamoja na; mateso, mashaka (hofu) na ubinafsi. Zaidi ya haya, kwa kuongozwa na tahakiki za wataalam wa awali kuhusu tamthilia hii, utafiti uligundua kuwa mhusika Sesota amewasilishwa kijazanda kuwakilisha maudhui ya ukoloni na ukoloni mamboleo. Ametumiwa na mtunzi kuwakilisha utawala wa wakoloni waliofahamika na unyakuzi wa ardhi. Haya yamedhihirishwa katika tamthilia kutokana na matendo yake ya kunyakua mali na binti katika kijiji cha Masononi.

Katika tamthilia ya *Arusi*, matendo na mazungumzo ya Mwanaheri (mkinzani) yalitathminiwa na kubainisha maudhui mbalimbali. Maudhui haya ni pamoja na ndoa, utamaduni, usaliti na ukatili. Pia kwa kuongozwa na watafiti wa awali kuhusu tamthilia hii, tulibaini kuwa Mwanaheri alitumiwa kijazanda kukuza maudhui ya siasa. Ndoa yake na Bukini ambayo haikutengemaa inawakilisha namna jumuiya ya Afrika Mashariki ilivyoundwa lakini jaribio hili likagonga mwamba.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa utakuwa wa manufaa kwa wasomi kwa kuwafahamisha na mbinu mbalimbali za usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia kwa ujumla. Vilevile, utafiti huu umeliziba pengo lilioachwa na tafiti za awali zilizoegemea kwenye aina zingine za wahusika wakiwemo watoto, wa kike, wa kiume, walemavu miongoni mwa wengine na kuzungumzia kwa uchache mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa.

Kwa kuzamia kwenye mkinzani, utafiti unatarajiwa kuwafaa watunzi wa tamthilia kuwa kuwafahamisha kuwa wanaweza kumuwasilisha mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa na kuwa kiini cha ukinzani. Vilevile utawaonyesha umuhimu ya kumuumba mhusika mkinzani katika tungo zao kwa kuwa ndiye anayejenga migogoro na taharuki hivyo kufanya maigizo kuvutia.

## 5.4 Changamoto Zilizokabili Utafiti

Zipo changamoto kadha wa kadha zilizokumba utafiti huu. Kwanza, kwa kuwa utafiti huu ulikuwa wa maktabani, kuliibuka tatizo la uhaba wa vitabu na majarida ya marejeleo mwafaka ya Kiswahili. Hili lilimlazimu mtafiti kutegemea kusoma vipengele

faafu kutoka lugha za kigeni hasa Kiingereza na kuvitafsiri. Miongoni mwa vitengo vilivyohitaji utafsiri ni nadharia kwa kuwa nadharia ya Naratolojia na ya Drama ni za kigeni. Kama inavyofamamika utafsiri hukumbwa na tatizo la kupotea kwa sehemu fulani ya maana ya awali basi hili likawa tatizo kwa mtafiti.

Mbali na hayo ugeni katika kutalii swala la mhusika mkinzani katika tamthilia ulimletea mtafiti changamoto za kupata marejeleo mwafaka. Hii ni kwa sababu tafiti za awali kuhusu mhusika zilifanywa kwa kujikita kwa aina zingine za wahusika kama vile wahusika watoto, wa kike, wa kiume na walemavu.

## 5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa mhusika mkinzani katika tamthilia teule za Ebrahim Hussein. Ulijikita kwenye utanzu wa tamthilia pekee na kujihusisha na aina moja ya mhusika yaani mkinzani. Pendekezo kwa watafiti wa baadaye ni kuwa, wanaweza kutafiti kuhusu usawiri wa mhusika mkinzani katika utanzu wa riwaya ama hadithi fupi au wakaangazia aina zingine za wahusika kama vile nguli au bapa.

Mbali na hayo, utafiti huu ulishughulikia mhusika mkinzani kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa katika tamthilia mbili na mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa katika tamthilia moja. Hata hivyo mtafiti hakuegemea kwenye kulinganisha sura hizi mbili za mhusika mkinzani katika tathilia teule. Kutokana na hili, watafiti wa siku za usoni wanaweza kushughulikia kulinganisha na kulinganua usawiri wa mhusika mkinzani kama mhusika aliyepo kwenye jukwaa na kama mhusika asiyekuwepo kwenye jukwaa.

**MAREJELEO**

Abrams, M. H. (1999). *A glossary of literary terms* (7th ed.). Harcourt Brace College Publishers.

Ackenman, J. (2022). *The dynamics of literary conflict: A comprehensive analysis*. Cambridge University Press.

Arege, T.I.M. (2012). Naration in Swahili Narrative Poetry: An Analysis of Utenzi wa Rasi ʼLghuli. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Aristotle (1920*). The Poetics*. Oxford: Clarenton press.

Ashcroft, B., Griffiths, G., & Tiffin, H. (2013). *The empire writes back: Theory and practice in post-colonial literatures* (2nd ed.). Routledge.

BAKIZA (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Bakize, L. H. (2021). Usawiri Chanya wa Watoto katika Fasihi ya Watoto kama Njia Faafu ya Kujenga Jamii Bora ya Leo na Kesho: Mifano Kutoka Vitabu Teule vya Watoto vya Kiswahili. *Jarida La Mnyampala*, 2, 83-94.

Barasa, J.M. (2013). Mtindo Katika Watu wa Gehana. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Barthes, I. (2001). *Literary Theory: The Basics*. New York: Routledge.

Beegle, J. (2015). The melancholy villain: An examination of the character of Don John in Shakespeare's *Much Ado About Nothing. CLA Journal Vol. 3, pp.1-10.*

Betti, M.J. (2015). *An Introduction to Drama*. PhD Thesis, University of Thiqar. (Unpublished).

Bloom, H. (1997). *Anxiety of Influence: A Theory of Poetry*. USA: OUP.

Bowen, K.D. (2003). Usawiri wa Wahusika Watoto katika Tamthilia Zilizopendekezwa katika Shule za Upili: *Visiki* na *Amezidi.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Bradford, R.F. (1992). *Tales From 1001 Arabian Nights.* Mumbai: Jaico Publishing House.

Carlson, S.D (2016). *Absent Characters: Stage Space and Social Change in Modern Drama.* Thesis of the Bestowal of Honours in the Major. (Unpublished).

Chatman, S. (1978). *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca, New York: Comell University Press.

Elam, K. (1980). *The structure of drama: A study of dramatic form and development*. Routledge.

Freytag, G., 1997 (1863). Die Technik des Dramas. In: H. Garland, & M. Garland (eds), *The Oxford Companion to German Literature*, edition 3. Oxford: Oxford University Press.Geertz, C., 1973. Cultures: selected essay. New York: Basic Books.

Garcia, J. (2024). *Conflicts in literary works: An analytical framework*. University Press.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse.* Ithaca: Comell University Press.

Giardino, A.P. (2009). Introduction: child abuse and neglect: *A Practical Guide to the evaluation of child physical abuse and neglect*, 3-30.

Gosling, S. D. (2008). *Personality and individual differences: The science of personality and its applications*. Sage Publications.

Griffith, K. (2010). *Writing Essays About Literature*. Cengage. Wadsworth Publishers.

Gultom, F. E. (2022). The Relationship Between Theme and Characters in Fiction Movie *Inside Out. BAHAS journ. Vol. 33. No. 1*. Universities Negeri Medan.

Haji, A.V. (2018). Kutathmini Mbinu za Usawiri wa Wahusika katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu*: Utafiti Linganishi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa).

Hammood, N.A., Mahmood, S.D., & Hashim, M.R. (2020). "The Offstage Character in Modern American Drama: Sam Shepard's Burried Child." *International Journal of Aplied Linguistics and English Literature* 9, no. 4 (2020): 117-124.

Hussein, E. (1967). *Alikiona*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1967). *Wakati Ukuta*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini* na *Ngao ya Jadi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1980). *Arusi*. Nairobi: Oxford University Press.

Hussein, E. (1988). *Kwenye Ukingo wa Thim*. Nairobi: Oxford University Press.

Hutcheon, L. (2000). *A Theory of Parody: The Teachings of the grotesque in the arts*. University of IIIinois Press.

Jameson, F. (2005). *Archaeologies of the future: The desire called utopia and other science fictions*. Verso.

Jung, C. G. (1964). *Man and  his Symbols*. Aldus Books.

Kanwa, O. (2022). Usawiri wa Wahusika wa Kiume katika Riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na Wanawake. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Keen, S. (2003). *Narrative Form*. London: Macmillan.

King'ei, G. K. (2010). *Msingi wa Isimujamii*. TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dar es salaam.

Kitali, H.N. (2011). Fani na Usawiri wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia ya *Pango* na *Mama ee*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: University of Nairobi Publishers.

Kitsao, J. (1982). An Investigation of Themes in Swahili Literature and an Application of Stylostatistics to Chosen Texts. A PhD Thesis from the University of Nairobi. (Unpublished).

Kott, J. (1990). *Shakespeare our contemporary*. Harcourt Brace Jovanovich.

Laura, R. (2016). *Read, Talk and Write: 35 Lessons That Teach Students to Analyse Fiction and Nonfiction*. Corwin Publishers.

Madsen, D. L. (2009). *The modern gothic and literary doubles: A study of the uncanny*. Palgrave Macmillan.

Mahfouz, S.M. (2012). The Presence of Absence: Catalytic and Omnipresent Offstage Characters in Modern American Drama. The Midwest Quarterly; Pittsburg Vol. 53, Iss. 4, (Summer 2012): 392-409,312,316.argolin, U. (1983). *Characterization in Narrative: Some Theoretical Prolegomena*. Neophilogogus.

Mazrui, A. (1980). *The African Condition: A Diagnosis*. Cambridge: Cambridge University Press.

McKee, R. (2020). *Story: Substance, Structure, Style, and the Principles of Screenwriting*. HarperCollins.

Mdee, N.W. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21.* Longhorn Publishers.

Moige, F. O. (2015). Usawiri wa Watoto Katika Riwaya za Kisasa za Kiswahili Zilizoandikwa na Muhamed Suleiman Muhamed na Euphrase Kezilahabi. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa).

Morrow, S.E. (2009). Absent Characters as Proximate Cause in Twentieth Century American Drama. [Masters Thesis, Georgia State University] doi:https://doi.org/10.57709/1059514

Mukobwa, J.N.M. (1985). Maendeleo ya Kimaudhui Katika Tamthilia Tano za Ebrahim N. Hussein. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkrumah, K. (1965). *Neo-colonialism: The last stage of imperialism*. International Publishers.

Oiko, E.G. (2017). Uhakiki wa Mtindo katika Tamthilia za Arege. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maasai Mara. (Haijachapishwa).

Okwena, S. (2019). Umahuluti wa Miundo katika Tamthilia za Ebrahim Hussein. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Olali, J. A. (2004). *Ebrahim Hussein and the evolution of Tanzanian drama*. East African Educational Publishers.

Oluoch, G.S. (2020). Migogoro ya Kisaikolojia katika Riwaya za *Mkama Ndume* na *Unaitwa Nani?* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijahapishwa).

Phelan, J. (1987). *Character Progression and the Mimetic-Didactic Distinction. Modern Philology.*

Plato. (1930).*The Republic, Books 1 to 5 trans. P. Shorey.* Cambrigde: Havard University Press.

Polti, G. (1921). *The thirty-six dramatic situations.* (L. E. E. W. de B. Thompson, Trans.). The Dramatic Publishing Company.

Ponera, A. S (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi.* Dar esalam: Karljamer Print Technology.

Propp, V. (1968). *Morphology of the Folktale*. University of Texas Press.

Raglan, L. (1956). *The Hero: A Study in Tradition Myth and Drama*. New York: Vintage Books.

Ricard, A. (2000). Ebrahim Hussein: Swahili Theatre and Individualism. Dar es Salaam: Mkuki wa Nyota Publishers.

Rimmon – Kenan, S. (1983).*Narrative Fiction*. London: Methuen& Co. Ltd.

Rose-Ackerman, S. (2016). *Corruption and government: Causes, consequences, and reform*. Cambridge University Press.

Rosefeldt, P. (2002). From Stage Interlude to Strange Snow: A Study of the Absent Character in Drama. *A Journal of Evolutionary Psychology* pp 117+. Institute for Evolutionary Psychology Publications.

Senkoro, E.M.K. (2011). *Fasihi.* Dar esalam: KAUTTU Ltd.

Shivaughn, K.M (2022). The Madwoman as Antagonist in English Gothic Fiction. Masters Thesis, University of Alberta, (Unpublished).

Smith, J. (2021). *The psychology of betrayal: Understanding trust and loyalty in relationships*. Academic Press.

Spector, J. (1973). *The Aesthetics of Freud: A Study in Psychoanalysis and Art.* New York: Praeger Publishers.

Stanzel, F. (1984). *A theory of Narrative*. London: Cambridge University Press.

Taylor, C. (2020). *Sources of the self: The making of the modern identity*. Harvard University Press.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Msingi na Vipengele Vyake.* Nairobi Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.

Yazdan, K. (2008). *An Introduction to Immigration and Exile Literature*. Tehran: Cheshmeh Publication.

Young, I. M. (2011). *Justice and the politics of difference*. Princeton University Press.